


# EP EBOOKS

THIS DDOCUMENT IS TRACKED, DO NOT SHARE

# NGUVU ZA SINDANO

## na Hadithi Nyingine

**Wahariri**
**Kaka FRED**
**Samwel OLUOCH**

**© KITOVU CHA HADITHI 2021**

Haki zote zimehifadhiwa. Ni marufuku na hatia kwa wenye silika za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya waandishi kupitia kwa wakili wao.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume cha sheria ataweza kushtakiwa.

**ISBN 978-9914-40-200-1**

---

**Imechapishwa kwa mara ya kwanza 2021 na Elong'o Publishers.**

**NGUVU ZA SINDANO**
**Na Hadithi Nyingine**

**Wahariri**
Kaka Fred: +**254716349065**
Baruapepe: kakafred25@gmail.com
Samwel Oluoch: +**254725658938**
Baruapepe: mwalimusammy7@gmail.com

# DIBAJI

Maisha ni mshumaa uso na mkesha. Unapoishi ishi maisha ya fawaishi kulingana na uhuru na uwezo wako. Kila mbwa ni mfalme katika himaya yake. Je, utapa tuzo ipi unapoinjikia mwenzio nyama? Kisasi hakilipi! **NGUVU ZA SINDANO** na Hadithi Nyingine ni antholojia ya kipekee iliyotalii katika nyanja zote za uhalisia wa jamii ya leo. Umeshuhudia insi wengine wakiuana madhila kisasi? Hadithi zote zimehaniki masuala yanayofanyika katika kizazi hiki cha wanaleo na mazingira yake. Waandishi wametupa mbinu chanya za kuepuka sampuli ya visa hivi. Maudhui mengine kama: masuala ibuka, ufisadi, udhalimu, nidhamu na mengine yamekusanywa na kuwekwa kwenye chombo kimoja. Kazi kwako msomaji.

Antholojia hii imepaliliwa na waandishi kutoka janibu tofauti tofauti hapa Kenya. Tamathali yametumika vyema ili kumkuza msomaji kwa maneno mapya yatakayoujenga ukwasi wa lugha na mazungumzo yake. Ama kweli, mwana mtamba kule humshinda mzee wa kale.

Isake antholojia hii uonje mapishi yenye virutubishi vyote vitakavyokuacha na afua njema katika umilisi wa Lugha ya Kiswahili. Usiteme utamu, chambilecho Kaka Daniel Siwa

**Kaka Fred**
Mhariri mkuu,
KITOVU CHA HADITHI.
1/6/2021

# VISA VILIVYOMO


DIBAJI ........................................................ 3
KIMBUNGA na Wepoh Wesah ........................................................ 5
NGUVU ZA SINDANO na Kaka Fred ........................................................ 12
PESA NYEUSI na Hector Mbati ........................................................ 19
ALIPORUDI na Samwel Nyongesa ........................................................ 24
TUNDU LA TAMAA na Vitalis Nadecho ........................................................ 30
ELIMU YA SUMU na Kamoti A. Nalianya ........................................................ 34
PANG'OKAPO JINO na Onkoba Humphrey ........................................................ 38
YAKIJA NAYATWAE na Kaka Maina ........................................................ 43
MALI YA UMANDE na Patrick Mukanga. ........................................................ 48
TUMAINI na Amos Khayota ........................................................ 51
BONDE LA MASIKITIKO na Mwalimu Sammy ........................................................ 55
MTINDI WAMPONDA na Moses Odongo ........................................................ 61
KILIMA CHENYE BUBUJIKO LA MOYO na Washington Bin Juma ........................................................ 65
DAWA YA MAKOVU na Moses Nawale ........................................................ 72
KILEMA CHA MUNGU KINA MWENDOWE na Elizabeth Barasa ........................................................ 77
SHEREHE. ........................................................ 84

# KIMBUNGA na Wepoh Wesah

*School of Oriental and African Studies (SOAS)* ni taasisi ya utafiti wa lugha Uingereza. Huko ndiko matilaba ya Mwenyezi yalikuwa yamemfikisha Uwepo Uwezo. Kesho atasajiliwa katika Kitivo cha Sanaa kusomea shahada ya uzamifu katika Ushairi mkongwe. Alipachikwa lakabu hiyo, *Uwepo Uwezo*, kutokana na uzoefu wake wa kusema hivyo kila wakati mambo yalipoonekana kwenda mvange, jina lake, Riki Arzaki, likafifia. Babake mzazi alifariki akiwa kikembe cha umri wa mwaka. Amepitia awamu ngumu sana katika maisha kweli, Mungu si Athumani. Uwepo alikikagua chumba ambacho kingekuwa mastakimu yake kwa miaka mitatu mtawalia. Aliporidhika, aliketi kitandani kuisoma Biblia kabla ya kulala. Ghafla, kumbukumbu za awali zikamrudia.

Uhusiano kati ya Uwepo Uwezo na Fatimata Matabu haukumjua kuwadi wala mshenga. Waliuzua wenyewe. Uwepo alipoiona tu picha yake mtandaoni, alinaswa kwa wajihi wake. Akamuomba usuhuba, naye akaridhia. Pupa ya kutaka kuwa na mke ikamtia msukumo kupanga miadi. Alikuwa mkomavu aliyewahi kuwa katika ndoa mbili zilizosambaratika. Wakaa waliokubaliana kukutana ulipaswa kuwa saa nane za mchana katika mkahawa wa *The Bliss* mjini Soko Mjinga. Uwepo hakufaitika. Alipawahi mahali hapo. Akajinunulia nakala ya jarida la *Mulika, Juzuu namba 16.* Alipoingia mkahawani, alichagua meza akahakikisha ameketi mkabala na lango ili atakapowasili Fati, macho yake yasimrubuni. Akasubiri.

Kila alipomwona msichana mwenye ngozi nyeupe, pumzi zilimwenda mbiombio. Wakati mwingine angeinuka tayari kumpokea hadi alipohakikisha siye, kwa kukosa kurudishiwa tabasamu. Mwendo wa saa moja jioni, Fati aliwasili akiandamana na vijana wawili aliowatambulisha kama Gad na Weba, binamuze. Ngozi yake ilikuwa laini sana, rangi ya maji ya kunde. Waliposalimiana, Uwepo aliajabia wororo wa vitanga vyake. Ungedhani ni vya mtoto aliyezaliwa. Hakuwahi kuonja sulubu za maisha huyu Fati. Vazi lake tu ndilo lililokuwa na walakini. Uwepo hakupenda sketi fupi! “Huyu ndiye Riki Arzaki, bwanangu,” akasema. Gad na Weba hawakusema lolote. Waliinuka na kumpa mkono Uwepo. Alishtuka kuitwa *“bwanangu”* kwani ulikuwa ndio mwanzo kukutana na Fati. Aliomba kuwaagizia kinywaji. “Kawaida” “*Captain Morgan”*, akadakia Fati. Mara iyo hiyo chupa kubwa ya mvinyo na gilasi nne zikaletwa. Uwepo alijua bei ya vileo. Aliinamisha kichwa chake akatafakari.

Fati alitoa kizibo na kuumimina kwenye gilasi zao isipokuwa ya Uwepo aliyeagiza soda aina ya *Sprite*. Walinyanyua gilasi zao na kuzigongesha pamoja polepole wakitamka kwa kauli moja, *"Cheers."* Weba alionja tu kiungwana na kutulia. Aghalabu wageni hao wangetoka nje kwa zamu kuongea kwa simu. Kwa Uwepo, lilikuwa jicho tu. Alikuwa makini kugundua kuwa walikuwa na msimbo wao wa mawasiliano. Mathalani, Gad baada ya kuwasiliana kwa simu aliwatangazia wenziwe kwamba *Raishaba imeiva*, nadhani kumaanisha, "Biashara imenoga". Wote watatu wakazikunja ngumi za mikono yao ya kulia na kuzigongesha pamoja jinsi walivyozifanya gilasi za pombe, ila mara hii badala ya kusema *"Cheers"*, kila mmoja aliishia kukigonga kifua chake mwenyewe mara mbili, kana kwamba alijitanua kwa kusema "Ni mimi".

Saa mbili unusu, Gad aliomba kuondoka na mwenzake, Weba. Wakaenda zao. Fati alimuomba Uwepo anunue chupa nyingine. Uwepo aliitikia. Fati akaiweka mkobani mwake kisha na wao wakaondoka kuenda kwa Uwepo. Fatimata hakuonyesha hisia zozote walipoingia chumbani. Alijipweteka kochini na kuomba maji ya kunywa. Uwepo alimpa maji baridi naye pia akaketi mkabala wake na kutaka kujua zaidi kumhusu Fatimata, almaarufu Fati. Akawa mwepesi wa kumjibu maswali yote aliyoulizwa. Kwa muhtasari, Fati alikuwa kitindamimba katika familia ya watoto wanane. Alizaliwa katika kitongoji cha Sitabicha karibu na mlima Masaba. Kitembo chake kimasomo ni cheti cha kidato cha nne baada ya kuzunguka katika shule nne kutokana na alichokiita *Kuonewa na walimu wa kike*. Tumaini lake ni kujiunga na chuo kikuu apate shahada, bora isiwe ya ualimu. Hakuchukua cheti chake cha kidato cha nne kutokana na kisaa cha karo. Uwepo aliridhika na maelezo hayo lakini akabaki kuwaza kama angeweza kugharimia maisha yake Fati. Ni siku ya kwanza lakini tayari alikuwa amehisi uzito wa kulipia vinywaji ghali pamoja na nauli. Fati hakuogopa sifa za kulala kwa Uwepo licha ya wao kukutana kwa mara ya kwanza.

Asubuhi waliondoka. Fati aliabiri daladala ya kumfikisha kwao Sitabicha, naye Uwepo akaenda masia kuelekea shuleni alikofunza. Waliahidiana kukutana tena mwendo wa saa tisa alasiri. "Mzungu" kwelikweli! Saa tisa kamili akawasili na begi kubwa mgongoni. Baada ya kulitua sakafuni, wakakumbatiana kwa muda mrefu.

Miezi tisa mtawalia walisukuma gurudumu la maisha. Uwepo akaona amepata utulivu moyoni mwake. Alipanga safari ya kwenda kujitambulisha kwa

wazaziwe Fati. Aliandamana na marafiki wake wawili. Walipokuwa huko, waliajabia umati uliofika kuhudhuria hafla hiyo. Ajabu zaidi ni kwamba hakuna yeyote aliyezungumza chochote kuhusu ndoa yao. Alipotaja jina "Fatimata", nyuso za watu zilionyesha taharuki. Kumbe hakujulikana hivyo, aliitwa Aderobi! Ilivyo desturi, akawaachia wazaziwe bahasha zao na kuwaaga.

Asubuhi siku iliyofuata, Fatimata akarejea. Alikuwa mlevi. Akajipweteka kochini na kuwasha sigara aliyoitoa mkobani mwake. Aliivuta. Uwepo hakuficha rangaito yake. "Mke wangu, kulikoni?" Fati hakujibu, aliendelea tu kwa starehe zake. Uwepo kwa kutotaka mvurugano, aliondoka na kuelekea Sokomjinga ili apitishe wakati.

Aliporudi alimkuta Fati akijishughulisha kuandaa chajio. Chumba amekinadhifisha. Hofu ya kuishi kama mseja ilichangia pakubwa kupalilia subira aliyokuwa nayo Uwepo. Alichelea vicheko kutoka kwa majirani na wenzi wake. Alitaka kuishi tu katika asasi ya ndoa kama binadamu wengine. Hakusema lolote wala kuonyesha hisia zozote. Alihofia sintofahamu. Fati aliendelea na mazoea ya kujitenga apigapo simu au kuipokea. Jioni moja alitoka nje kwa pupa kupokea simu. Baada ya kipindi kirefu alirudi ndani ya nyumba akitokwa na machozi. "Naondoka sasa hivi", akaanza. "Nimepokea mwito wa dharura niende katika Hosipitali ya wilaya ambako amelazwa wifi, alienda kujifungua". Hakusubiri jibu kutoka kwa mumewe. Akachukua manukato na kujifukiza. Akaondoka na kumwacha Uwepo kinywa wazi.

Alirauka asubuhi kwenda kazini. Aliporejea alasiri akafululiza moja kwa moja hadi chumbagonezi. Fati alikuwa amelala fofofo. Mseto wa uvundo na harufu kali ya vileo ulihanikiza. Uwepo alitiririkwa na machozi. Akajituma sokoni kwa Mfalme, mradi apate kubarizi na kupunga upepo. Alirejea jioni na kulala kochini, raghba ya malaji imemkwepa. Asubuhi ilipofika walitazamana tu kana kwamba hakukuwa na la mno. Maisha yakaendelea. Jumamosi moja mafunguliang'ombe, mlango wa nyumba yao ulibishwa kwa njia hafifu. Fati akawahi kuufungua. Kisha akaenda kumuamsha Uwepo kwa maneno, "Tuna mgeni." Uwepo alimkuta Weba, yule binamu mpole na mnyamavu. Uwepo akaelekea hamamuni. Aliporejea chumbani, alimkuta akinawa uso na kujipodoa. Kumbe sherehe ilikuwa ianze asubuhi hiyo! Fati alimwambia Uwepo avae kisha awakute katika kilabu kilichoko hapo karibu kiitwacho "KWA RAHA ZAKO". Akaandamana na Weba.

Baada ya kujikwatua alienda kujiunga nao. Aliwakuta wamejibanza pembeni mwa ukumbi. Hakukuwa na mazungumzo mengi katika kikao chao.

Fati alimuagiza hadimu aandike chakula mezani. Aliitikia. Akarejea na sinia kubwa iliyojaa vipande vya kuku na sima. Wote watatu wakala shibe yao. Weba akamtaka Uwepo amruhusu kutumia simu yake. Akajitenga kwa mawasiliano. Aliporejea, alimkabidhi Uwepo simu yake na kuomba kuondoka. Waliposalia wawili, Fati na Uwepo walitawaliwa na kimya kirefu chenye mshindo mkubwa. Kisha Uwepo akamuuliza Fati, “Ulisema mna uhusiano gani na Weba?” “Yeye ni mwana wa wifi wa shangazi yangu, ni binamu.” Uwepo alionekana kuwa na tashwishi na jibu hilo. Mhudumu aliwaletea ankra. Baada ya Uwepo kuikagua, akatoa shilingi elfu nne mia sita na kugharimika. Wakaondoka na kuelekea chumbani mwao. Saa mbili kasorobo, Uwepo alipokea simu kutoka kwa nambari ambayo hakuitambua. Ilikuwa sauti ya kiume. “*Hello*? Unamfahamu Weba? Ulikuwa naye mwisho saa ngapi?” “Naam, saa tano mchana?” “Huyo Weba amekufa." “Ameteketezwa na umati,” akasema na kukata simu. Alipomfahamisha Fati alionekana mwingi wa hofu. Akamuomba Uwepo asithubutu kulitaja jina la Weba popote! Uwepo alijaribu kujikaza lakini alimshuku Fati. Jioni moja Uwepo alishikwa na msokoto wa tumbo na kuhisi uchungu uliokithiri tumboni, sehemu ya chini ya kitovu chake. Hakufaitika, akawahi kwenda zahanatini ili aweze kugangwa. “Kisonono! Ulitembea kiholela," ndivyo alivyosema tabibu. Uwepo alibaki kuduwaa. Biwi la simanzi likamgubika. “Nina mke, wala sijawa mzinzi wa kuchuma kisonono mie,” alitamka. “Basi kakuchumia yeye”, akajibu daktari. Akamhesabia vidonge vya kumeza pamoja na maagizo ya kufuata yeye na mkewe. Baada ya kisa, mkasa. Fati alienda kumzuru dadake, Karoli. Mumewe alikuwa askari. Aliporejea, alikuwa na simu mpya muundo wa *OPPO*.Hakusema alivyoipata. Jumapili, saa tano asubuhi. Askari waliubisha mlango wake. Waliandamana na mwanamume mmoja njorinjori na mwanamke aliyetiririkwa na machozi. “Yu wapi Nancy?” Akauliza Greg, mmoja wa askari hao. Fatimata kusikia sauti, alijitokeza mwenyewe kutoka chumba cha kulala. “Kuja na hiyo simu”, akaamrisha Greg. “Afande, kuna shida?” Uwepo akauliza. “Kidogo tu, itakwisha,” alijibiwa.

Uwepo alimwuliza Fati, “Hawa ni kina nani?” "Mimi ndiye ninayewajua”, akajibu Fati na kuandamana nao. Alipowafuata hadi kwenye kituo cha polisi, Uwepo alimaizi kwamba mwanamume huyo mrefu ndiye aliyekuwa mwenye simu. Aliishi karibu na Karoli dadake Fati. Fati alimpora simu wakiwa katika harakati za ulevi na mapenzi haramu! Mradi simu ilikuwa imepatikana wageni hao hawakuwa na budi kurudi makwao. Ilibidi Uwepo agharimike kumnunulia

Fati uhuru wake kwani kwao, mkono mtupu haulambwi. Akatoa shilingi elfu nane pesa taslimu. Fati alifululiza hadi chumbani.

Aliporudi alimpata Fati akiwa mlevi chakari. Chupa mbili kubwa za mvinyo zilikuwa mezani ila hazikuwa na pombe. Alipoboboka, kujaribu kutembea, alianguka kwenye sakafu na kulala. "Huyu ni nani hasa? Nancy? Aderobi au Fati? Tutashirikiana kuujenga mustakabali wetu kweli?" Akiwa katika lindi la mawazo, aliamua kumpigia simu Karoli angaa apate kumsaili. Akafanikiwa kumpata kwa simu. Kwa mujibu wa Karoli, Aderobi alikuwa na taksiri. Alikuwa kiberenge asiyejali afya wala usalama wake. Anatagusana kiholela na waja wa sampuli zote. Aila yao haina uhusiano wowote wa kiukoo na marehemu Weba wala Gad anayetajwa. Ufunuo huu ulikuwa kama dhoruba kwa Uwepo. Alibaki kaduwazwa asiwe na la kuamba. Alibaki katika hali hiyo kwa muda mrefu hadi alipogutushwa na usiahi mkubwa kutoka kwa Fati. Aligaragara sakafuni akilia huku akiminyaminya tumbole na kutiririkwa na kijasho. Aliinuka kwa shida akamimina maji kutoka kibuyuni na kuyanywa kwa pupa. "Nipeleke hospitalini." Na kweli alikuwa hoi! Uwepo hakusita. Alipohakikisha kuwa Fati alikuwa salama mikononi mwa matabibu, alirudi nyumbani akalala. Mawio yalimkuta hospitalini minghairi ya idhini kutoka kazini. Daktari akamwongoza hadi wodi ya akina mama kujifungulia. Huko alimkuta Fati akiwa amevalia sare ya hospitali iliyompwaya.

Alikuwa amelala chali, katulia tuli. Daktari akamwashiria kutazama mvunguni. Uwepo pumzi zikamkanganya na kumwenda mbiombio. Kijusi! Nusra apige usiahi. "Tulia," daktari akamrai huku akimshika mkono. Uwepo akamshikilia daktari begani na kumwomba watoke nje. Walifululiza hadi ofisini mwa daktari huyo, wakaketi mkabala. "*Tell me the genesis of all these*." akaanza Uwepo. Daktari akamkagua kwa macho kisha akasema, "This is abortion." "Induced or spontaneous?" akauliza Uwepo. "Induced", akadakia daktari. Uwepo aliangema. Hakutaka tena mjadala zaidi. Alitaka kutoka katika mazingira hayo. Alikuwa ameingiwa na mzizimo wa hofu. "*Bili*?" akauliza Uwepo. "Sitini na nne alfu," akamjibu daktari.

Haikuwa hoja, mradi alikuwa na kadi ya Bima ya Hospitali ambayo ingemsaidia kugharimia. Baada ya kukamilisha shughuli, Uwepo alilipia teksi wakarudi nyumbani. Alirudi sokoni akanunua matikiti, maparachichi, mananasi na ndizi. Akamwekea Fati mezani karibu na kitanda kisha akaelekea kazini. Alitamani ukiwa. Akaingia katika ofisi ya Idara ya Kiswahili. Sudi ni kwamba hamkuwa na mtu. Akaukomelea mlango na kuketi kitini. Alijihisi mwele.

Alihofia angepatwa na shinikizo la damu au msongo wa mawazo. Akazama katika tafakuri. Alikumbuka yote ambayo ameyapitia tangu alipokutana na Fatimata.

Aliwaza. “Ni mwanamke au jini huyu? Nikizidi kuwa na saburi nitaweza kuyafikia matarajio?” Alikumbuka alivyompata Fati akiwa amelala, mlevi chakari! Alikumbuka Fati alivyomwachia upweke akisingizia kupokea mwito wa dharura kwenda hospitalini ili kumhudumia wifi akijifungua. Alikumbuka fedheha ya mkewe kuandamwa na kupatwa na simu ya wizi. Alikumbuka kisonono, akashika tama. Alikumbuka gharama zote, zote hadi hii ya kulipa sitini na nne alfu, kwa sababu ya Fati! Alitamauka. Atasubiri hadi Fati apate afueni kisha itabidi wazungumze. Ama akubali kufungua ukurasa mpya wa maisha au aridhie kuandikiwa talaka.

Aliporejea chumbani jioni hiyo, alimkuta mwanamke wa umri wa makamo hivi, aliyejitambulisha kama Moraa, shogake Fati. Alikuwa amepika sima kwa samaki wakawa wanakula na Fati. Alipokuwa tayari kuondoka, Fati alihiari kumsindikiza, mbali na kwamba hakuwa amepata nafuu. Alikawia sana kabla ya kurudi chumbani. Uwepo alipoonyesha kutoridhika, Fati alimtolea macho na kumkaripia. Akamwambia ilibidi awe mwanamume, akome kujidukiza kwa mambo ya wanawake. Uwepo alifadhaika. Akamwomba radhi. Chumba kikatawaliwa na ukimya wa ajabu hadi wawili hao walipoenda kulala.

Juni tarehe kumi na nne itasalia kama kovu lisiloweza kupona. Fati alitaka shilingi elfu mbili ili asukwe nywele. Uwepo akamtolea elfu tatu. Asukwe nywele kisha anunue chakula. Alipofika tu shuleni, kinara wake akamjuza kwamba ilibidi asafiri hadi jimbo la Uasin Gishu katika Shule ya Wasichana ya Kebenet. Huko angetoa mhadhara kuhusu ushairi, fani ambayo alikuwa amebobea. Alimjuza mkewe kupitia kwa simu kisha akaenda. Ilikuwa shughuli ya siku nzima, hivyo alirudi sokoni Kwa Mfalme mwendo wa saa tatu usiku. Kulikuwa na kiza katika chumba chake. Akamulika kwa mwanga wa rununu yake ili kuhakikisha kwamba hakukosea chumba. Kilikuwa chake, nambari nne mlangoni. Akausukuma mlango polepole na kubonyeza swichi ili kusambaza umeme. Hamkuwa na kitu chochote sebuleni! Akajitoma katika chumba cha kulala. Kulikuwa na kitanda tu, bila malazi! Ukutani katika msumari kulining’inia kanga moja mpya kabisa yenye maandishi “Umdhaniae ndiye kumbe siye”.

Akakadiria hasara aliyokuwa ameipata: Kochi, runinga, mtambo wa muziki, zulia la Uajemi, mapazia pamoja na picha zote za mapambo. Hata suti!

Suti ya mshono wa kipekee ambayo aliwahi kuivaa mara moja tu, kisha akaikunja vizuri na kuiweka kwa ajili ya hafla muhimu. Uwepo aliwaza. Kumbe mjo wa Fati haukuwa wa kawaida? Amemtendea magube tumbi nzima! Kimekuwa kipindi cha mpito wa upepo mkali, upepo wa kusababisha hasara isiyokadirika. Dhoruba hasa. Alipokumbuka kwamba alikuwa ameweka vyeti na stakabadhi zake zote katika hifadhi ya mamake mzazi, "Alhamdulilahi" nyingi zilimtoka kinywani.

Yamkini Uwepo alibaki katika lindi la fikra kwa kipindi kirefu kwani alipoufungua mlango, nje kulikuwa kumepambazuka. Jirani mmoja kwa jina Stella, ambaye pia alikuwa shogake Fati alikuwa amesimama huko nje. Alipomuona Uwepo, Stella alitabasamu, kisha kama aliyejizungumzia mwenyewe akasema, "Ni kama alihamia kwa Moraa". Akaingia katika chumba chake. Hiyo ndiyo iliyokuwa mara ya mwisho kwa Uwepo Uwezo kusikia habari kumhusu Fatimata Matabu. Uwepo aligutuka ghafla akakumbuka yuko ughaibuni. Kesho atasajiliwa rasmi katika chuo maarufu ulimwenguni, *SOAS*, ili kuzama katika shahada ya uzamifu. Amelenga mbele, haangalii tena ya gubeti. Akawaza: Nitakapokuwa nikisoma nitaandika kitabu. Naam, nitaandika kitabu chenye anwani "KIMBUNGA". Aliifungua Biblia yake akaisoma. Akasujudu na kusali, kisha akalala.

| **Jitathmini** |
|---|
| a) *Taja madhara yoyote matano yanayotokana na ukosefu wa uaminifu katika familia.* |
| b) *Eleza kwa ufasaha ufaafu wa anwani KIMBUNGA kwa mujibu wa hadithi uliyoisoma.* |
| c) *"Uwepo ni mvumilivu." Fafanua kauli hii kwa kurejelea hadithi hii.* |

# NGUVU ZA SINDANO na Kaka Fred

Chimbuko lake lilisalia kitendawili kwa wengi. Kichwa chake kilifurika busara na hekima. Baadhi ya wakazi walimwona kuwa punguani huku wengine wakikisia kuwa ulemavu wake wa akili ulitokana baada ya wavyele wake kumtupa akiwa mchanga. Mzee Fichua hakuwa mpiga mtindi. Alipata umaarufu kutokana na uganga wake wa kiasili. Watoto wenye umri mdogo walimpenda sana labda kwa vitushi vyake. Wengine walimnunulia pipi na peremende, vyote vyenye umbo la mduara na kumpa. Alivipenda sana vimumunyi hivyo.

Mzee Fichua alikuwa mtu wa watu. Hakukosa matangani wala harusini au kwenye hafla za michango. Hakupewa mialiko asilani labda ungejiuliza alifikaje kule? Ndilo lililokuwa swali la kila mmoja aliyemwona. Mavazi yake ya mavani yalitisha. Nywele za vunga zilikamilisha umbo la wajihi upande wa juu. Mkononi hakukosa mkongojo uliompa kazi kila jua lilipochomoza. Badala ya kujisetiri nao, yeye aliuweka mabegani akitembea huku akiimba nyimbo za mtindo wa *zilizopendwa*. Wakati mwingine mkongojo huo ulitumika kama silaha alipokuwa msituni akitafuta dawa za wateja wake. Kichwani, shumburere ilishika hatamu huku kandambili zikishika doria miguuni. Hayo hayakukamilisha sura yake, mkononi alivalia pambo kubwa la Timbi huku kigesi kikitawala miguu yake. Shingoni, hakukusazwa. Mkufu mrefu ulitalii hadi kifuani. Ilisemekana kuwa mkufu huo alipewa na babu yake. Mzee Fichua alikuwa mtu wa kutisha, endapo ungemwona kwa mara ya kwanza. Wenye ugonjwa wa '*Siri*', walifanikiwa kupona kutokana na ugwiji wake kwani alikuwa mzuza shupavu.

"Mzee Kombo hujambo?", Mzee Fichua alimsalimu. "Sijambo Mzee Fichua. Huu mguu wangu umepatwa kwa meno ya Moma. Huyo Moma alikuwa akikimbilia usalama wake baada ya kuniona. Nilipojaribu kumfuata, sikumwona kutembea mita mbili nilimkuta miguuni. Nguvu za kumfuata tena zilinitoka; baadaye niligundua kuwa alikuwa amenipa jeraha!" Mzee alikitwaa kichondo chake na kuudadisi mguu huo. "Yule nyoka alikuwa na madoadoa ngozini?”. "Naam! Naomba msaada wako maana najua wewe ni mnunguri hodari hapa kijijini." "Unapomtafuta nyoka, anzia miguuni pako! Hii ni dawa ya funganyumba. Maagizo yake ni kama yale ya juzi niliyokupa. "Shukrani sana usisahau kuwa Jumamosi hii kuna mkutano wa chifu," Mzee Kombo alimkumbusha tabibu wake.

Jumamosi alikuwa akiwahudumia wateja wake. Kila mara alielekea msituni kutafuta dawa. Alikuwa akiwarai wagonjwa kutembelea vituo vya afya endapo angepata uwele asioujua. Nayo siku ya Jumapili hakukosa maabadini. Alikuwa mcha Mungu.

Wateja wengi walimiminika siku ya Jumamosi; wa kwanza kufika alikuwa Bi. Kale. Bi. Kale alikuwa akifanya kazi katika ofisi ya hatimiliki kwenye kijiji cha Walemakili. Alikuwa mchapakazi asiyependa maneno ya auni. Siku moja, Daktari Robo alimtembelea katika ofisi yake na kumsihi ampe saini ya kiwanja fulani alichokuwa amepewa na mwenyekiti wa mtaa kinyume cha sheria. Bi. Kale alipogundua kuwa zilikuwa na hitilafu, alidinda kumpa saini hiyo. Jambo hilo lilimkera sana na kuapa kulipiza kisasi kwani sheria zilimwandama Daktari Robo baadaye na kisha akakirudisha kiwanja kwa mmiliki halali. Jambo hilo lilimfurahisha sana Mzee Fichua baada ya kusimuliwa kisa hicho. Alimwonya dhidi ya uporaji wa mali ya umma.

"Shikamoo Mzee Fichua?" Mzee Fichua alipigwa na mshangao kumwona mwarabu aliyekuwa ameandamana naye. "Marahaba Bi. Kale, karibuni! Leo nimeona nyongeza ya rangi ngeni hapa kwangu! Huyu ukamtoa wapi?" Kabla ya matibabu, Mzee Fichua alikuwa na mazoea ya kupata taarifa kuhusu wateja wake. Hata hivyo, alifahamishwa bayana na Bi. Kale. "Huyu anaitwa Bahshar, ametoka Uarabuni. Alikuja huku na aila yake kwa ajili ya kutalii huku lakini alipofika akalemewa na ugonjwa wa kifaduro." Bi. Kale alieleza. "Kifaduro! Kifaduro huwashika watoto inakuwaje huyu mtu mzima?" Wote walicheka. Mteja mwingine aliyekuwa ameandamana nao alimsawazisha. "Samahani, huyu ni mtoto, mazingira yao huwafanya kuwa na miili mikubwa ila usihofu!" Aliridhika kwa maelezo hayo. Alichukua magome na mizizi ya mng'ong'o na kumpa. "Mweleze kwa lugha yenu kuwa awe akichemsha maji kikombe na anywe mara tatu baada ya mlo". Alimgeukia Bi. Kale. Tatizo lake alilijua vizuri. "Naomba ukanawe mikono pale, leo nitakupa hii dawa ya mizizi ya mjafari. Ningependa utumie hii tuone. Shida ya tumbo imepata suluhu." Alikitoa kisu chake na kuikata mizizi hiyo ya mjafari vipande vipande na kumkabidhi. "Mimi siuzi dawa za kuua watu, hilo unalijua!" Mteja wa mwisho alikuwa akisumbuliwa na mishipa. Alipewa dawa ya kania. Kila alipotembelewa na wateja wake aliwasisitizia kutembelea vituo vya afya kwa uchunguzi zaidi. Bi. Kale alimwahidi kurejea tena.

Chifu aliitisha mkutano kijijini. Mkutano huo ulihusu visa vya wizi vilivyokithiri katika kijiji hicho. "Kijiji chetu kimekumbwa na visa vingi sana

vya wizi na unyang'anyi wa kimabavu. Ningeomba maoni ya kudhibiti hili suala. Kabla ya kutoa fursa hiyo ningeomba Mzee Mala, mwenyekiti wa mtaa huu atupe maoni yake. Mzee Mala alikuwa akinakili vipengee fulani kwenye shajara yake. "Asante sana Bwana chifu kwa fursa ino adimu. Itifaki nzima itambuliwe! Wakazi wangu wamekuwa wakihangaishwa na wezi waliojihami kwa muda mrefu. Juzi, kondoo wa Bi. Hangaiko aliibwa. Kufuli la mlango wake wa jikoni alimokuwa kondoo yule lilikatwa kwa msumeno nikiwa bado nafuatilia tukio hilo, seng'enge ya Baba Karimu ilichukuliwa na mtu asiyefahamika. Baba Karimu alikuwa ameenda kuwatafuta mafundi wamjengee uzio wake. Aliporudi hakupata seng'enge hiyo. Nilifanya ujasusi wangu ila sijapata fununu za mhusika". Hadhira ilisalia kimya huku Bi. Hangaiko na Baba Karimu wakithibitisha maneno ya mwenyekiti kwa kutikisa vichwa vyao.

Mzee Mala aliendelea, "Bwana Chifu, kisa cha leo kimenishtua sana. Genge la majambazi lilivamia jumba la jirani yangu anayeishi Uswisi. Walifanikiwa kuiba; makochi, kiyoyozi, televisheni, kamera na vitu vyenye dhamana ya takribani laki saba. Tulipopata habari hizo tulijihami vilivyo ila wakatutangulia kwa maarifa. Walifanikiwa kuhepa." Baada ya kumaliza kauli yake, Mzee Fichua alisimama.

"Chifu, suala la wizi na ujambazi kweli limetupokonya utajiri wetu. Ukitaka kufika kwa mfalme bila idhini yake basi tumia mavazi ya mwanawe. Hivi hamjashuhudia wizi wa mikufu ya dhahabu kuibwa kwenye kasri? Tena ndani ya kichumba cha siri asichoingia mtu ila yeye na wanawe! Je, nani aliyetoa siri hiyo ya kuwepo kwa mikufu? Zaidi ya maseremala walioijenga kasri hiyo walioangamizwa baadaye. Wanakijiji wenzangu, tambueni kuwa siri ya nyani kamwulize kima."Misemo na mafumbo hayo yalionekena magumu kwenye mkutano huo. "Ukitaka kumtawala mtu mgawie. Ili kuwanasa hawa wezi teua jopo la walinda usalama tena litoke miongoni mwa vijana wasio na kazi. Wanaotuibia ni hawa vijana wetu. Ni watoto wetu, wengine ni wadogo. Mwizi asiye na silaha si mwizi, silaha yake ni njaa. Licha ya kuwa na silaha hawatumii. Kwa ufupi, visa hivi vinatekelezwa na vijana wetu wasio na kazi wala bazi, hawana cha kujishughulisha, si bure wakatumia mabavu". Maoni ya Mzee Fichua yalitazamiwa vyema na kila mtu. Chifu aliteua vijana kumi na kupewa kibarua cha kulinda kijiji hicho. Mkutano ulitamatika. Huo ndio uliokuwa mwisho wa uvamizi.

Bi. Kale alikumbuka muda wa kurudi kwa Mzee Fichua. Alirauka mapema ili apokee huduma haraka kwani alikuwa na mkutano ofisini. Alifika

saa mbili na kumkuta Mzee Fichua akitia kisu chake makali. "Karibu sana Bi. Kale, hujambo?" Mzee Fichua alimwamkua."Sijambo daktari, leo nimekuja mapema!" alimjuza. "Umefanya vizuri. Naona hali yako yaendelea kuimarika." Bi. Kale alipewa huduma kisha akaondoka. Alipokuwa akisubiri bajaji baada ya kufika stanini, alishikwa na masua yaliyomtuma ardhini bila nauli. Alikimbizwa hospitalini Okoauhai na wasamaria wema. Aliwekwa kwenye chumba cha sadaruki. Wauguzi walimpa huduma ya kwanza ikiwemo dawa ya shazasi huku wakimsubiri daktari.

Daktari Robo alifika baada ya kupokea ujumbe. Aliitisha vifaa vyake; si glovu, si kipimajoto, si kirimbo, si sindano, si topozi, si sirinji. Daktari Robo alikuwa tayari kupambana na honi za mauti. Si walisema hatamu ikifika punda lazima aende? Alimgeuza mgonjwa aliyekuwa si hayati si mamati, alipomtazama vizuri hisia zake zilimpa jina la mteja wake. "Huyu ni Bi. Kale? Mmmm! Usimtukane mkunga na uzazi ungalipo! Alisema ataifuta nambari yangu kumbe msiba hauji mara moja". Daktari Robo alikumbuka jinsi Bi. Kale alivyomdhalilisha na kumvunjia heshima baada ya kukataa kumpa sahihi ya kiwanja fulani. Daktari Robo alimwendea siku moja ili ampe saini yake lakini alikataa katakata hata baada ya kuahidiwa kitita kikubwa cha ngwenje. Niupoteze muda wangu kwa ujinga huu? Mwanzo, saini pekee alikataa kuniwekea kwenye karatasi zangu nilizokuwa nimetolea jasho la chai akafanya nipoteze hela zangu! Laiti hawa wauguzi wangejua ulichonitendea wasingeniita! Madhali nimefika nitakamilisha ahadi yangu'. Daktari Robo alijisemea kimoyomoyo. Alielekea kwenye chumba cha famasi na kuchukua vidonge vyenye asali chungu**.** Aliporudi aliwaulizia wauguzi ikiwa wanamfahamu huyu mgonjwa. "Hatuna ufahamu naye, aliletwa na wasamaria wema. Huu hapa mkoba wake labda kuna kitu cha kutuelekeza. Aliupekua polepole na kisha kupata dawa ya pagao aliyokuwa amepewa kwa Mzee Fichua. 'Hmm! Lazima nitumie kivuli hiki kuwinda wanyama wanaoishi kivulini'. Alirudisha ndani na kisha kuichukua dawa aliyoitoa famasini. Wakati huu wote, Bi. Kale alikuwa akirudisha ufahamu wake, japo hakujielewa wala kuelewa kilichokuwa kikitendeka. Taswira ya hasidi wake haikumnasa. Alipogundua kuwa Bi. Kale 'alikuwa macho' alivalia barakoa na glovu pamoja na miwani yake kisha akatia dawa kwenye bomba na kumiminia mishipani. Bi. Kale alitii amri.

Aliwajuza wauguzi kutoa taarifa kuhusu mgonjwa huyo ili waje wakamshughulikie maana alikuwa tayari kakataa uhai. Wauguzi walifanya uchunguzi na wakapata aila yake. Mzee Kale alipofika, alishtuka kukutana na

mwili wa mkewe uso kwa macho. "Mkeo aliletwa hapa asubuhi akiwa katika hali mahututi. Vipimo vilionesha kuwa alikuwa na chembechembe za sumu ya dawa za kiasili zilizokuwa zimebana mishipa kwa ganzi!" Wauguzi walimtaarifu. Bw. Kale alipasua kilio na kuelekea karibu na mwili wa mkewe. Nimekukanya mara ngapi kuhusu huyo mzuza wako, ona sasa zawadi yake!" "Tafadhali punguza kelele, kuna wagonjwa wengine wasiopenda kelele," Wauguzi walihamaki. Iliwabidi wauguzi wauondoe mwili wa Bi. Kale na kisha kuupeleka kwenye mafuo.

Aila ya Bi. Kale ilielekea moja kwa moja hadi kwa Mzee Fichua. Mzee Fichua alikuwa amepata taarifa ya kuzimia kwa mtu fulani japo hakujua kuwa alikuwa Bi. Kale. Alikuwa katika hamsini zake. Umayamaya wa watu wenye ghadhabu za mkizi walitua kwa fujo. "Wewe mzee, kama ni ada mbona hukutuambia tukakupe? Kwa nini ukatize uhai wa mtu aliye hai kwa dhamana ya pesa zisizojua thamani ya uhai? Mbona! Mbona mke wangu?" Mzee Kale alimaka. "Jamani nipeleke polepole. Nipe muhtasari!" Mzee wa watu hakujua lolote wala chochote! Hakupewa fursa ya kujieleza wala hakuna aliyemweleza kwa upana! Kabla ya kumaliza kauli yake kijana mmoja alimpiga kwa silaha butu. Kichapo cha kipopo kilimtembelea Mzee Fichua kiasi cha kumsindikiza Bi. Kale.

"Jamani mhurumie huyu mzee, sijaona akiua miaka hii yote! Maskini mzee wa watu!" Mwanamke mmoja alijaribu kudhihirisha ukweli lakini moto wa kandili haupiki. Bwana Funda naye alikuwa pale huku kinywa chake kakifunga asiseme lolote. Alichukua rununu na kuwapigia polisi. Karandinga liliwasili na kigaro cha askari. Walilipua vitozamachozi huku kila mmoja akiaminia mguu wake. Walimchukua Mzee Fichua na kumpeleka hospitalini.

Daktari Robo aliamua kwenda kusherehekea matokeo yake. Akiwa katika hali ya kubugia alipokea simu kutoka hospitali ya Okoauhai kwa mara nyingine na kufahamishwa kuwa mgonjwa mwingine alikuwa amefika na alikuwa akichungulia kaburi. Aliona ni heri aende kule ili aokoe uhai. Alichukua chupa za pombe na kuzitia kwenye kiti cha mbele cha gari lake. Alirudi tena na kisha kulipa gharama yake kupitia njia ya simu. Mhudumu mmoja alimwonya kuendesha gari akiwa mlevi, lakini hakusikia la mwadhini wala mteka maji msikitini. Alichukua funguo na kutia gari moto. Aliliendesha gari lake kwa kasi ili afike haraka. Alipofika karibu na soko la Lurare, gari lake lilikosa mwelekeo na kugongana na lori kubwa lililokuwa likibeba vyuma. Lori lilibingirika na kuwaua watu kumi na wanne huku wengine wakivunjika viungo vya mili yao.

Vyuma hivyo vilitapakaa kote huku vikiwavunja waliopatikana. Mwanamke mmoja aliyekuwa amehimili aligongwa ghafla kwa chuma tumboni. Kijusi kilisalimu amri papo hapo. Mtu mmoja mwenye umri wa makamo hakusazwa na vyuma hivyo, alipokuwa mbioni kujinusuru, alikatwa shingo yake. Gari jingine la mafuta lilikosa mwelekeo na kuangushwa. Soko la Lurare liliona ya Firauni. Mauti yalibisha. Hakika, lilikuwa janga la taifa. Miongoni mwa wale waliovunjika ni mwanawe mwendazake Bi. Kale aliyekuwa akielekea sokoni kuchapisha chapa za barua za harambee katika mazishi ya mama yake.

Hospitali ya Okoauhai ilishiba machozi ya simanzi. Nesi walionekana kubeba majeruhi na wafu kwenye machela. Kwa bahati nzuri Daktari Robo hakufariki dunia. Alikuwa na majeraha madogo madogo. Aliweza kupelekwa kule kule hospitalini. Serikali iliagiza miili yote kufanyiwa upasuaji ili wenyewe watambuliwe. Sampuli za msimbojeni zilitolewa. Rais aliagiza madaktari kutoka taifa la Dakibora. Dakibora ni taifa lililoaminika kuwa na madaktari wenye tajiriba katika sekta ya afya. Huko nyumbani, familia ya Bi. Kale ilipokea pigo jingine lililowavunja mioyo. Chudere wake Bi. Kale naye alikuwa matatani. Miguu yote ilikuwa imevunjwavunjwa. Ilibidi kusitisha harambee hiyo na kuelekeza macho yao kwa chudere wao. Kweli, siku ya fuko kufa mashimo yote hujaa maji.

Siku iliyofuata, madaktari walitua katika hospitali ya Okoauhai. Shughuli ya upasuaji wa miili iling'oa nanga ili kubaini familia walikotoka. Wahazigi walifanya kazi yao. Vipimo vilichukuliwa na kupelekwa maabarani. Mzee Fichua alikuwa miongoni mwa wawele waliopata huduma za madaktari hao kutoka Dakibora.

Aila ya Bi. Kale ilikata kauli ya kumzika Bi. Kale ili kuepuka gharama za mochwari. Asubuhi iliyofuata waliamua kwenda kuuleta mwili wake. Walipofika mochwarini, walishtuka kutopata mwili wa Bi. Kale. Iliwabidi waelekee kwenye ofisi za hospitali hiyo. Ukaguzi ulibaini kuwa mwili wa Bi. Kale ulikuwa miongoni mwa ile miili iliyochukuliwa ili kufanyiwa vipimo tena. Wauguzi waliouchukua mwili huo hawakuwa na ufahamu kuuhusu, isitoshe ulikuwa karibu na miili iliyoletwa baada ya ajali. Walishangaa kwa nini wafanyakazi hao walikuwa watepetevu kiasi hicho. Iliwalazimu wasubiri matokeo ya vipimo. Siku tatu zilipotamatika, vipimo vilitolewa na waziri wa afya, "Makiwa kwa familia, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao. Poleni kwa wale waliopata majeraha. Uchunguzi uliofanywa ulibaini kuwa dereva aliyekuwa na gari dogo ndiye aliyezua haya. Alikuwa akiendesha gari

hilo kwa kasi akiwa mlevi chakari. Isitoshe, chupa za vileo zilipatikana kwenye gari lake kabla ya ajali kutokea, maafisa wa barabarani walijaribu kumsimamisha lakini hakutii amri. Daktari Robo ana kosa la kuendesha gari akiwa mlevi. Kitengo husika kitampa adhabu kali atakapotoka hospitalini. Ajali hii ilisababishwa pale gari lake lilipokosa mwelekeo na kugongana ana kwa ana na lori lililokuwa likibeba vyuma katika soko la Lurare. Lori liliwaua watu kumi na wanne. Kwa sasa, vifo vinne viliongezeka huku majeruhi wakisalia hamsini wakiwemo madereva wote wawili. Vipimo vimechukuliwa na familia zote zitapewa wapendwa wao. Mwili mmoja haukuwa na majeruhi ila vipimo vilionesha kuwa ulikuwa na dawa za sumu. Kulingana na utafiti wetu, tuligundua kuwa Daktari Robo ndiye aliyekuwa akimshughulikia mgonjwa huyo aliyefahamika kuwa Bi. Kale. Japo habari zilizotoka awali zilikuwa za uzandiki. Kamera za siri zimetuonyesha kilichotendeka na mhusika atachukuliwa hatua za kisheria." Kimya kilitanda kwenye kikao cha mazishi ya Bi. Kale. Habari ziliwatatanisha mara sumu ya vidonge mara sumu ya dawa za mzuza. Ujumbe ulitumwa kwa aila hiyo kusitisha mazishi hayo. Wiki tatu baadaye, Daktari Robo alishtakiwa na kupewa adhabu ya kugharimia maziko.

Mahakama ilimpa adhabu ya kumlipa Mzee Fichua ridhaa kwa kosa la kusingizia. Isitoshe, Shirika la Afya lilimnyima kibali cha kutibu kwa muda wa miaka sita. Daktari Robo aliliuza shamba lake lililokuwa mjini na baadhi ya mali yake ili kujazia dhamana ya shilingi milioni hamsini zilizohitajika. Mzee Fichua alirejea nyumbani akiwa na mfuko mnene lakini afya yake ilimnyima furaha yake ya awali. Aliweza kuwasamehe wote waliomtia mashakani! Alimsamehe Daktari Robo na kuomba dhamana ile iiendee familia ya Bi. Kale. Alizilaumu nguvu za sindano yake akatambua kuwa uovu haulipwi kwa uovu!

| ***Jitathmini*.** |
|---|
| **a)** *Eleza maudhui manne yaliyojitokeza kwenye kisa hiki* |
| **b)** *Andika muhtasari wa kisa hiki Nguvu za Sindano.* |
| **c)** *Kisasi hakilipi, andika insha ukidhibitisha kauli hii.* |

# PESA NYEUSI na Hector Mbati

Kengele ilikiriza kuashiria mwisho wa siku. Mara nyingi mlio huu ulileta tabasamu miongoni mwa wanafunzi baada ya mseto wa matukio shuleni. Leo hii naandamana na sahibu wangu wa dhati almaarufu Babu. Ingawa alikuwa mchanga kiumri, tabia na matendo yake yalikuwa ya kiutu uzima. Nilimpenda sana Babu. Hatukuchocheana vidondo kamwe. Tuwapo njiani kwenda nyumbani, tulipenda kuyatafuta matunda kwenye miti iliyokuwa kando ya barabara, tukayachuma na kuyala ili kushtaki njaa.

Leo, katika harakati za kutafuta matunda kama ilivyo kawaida yetu tutokapo shuleni, gari aina ya Isuzu liliwasili ghafla. Dereva ambaye alikuwa amevalia miwani mieusi tititi ja makaa alishusha kioo cha gari lake na kisha akatutazama kama tuliokuwa shidani. Alitutazama kwa takriban sekunde thelathini. Lilikuwa pandikizi la mtu. Sura yake ilikuwa ya kutisha. Wasiwasi ulituvaa kama nguo. Roho zetu zikatudunda kama ngoma ya Wazaramo. Tulishindwa kufahamu baya tulilotenda. Tulimwona akifungua mlango wa gari lake na kushuka kwa mwendo wa madaha ungedhani ni mgeni aliyetoka Ulaya na kuwasili Afrika kwa mara ya kwanza. “Nyinyi ni akina nani na mnatafuta nini hapa?” Aliuliza kwa sauti ya simba.

Babu alikuwa akitetemeka ja tete motoni. Kwa upande mwingine nilijitia ujasiri japo kijasho chembamba kilizidi kunidondoka usoni kuashiria wazi hawafu ya mwasi. Nilitarajia mwandani wangu Babu azungumze na huyu mgeni tusiyemjua lakini ulimi wake ukawa mzito, akawa wa maji mtungini. Nilijitia ujasiri na kumueleza bayana kwamba sisi tulikuwa wanafunzi wa shule ya upili Mnarani na tulikuwa tukielekea nyumbani. Pindi nilipomaliza kujieleza, dereva yule alianza kunena nasi. Alitueleza kwamba yeye ni mgeni na alitaka kufahamu eneo letu vyema. Alitukaribisha kuabiri naye garini. Hatukuwa tumezoea kuabiri gari tusilolijua kwa sababu visa vingi vya ulanguzi wa watoto vilikuwa vimekithiri. Babu aliomba tuingie garini angalau tufike nyumbani mapema. Tuliingia garini huku tabasamu ikituvaa nyusoni.

Safari ilianza, Babu ndiye aliyechukua jukumu la uelekezi nami nikachukua jukumu la kusimulia hadithi mbalimbali kuhusu eneo letu na jamii yetu. Kwa muda huu wote dereva ambaye baadaye alijitambulisha kama Mtindi alikuwa akitikisa kichwa ishara ya kuwa nasi. Alikuwa akielewa maelezo yetu kwa ufasaha. Tulitembelea vitongoji vyote katika wilaya nzima. Ilikuwa safari iliyofana sana. Kwa mara ya kwanza nilijihisi mtalii katika eneo ambalo

nilifahamu kwa miaka mingi. Baada ya matembezi hayo, Mtindi alituomba tuandamane naye mkahawani.

Kutokana na ukarimu tuliokuwa nao na mafunzo tuliyopokea shuleni kutoka kwa walimu wetu, hatukuwa na budi. Tulipofika mkahawani Mtindi aliagiza vyakula vya kila aina kuletwa mezani. Milo mbalimbali ililetwa. Tuliajabia sana kwa tendo hilo la ukarimu. Tulikula hadi matumbo yetu yakasalimu amri. Babu naye hakukoma kuendelea kula, aliamini kwamba bahati kama hiyo ni nadra sana kuipata maishani kwani siku zote alisadiki kuwa bahati huja mara moja. Tulimshukuru sana Mtindi kwa wema ambao alitufanyia siku hiyo. Babu aliomba ruhusa ya kuondoka kwani wazazi wake walikuwa wenye masharti makali na iwapo angerejea nyumbani kama amechelewa angepewa kichapo cha mbwa, hivyo basi tulimruhusu aondoke kwani nyumbani kwao kulikuwa mkabala na mkahawa huo.

Muda ulizidi kuyoyoma. Kutokana na ukarimu huo sikutaka kufanya tendo lolote ambalo huenda lingefanya nafsi yake kujuta. Nilijizuia hadi wakati ambapo mwenyewe angenieleza sasa ni wakati wa kuelekea nyumbani. Mtindi alitoa bunda la noti mfukoni kisha akalipia gharama ya vyakula. Nilitafakari nilipomwona Mtindi akirejesha mabunda ya noti kwenye mkoba ambao alikuwa ameubeba. Nilisadiki kwamba dunia ina wenyewe na wageni, matabaka ya walalahoi, wachochole, wasinacho dhidi ya walalahai walinacho na wanaojiweza katika jamii. Nilikumbuka umaskini ulioshamiri nyumbani. Ilikua bahati mkono kwenda kinywani. Tulizoea hali hiyo. Maskini wa Mungu tungebahatika kula mara moja kwa siku. Si neno insi huwa na bahati yake maishani. Nilitamani sana nimweleze hali halisi ya maisha kwa kuwa nilimuona kama mja mwenye roho ya wema. Nilidhani kipindi kile cha kujiburudisha kimekamilika kumbe nilikuwa nimekosea. Mtindi alinihakikishia usalama wangu na kunieleza nisiwe na wasiwasi kwani angenirejesha hadi nyumbani. Aliniomba tuandamane naye katika chumba cha pili. Kwa hakika sikufahamu haswa chumba hiki kilikuwa cha kazi gani. Chumbani, tulikaribishwa kwa mandhari tofauti kabisa. Taa za rangi mbalimbali zilining'inia kwenye dari. Naam, hapo mwanzo nilikuwa nimehadithiwa kuhusu kilabu cha Mang'weni ambacho sifa zake zilikuwa zimeenea kote kijijini na nje ya nchi. Mziki maarufu aina ya Rhumba ulirindima kwa sauti ya juu. Hapa watu walikuwa wameketi wawili wawili, yaani jinsia ya kike na ya kiume. Haya yalikuwa matukio ambayo nilikuwa nakikumbana nayo kwa mara ya kwanza. Vileo vya kila aina vilitapakaa mezani.

Nyumbani wavyele wangu walinisaka kila mahali. Walimpigia simu mwalimu wa darasa, naibu wa mwalimu mkuu, mwalimu mkuu na masahibu wangu ila hawakupata jibu. Waliamua kuelekea katika kituo cha polisi cha Chezaukamatwe kuandikisha ripoti ya kupotea kwangu, Zainabu. Vidosho walijaa humu, mitindo yao ya matembezi ilikuwa ya kumpa mtu mshawasha. Wote waliofika humu walionekana kuwa na furaha usoni. Muziki ulichezwa kwa utaratibu. Aidha, muziki huu uliwavutia wengi waliofika ukumbini na kunengua viuno. "Che! Che! Che! Che! Unapenda vitu vya che! Sigara hutaki waacha!" Ndo wimbo uliohanikiza kwenye ukumbi huu. Kila mwanamume alikuwa na kidosho ambaye aghalabu walisakata densi pamoja. Taa za rangi mbalimbali zilizidi kuurembesha ukumbi huu na kuufanya uvutie. Aghalabu ni mandhari yaliyowafanya wateja wazidi kuagiza zaidi vileo ili kuonyesha uwezo wao wa kihela mbele ya mabinti ambao walikuwa wameumbwa na kurembeka wakawa mbeja. Wateja wa kiume waliketi kwenye viti maarufu kama "sina taabu" na mabinti wawili wawili mbele ya kaunta ili pochi zao ziwatetee.

Binti mmoja ambaye nilikuja kumfahamu baadaye kama Maria alifika tulipokuwa tumesimama. Tabasamu yake ilikuwa ya mnato uliowafanya wote waliofika kilabuni pale kumviziavizia popote alipoenda kwani alipotabasamu ungehisi msisimko wa damu mwilini. Alituelekeza pembeni na kisha akatuamkua kwa salamu kama ilivyokuwa ada. Maria alikuwa mhudumu mcheshi sana. Alifika na kutuagizia *order* yetu. Mtindi alinitazama kwa makini na subira ambayo ilileta hali ya utulivu wa takribani dakika moja. Ni vipi ningelijibu swali hili alilouliza Maria? Laiti angalijua ni mara yangu ya kwanza kufika baani. Wazazi wangu Omari na Riziki walikuwa wamenilea kwa hulka za Kikristo na ambayo ilipinga mtindi wa aina yoyote. Ni mshangao upi ungewapata iwapo wangetambua kuwa mwanao wa pekee Zainabu amejitosa mtungini? Walijikimu kwa riziki iliyokuwa ya kipato cha chini ili kuhakikisha kwamba nimeelea katika nyanja za elimu ili baadaye kuwaondoa katika lindi la uchochole. Isitoshe, nilikuwa na umri wa miaka kumi na saba na mwanafunzi katika kidato cha tatu aliyetazamia kuufanya mtihani wa kitaifa mwaka uliofuata.

Nafsi ilizidi kunihukumu. Fuadi ilizidi kudunda. Kitumbua kilikuwa kimeingia mchanga. Mtindi aliyeonekana kuwa na ufahamu wa majina mbalimbali ya vileo alidakiza mazungumzo yangu na Maria kabla sijajibu. Naam, akawa ameniondoa katika mtego wa swali la Maria ambalo lilikuwa la kwanza maishani katika mandhari hayo maalum. "Leta ya juzi mbili baridi,"

aliagiza Mtindi. “Zainabu, wajua haya maisha wakati mwingine unastahili kupumzisha nafsi na msongo wa mawazo baada ya shughuli mbalimbali za kutwa. Vinywaji hivi havina athari yoyote kwenye mwili wa binadamu. Ukionja nakuhakikishia kwamba hata masomoni utatia fora kwa kuwa humfanya mtu kufikiria kwa kina na kudadavua masomo kwa undani. Hivi unionavyo nilianza kutumia *vinywaji* katika shule ya msingi na havijaniathiri kwa vyovyote vile. Kwa hivyo, chaguo hapa ni lako”. Alieleza Mtindi. Baada ya kunihadithia kisa chake, alifungua soda na kileo hicho cha *Krome* na kumimina kwenye glasi. Ama kweli hela zina uwezo wa kubadili harakati na mipango mbalimbali katika maisha.

Maelezo ya Mtindi yaliniacha kwenye njiapanda. “Je, nikubali kuonja ili kumuonyesha tu pamoja?" "Na nisipoonja atanionaje?" Si nitakuwa nimeisaliti nafsi yake?" Potelea pote!” Nilichukua kileo na moja kwa moja nikakimimina gilasini kama aliyekuwa na uzoefu wa kupigiwa mfano. Nilianza kubugia pombe hiyo kwa pupa huku Mtindi akizidi kunipa motisha kuwa glasi moja tu haitoshi. Uchu na ulafi wangu mithili ya fisi ulisababisha ninywe pombe hiyo bila kusaza. Mtindi alinipongeza kwa kuonyesha ujasiri kwa kubugia pombe hiyo yote. Nilianza kuhisi kisunzi akilini. Mwili uliingiwa na mchecheto uliofanya nianze kububujikwa na maneno ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha rasmi pindi mtu anapopiga mtindi. Muziki wa Rhumba uliokuwa unasikika kote ulinivutia hadi jukwaani. “Kumbe kuna dunia ya raha mustarehe? Sitarejea shuleni tena,” nilijiambia mawazoni. Kwa upande mwingine Mtindi alizidi kubugia kileo chake kwa ustaarabu. Mrina asali hasahau mzinga. Hamu ya kuendelea kulewa ilinijia na kunirai niendelea kubugia chupa zaidi. Tulijiburudisha na vileo vya kila aina. Ilipowadia saa sita usiku, fahamu zetu zilianza kutoweka. Mtindi akawa hajielewi hajifahamu. Nami pia sikusazwa kwa kuwa fahamu zangu zilinionyesha nikiwa dunia ya pili, dunia isiyoeleweka. Tulijilaza kochini na usingizi ukatuchukua moja kwa moja. Mabinti waliokuwepo kutokana na uzoefu wao pale kilabuni, walitujongelea na kuanza kutupapasa ishara kwamba walikuwa na nia fiche. Wengine walikuwa na nia ya kushiriki nasi kimapenzi na wengine nia yao ikawa ni kutuhadaa na kutupora vitu vyote tulivyokuwa navyo. Saa kumi alfajiri, fahamu ziliporejea, nilimwamsha Mtindi ambaye bado alikumbwa na lepe la usingizi. Aliitikia wito na kuamka. Alipoamka alipigwa na butwaa pale alipoupeleka mkono wake mfukoni na kutambua kuwa simu yake pamoja na fedha alizokuwa nazo zimepata wamiliki wapya! Biwi la mashaka lilitukaba. Tulisalia katika

njiapanda kwani mhudumu tayari alikuwa ashatupa risiti iliyoorodhesha vinywaji pamoja na hela ambazo tulistahili kulipa. “Leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo. Siku ya fuko kufa maji hujaa mashimoni, leo tutafungwa kwa kutolipa bili.” Alisema Mtindi. Usemi wake uliniacha katika hali ya taharuki. Sikuamini sasa mkono wa sheria ulikuwa unatukodelea macho. Mhudumu alimaka kwa sauti ya juu. Alipoona tumekataa wito wake wa kupeleka hela hizo, alipiga simu katika kituo cha polisi cha Chezaukamatwe. Nilitamani dunia ipasuke na kunimeza mzima mzima nikiwa hai lakini wapi. Nilijuta sana kukubali pendekezo la kuingia na kushiriki ulevi.

“Nitakuwa mgeni wa nani?” Machozi yalianza kunidondoka, nilihisi nafsi ikinihukumu kwa kuwa nilikuwa nimewasaliti wazazi. Ama kweli nilijutia matendo yangu ambayo baadaye yamekuja kuisaliti nafsi yangu na jamii yangu kwa jumla. Karandinga la polisi liliwasili katika kilabu cha Mang’weni. Polisi waliokuwa wamevalia sura za kazi walituchukua hangahanga wakatutupa ndani ya gari lao kama gunia la wimbi wa gongo. Inspekta Kali aliponiona alinitambua maana maelezo ya wazazi wangu yalimfika akilini. Baada ya kugundua kuwa Mtindi alikuwa mlanguzi wa watoto, polisi walimtia mbaroni na kushtakiwa mahakamani kwa kosa la kuwalangua wasomi kwa kutumia pesa nyeusi.

| **Jitathmini** |
|---|
| ***a)*** *Eleza kikamilifu maudhui ya usaliti.* |
| ***b)*** *Eleza maudhui manne yaliyojitokeza kwenye hadithi hii.* |
| *c)* *Eleza sifa tano za Zainabu.* |

# ALIPORUDI na Samwel Nyongesa

Mama Zitu hakuonekana mtulivu wa mawazo alikuwa mama mwenye siri. Sikuwa nimedhibitisha methali kuwa mama wa kambo si mama. Kwangu, kila mama alikuwa ni mama. Katu alijulikana kwa mwendo wake wa arubii, hivyo alitumwa dukani**.** Kwani hakuamini kuwa polepole ndio mwendo. Nami mama hakuuacha uvivu uniandame na kunitawala, alinituma shoka kwa mama Sara. Niliona fahari kwani nilijua kuwa nimepata fursa ya kuenda kumsabahi msiri wangu Ben. Kwa hakika tuikuwa marafiki wa chanda na pete. Tulifuatana sanjari mithili ya maamuna na imamu. Lakini si amuka twende ni kwa wapatanao? Nani asiyejua hili? Nilipiga milundi ya guu mosi guu pili hadi kiamboni kwa muhebi wangu. Nilifululiza moja kwa moja hadi jikoni. "Umeniamkia leo?  Lo! Leo nitalala njaa" Alisema mama Sara." Kwa nini mama?" Niliuliza huku nikikosa kujizuia kwa kicheko. Huu ndio utani niliouzoea pindi niingiapo kwa mama huyu mcheshi." Ben yuko wapi?" Nilimwuliza. "Alipofunga shule alifunga safari kuelekea kule kwa mjomba wake Kazamoyo" Mama alijibu. Nilijihisi mchovu na mpweke. Ama kwa hakika, upweke ni uvundo.

Alinidadisi kwa muda huku akichochea moto ili kuharakisha upishi wa chajio. Kwani, yalikuwa ni majira ya saa thenashara. "Ulitaka kucheza naye?" Sikujua niseme la au ndiyo maana ningekana ningedanganya maadamu nilikuwa nataka kucheza. Nisingekubali maadamu kiza cha kaniki kilikuwa chajimwayamwaya kushika usukani. Nilipuuza swali lake. "A...a...a, nilikuwa nataka uniazime shoka," "Subiri tule" alisema. "Nashukuru usiku u karibu", nilimsihi. Alinipa shoka nami nikamuaga.

Nilichapua miguu wanguwangu huku maswali belele yakinizonga. "Mbona Ben aliondoka bila kunipa mkono wa buriani? Atarudi lini? Nami nitacheza na nani? Nilipiga moyo konde na kuishawishi nafsi yangu kuwa ningecheza na kuku wetu pamoja na panya. Nilipozinduka kutoka mawazoni, nilikuwa tayari nimewasili maskanini mwetu. Nilisikia sauti ya watu wawili. Miguu ilinionya kuwa nisipaparike, niende taratibu. Sauti ya mwanamke ilisikika ikiamuru. Haikuwa ngeni kwangu ilikuwa ni ya mama Zitu." Nataka arudi akiwa maiti" Sauti ya kiume ikasikika ikirudia maneno yale, "Wamtaka arudi akiwa maiti?" "Nisemavyo" Mama alijibu.

Mama Zitu alitoka nje akiandamana na mwanamume mwenye nywele za singa. Alikuwa na sura ya kutisha. Mama alishtuka japo hakuonyesha dhahiri."Umefika mapema?" Mama aliuliza." Ndiyo mama," nilijibu. Niliingia chumbani kichwa changu kikialama kutokana na maswali mzomzo yaliyokuwa yakibishana kuingia na kutoka. "Arudi akiwa maiti? Ni nani huyo? Ni kwa nini?" Maswali haya yalienda yakamfikia Katu aliyekuwa karudi na kusimama karibu na mlango.

“Nani huyo arudi akiwa maiti?" Aliuliza. "Wataka kujua?" Nilimwuliza. “Hata mimi sijui," alisema." Unamaanisha nini unaposema hujui?" Aliuliza." Hata mimi nilimsikia tu mama akimwamuru mgeni wake." Ghafla bin vuu, mama aliingia. Kila mtu alijipa shughuli ambazo hazikuwepo. Mimi nilijikuta nikiwa na ufagio nikifagia ukuta badala ya sakafu. Kaka yangu Katu naye katika kuchanganyikiwa, alijikuta akivitandua vitambaa badala ya kuvitandika. “Mwafanya nini?" Mama aliuliza. "Nenda ukaake moto ukaanze upishi" Katu aliondoka kwa haraka. Nilibaki nikiyapepesa macho tu. " Nenda ukavisafishe vyombo vya kulia!" Mama aliniamuru.

Mama Zitu alifahamika kwa adhabu za kukumbukwa. Sijui mbona siku hiyo aliamua kutusamehe. Pengine alifahamu fika kuwa, kukosa si kosa bali kukoseakosea ndiko kukosa. Ama amesubiri tule tushibe?

Ijumaa, siku ya kuzaliwa kwangu, sote tulijihimu alfajiri mbichi. Jua lilikuwa halijayeyushusha umande. Tulikuwa na shughuli ainati za kukamilisha kabla ya wageni kuwasili: kufyeka, kupamba ukumbi, kupika na kujinadhifisha zilikuwa zimetukodolea macho. Saa nne, wageni walianza kufika na kuwasili kwa makundi ya wawili, watatu na wanne. Ukumbi ulikuwa umepambwa kwa mapambo anuwai. Maua yenye rangi mbalimbali yalipendeza na kutaanisi machoni pa wengi. Nilihisi mzizimo wa furaha mishipani nilipokuwa nikiwakaribisha marafiki zangu. Hakika, raha ya karamu ni watu.

Tafrija ilianza kwa dua. Yakafuatwa na mahubiri mafupi yaliyosheheni ucheshi. Meza ziliandikwa kwa vyakula vya kumezewa mate. Bwalo lilijaa sisisi ya watu waliojipa kazi ya mdomo. Kwetu kulifahamika kwa maandalizi ya sherehe za kupigiwa mfano. Si vijisherehe vya kula urudi nyumbani ukiwa na tamaa ya chakula. Kaka yangu Katu aliamua kututumbuiza kwa muziki wa kuongoa. Hata wewe wajua muziki mtamu huandamana na viuno kunenguliwa pamoja na mabega kuchezeshwa.

Wakati wa kula keki na kuteremsha kwa maji baridi shadidi ya matunda ulijiri. Mfawidhi alitoa amri "Mwenye sherehe ajongee mbele ili akate keki".

Niliitikia wito. Nilitembea kwa mbwembwe zilizovaana sawasawa na suti yangu nyeusi tititi kama kaniki. Nilikishika kisu tayari kuikata keki iliyozua gumzo miongoni mwa watoto katika mtaa wa Madongoporomoka. Nilianza kuigusa ili kutafuta pa kufungulia ili nione muhebi baba yangu kaandika ujumbe gani juu ya keki hiyo. Nyimbo za kuongoaongoa zilihinikiza anga. Kabla ya sekunde kuunda dakika, simu ya mama ilipigwa. “Hello! Unasema nini?! Eti amekufa!" "Nani" Katu aliuliza hata kabla mama hajamaliza kuzungumza kwa simu.

“Baba yenu ameenda mbele za haki" Mama alisema kwa huzuni. Kisu kilinitoka mkononi kikaanguka. Nilikuwa nikitetemeka mithili ya kondoo mwenye manyoya haba. Nililia kwa kite na simanzi. Ni nani asiyelia anapofikwa na msiba? Tuliotarajia kuila keki, tulikula habari za tanzia. Wandani wetu walirudi kwao kwa huzuni huku wakizieneza habari za hivi punde. Siku ile ilibaki katika kumbukumbu za kichwa changu. Siku ya uchungu. Kiamboni mwetu mlifurika watu karibu kuwatapika wengine. Vilio vilitawala anga nzima. Hii ndiyo siku iliyoratibiwa kumpumzisha baba. Kwa mujibu wa mila zetu, mtu yeyote aliyefariki kutokana na maradhi yasiyojulikana hakawii kuzikwa. Mwili uliletwa takribani saa tisa unusu. Jeneza lilitolewa katika gari jeusi tititi. Baba alikuwa amenyooka twa, hasemi haneni, hamkumbatii mtu tena wala kutabasamu. Nilipiga foleni sawa na watu wengine ili kuutazama mwili.

Machozi yaliusafisha uso wangu. Baada ya kuuona mwili nilisimama kando nikishauriwa la kufanya. Mwanamume ambaye hakufahamika na wengi alionekana ghafla. Kila mja alimuangalia kwa jicho la “siji” Mimi nilimfahamu fika. Nilibaini kuwa alikuja kuhakikisha kuwa amerudi akiwa maiti. Baba alipewa heshima za mwisho na kutiwa katika chumba chake cha milele. Alilazwa karibu na kaburi la mama yangu Subira.Tulibaki tukiliwazana na Katu. Ilibid waama wino wa Mungu haufutiki aidha, mwanadamu hadumu.

Mama Zitu hakuonekana mtulivu. Nakumbuka nikimwona na jembe akielekea katika shamba la migomba. Alikuwa na mkoba ambao sikujua ulibeba nini. Alichimba shimo na kukichomoa kijisanduku mkobani na kukizika huku akiwa na uhakika kuwa hakuna aliyemwona. Katika harakati za watu kutanzuka, mimi na Katu tulijawa na ari kutaka kujua kilichokuwa kijisandukuni. Tulienda hadi alikoficha na kukichimbua. Kilikuwa mbali, japo matumaini yalionekana ya kukifikia. Hatimaye kijisanduku kiling'olewa, matumaini ya kujua kilichokuwa ndani yalizikwa katika kaburi la sahau. Kilikuwa kimefungwa kwa

kufuli. Katu alikichukua na kukificha kwingineko. Tuliuficha ushahidi wa kuchimbua pale na tukaondoka.

Tulifungua ukurasa mpya wa maisha. Maisha ya kuikumbatia shubiri baada ya asali. Ndugu yangu alijikaza kisabuni na kuukamilisha mitihani wake wa kidato cha nne. Nami niliona giza. Nilihamishwa kutoka shule ya bweni hadi shule ya kutwa. Nilikuwa katika darasa la sita. Nilikuwa mwana mkembe hata ubwabwa wa shingo ulikuwa haujanitoka. Mama Zitu alizionyesha kucha zake peupe. Hapa ndipo nilipomaizi kuwa mama wa kambo si mama. Maji yalipozidi unga, Katu aliamua kutokubali katu. Aliamua kugura nyumbani.

Asubuhi kabla ya kufunga safari, mama alimwamkia kwa matusi. "Nenda! Hapa hapana lako! Na usirudi! Ukirudi ndipo utakapojua fahiwa ya Zitu " Katu aliuchukua mkoba wake kuukuu na kujiondokea. "Katu usiniache," nilisema huku nikimkimbilia. Nilipokezwa kofi lililoniangusha pu na kuniacha nikiona vimulimuli. Nilipopata fahamu, sikujua alikuwa ameifuata njia gani. Katu alikuwa na hasira za mkizi, hata hivyo, sikumlaumu. Nikikumbuka kichapo alichopokezwa usiku huo, nikaanza kulengwalengwa na machozi. Sikujua nilikuwa nikilia kutokana na uchungu wa kofi au kumhurumia Katu.

Kila kuchao maisha yalichukua mkondo mpya. Nilijikuta nimebaki mtoto peke yangu ndani ya kucha za simba jike. Sikukata tamaa ya kuenda shuleni, kwani nilijua kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha. Aghalabu nilikuwa nikienda shuleni bila staftahi na kushinda bila kishuka. Nilikuwa nikila kitabu na kushiba kwa maarifa. Mawazo kuhusu ndugu yangu aliyepeperushwa na upepo kama tiara yalibaki kunitawala. Wakati mwingine nilikuwa na bahati kama mtende kupokezwa chai kule kwa akina Ben ingawa kila siku haikuwa Ijumaa. Ndugu yangu aliwaomba wanikaribishe kila mara. Angewalipa gharama zote angerudi. Kitendawili kilikuwa ni, angerudi lini? Angerudi akiwa maiti kama baba yangu? Nilijiuliza maswali haya yote nikiwa darasani peke yangu. Machozi yalinitoka njia mbilimbili nikashindwa kuendelea kusoma.

Niliamua kuyafanya madhila kuwa sehemu ya maisha. Nipatapo cha kutia kinywani, Mungu ni mwema, nikosapo nilijitia moyo kuwa ipo siku. Miaka miwili ilikuwa imetimia tangu Katu aondoke. Nilikuwa nimeufanya mtihani wangu wa kitaifa. Nilifua dafu licha ya changamoto si haba. Nilikuwa nambari moja kwa kuzoa alama mia tatu na sabini. Hili halikunifurahisha hata kidogo. Mtihani ulikuwa ni, nani angenilipia karo ya shule ya upili. Eti mama Zitu! Huyo hawezi kuharibu pesa zake kwa kulipia Heri karo. Hata anaafadhalisha kuzimwaga baharini.

Siku ilianza vyema kama siku nyingine yoyote. Sikuwa na budi kuzikumbatia gange zangu za siku. Ulikuwa ni mwendo wa saa nne, mama aliniita huku akiingia sebuleni nilimokuwa nikifagia. "Heri?" " Naam mama," niliitika. "Umevisafisha vyombo?" Aliuliza. " Nafagia nyumba kisha nivisafishe." Umechota maji?" Aliuliza." L...l...l...la," nilijibu kwa kubwabwaja. "Unangoja nini? Ee! Kazi yako ni kula tu sivyo?" Alinifokea. "Mama, nimepika chai saa hii tukanywa na nikarejelea kazi zangu. Hata mi...." Kabla sijamaliza usemi wangu, nilimtazama nikamwona jinsi alivyopandwa na mori.

Alinimalizia maneno yale."Hata wewe huchoka?" Aliuliza kwa kejeli. "Sikukusudia kusema hivyo," nilisema kwa woga. "Ulikusudia kusema nini mpumbavu?" Niliamua kujipa ujasiri bandia. Nilijiwashia moto wa kunioka ningali hai. Alianza kutafuta msema kweli chini ya kiti. Nilijifanya ninamsaidia kutafuta. Nilitafuta chini ya kiti karibu na mlango. Kisha nikachapua miguu wanguwangu kuelekea barabarani. Mama naye alitoka mle na jifimbo mkononi. Mchakamchaka chinja, mchakamchaka chinja. Baraste ilitutambua kuwa vigogo wa mbio. Tulipofika kwenye mlima alipoteza matumaini na kusimama." Nenda kabisa! Na ukirudi nitaku....," hakumaliza kauli yake.

Niliamua kujisetiri karibu na mti wa mkuyu. “Niache!" “Heri! Usiniogope, ni mimi Katu,” alisema kwa huruma. Naomba maji ninywe,”. Aliingia garini na kurejea na chupa ya maji. Niliyapiga mafunda mazito. Nilikonga kiu. Nilipata nguvu. “Wasema wewe ni mtoto wa mzee Papatu na mama Subira?” Niliuliza. “Ndiyo,” Katu aliitika. “Magari kwetu yalizikwa pamoja na wazazi wangu wewe ukalitoa wapi? Katu alishindwa kujieleza. Aliingia garini na kukitoa kisanduku tulichokificha. Kilikuwa na kufuli jipya. Nilibung'aa. Tulikumbatiana kwa huzuni na furaha. Tuliabiri gari kuelekea nyumbani. Mama Zitu alipoliona gari alisimama katikati ya mlango. Hatukuwa na haraka ya kutoka garini. Ilimbidi ajongee karibu ili kujua waliokuwa mle. “U hali gani?" Alimsabahi Katu. Nafikiri hakuniona."Ni buheri wa afya mama.” “Nikusaidie vipi umepotea? Katu!" “Ndiyo mama." Mama alichanganyikiwa. “Ile sumu uliyoila usiku wa siku ile, hukufa! Na kipigo kile pia hakikukudhuru?” Nilihisi mzizimo wa hasira.

“Mama, nimerudi lakini sitakuwa mzigo wako. Naomba kwa leo tulale jikoni na kakangu kesho tutajipanga. Nimezungumza na mhandisi atakayekuja kuanza kunijengea nyumba" Katu alisema huku akiashiria chumba ambacho kilikuwa kimejiinamia kwa masikitiko. “Usilete hata maji ya kunywa, " aliongeza. Mama Zitu alionekana mwenye hawafu. “Ulipotoka hapa ulienda vipi?" Niliuliza baada ya kuutandika mkeka na kuukalia." Usiulize, ni safari

ndefu. “Wanangu, naomba mnisamehe,” machozi yalimtoka huku akianguka kwenye magoti." Najua niliyoyatenda hayakuwa mazuri, nilimuua mama yenu pamoja na b-b-b-ba-ba yenu." Mama Zitu alisema huku kilio kikimzidi. "Naomba shufaa, sifai kuishi hapa tena. Nasikitika sana moyoni,” alisema kwa huzuni.

“Ripoti hizo tunazo hatuna ubaya nawe. Tumekusamehe" Katu alisema. Mama aliamka na kuondoka polepole bila neno. Aibu ilimvaa na kumtawala. Usiku ulikuwa tayari umeingia. Nanigwanzula walionekana kote chumbani mle. Katu alitoa chakula alichokuwa amekinunua tukaushtaki ubao.

Bado nilikuwa mwingi wa maswali. “Ulisema wewe ni mhasibu? Kulienda vipi hadi ukapata nafasi ya kusomea taaluma hii?". Katu hakumpa jibu ila alimpa ahadi ya kumweleza baada ya kumaliza hatima yake. “Hizi hapa ni hatimiliki za shamba hili, na hivi ni vyeti vya hazina za benki. Katu aliporudi, nilitabasamu tena.

| ***Jitathmini:*** |
|---|
| ***a)*** *Kulingana na hadithi hii saa thenashara ni saa ngapi?*<br>***b)*** *Taja tamathali za usemi zilizotumika katika hadithi hii.*<br>***c)*** *Kwa maneno yasiyopungua ukurasa mmoja unusu, eleza umuhimu wa malezi bora kwa mtoto.* |

# TUNDU LA TAMAA na Vitalis Nadecho

Taifa la Wasakatonge lilikuwa linapona makovu ya moyo. Ulikuwa uchaguzi uliojaa sera za upepo. Wengine wakitumia nafasi hiyo kuwashawishi wapiga kura "*kuwakumbuka debeni"*. Wawaniaji wa nyadhifa mbalimbali walijitosa ulingoni kujaribu bahati zao. Wadhifa wa urais ulimezewa mate na wenye nafasi serikalini. Wote walikuwa wameidhinishwa na tume ya uchaguzi na mipaka ya taifa hilo. Kila mgombea alikuwa na matumaini si haba kutia guu ikuluni.

Kila mgombea alikuwa na manifesto yake ambayo aliamini kuwa bora kuliko ya wenzake. Wananchi walizifurahia sana kampeni hizo kwani walikuwa na hakika ya kurejea viamboni wakiwa na "*mifuko iliyoshiba*," mashatitao na leso zenye picha kubwa za mgombeaji. Mikutano haikukosa nyimbo za kukashifu wapinzani na hata kufichuana sakata mbalimbali katika idara za serikali.

Kivumbi kikali kilitarajiwa kati ya Bw. Fadhili na mpinzani wake Bw. Shoto.Wawili hao walikuwa marafiki wa dhati wala sio wa chati kabla ya kuisambaratisha ndoa yao ya siasa na kila mmoja kufuata hamsini zake. Kipindi hicho Bw. Fadhili alikuwa kiongozi wa chama chao cha *DEMOKRASIA NA HAKI*. Walifahamiana namna mtu afahamuvyo kitanga cha mkonowe. Mielekeo hii tofauti iliwafanya viongozi hawa wawili kutopikika katika chungu kimoja na labda kumfanya kila mmoja kubisha mlango wa ikulu. Bw. Fadhili alikuwa mchache wa maneno labda kutokana na ukongwe uliomnyemelea huku mpinzani wake mkuu akiwa chiriku. Hata hivyo Bw. Shoto alitumia uwezo wake kifedha kuinua jamii kwa kuwapa misaada huku mwenzake akitegemea historia yake katika siasa za kanda na vilevile wingi wa maeneo yaliyomwahidi kumuunga mkono.

Siku ya uchaguzi iliwadia. Wananchi walijitokeza kiasi cha haja kwenye vituo vyao ili kutimiza jukumu lao la kuchagua viongozi waliowaridhisha katika kampeni. Licha ya kuwa kinyume cha sheria kupigia debe kiongozi yeyote siku hiyo, wapo walioonekana wakitoa chauchau kwa wapiga kura nao baadhi ya wapiga kura wakiendeleza kauli yao ya "KULA KWA MAFISADI, KURA KWA VIONGOZI". Vyombo vya habari navyo vilikuwa vimejenga mahema katika maeneo yale ili kuangazia kila tukio huku vikosi vya usalama navyo vikishika doria.

Bw. Shoto alifika katika shule ya msingi ya Mambo kwa shangingi jeupe tamthili ya theluji saa tatu asubuhi pamoja na mkewe na mwanawe. Punde tu baada yao kutimiza wajibu wao wa kisheria, kundi la vijana liliwaandama huku wakipaza sauti za kumshabikia. Hatua hiyo iliwakera walindausalama na kuwalazimu kuwatawanya huku kiongozi akijitoma garini na kulitia moto. Shughuli za upigaji kura ziliendelea na hatimaye vituo vyote vikafungwa majira ya saa kumi na moja jioni. Ama kweli ulikuwa uchaguzi wa aina yake. Tofauti na chaguzi zilizotangulia, wapiga kura walijitokeza kwa wingi wakiwemo wakongwe. Baadhi yao wakipata ufadhili wa usafiri kuwawezesha kupiga kura.

Shughuli kwenye vituo vya upigaji kura zilipofikia tamati, masanduku yalisafirishwa na wasimamizi wa vituo kwa magari hadi kwenye kituo rasmi cha kujumlisha kura hizo. Wengi wa Wanasakatonge ambao hawakuwa na uwezo wa kumiliki runinga walifuatilia shughuli hiyo nzima kwenye rungoya huku kituo cha Fichua kikimiliki idhini ya kuyapeperusha matokeo hayo ya uchaguzi. Baadhi ya maajenti na wanahabari hawakuruhusiwa kwenye maeneo ya kujumlisha kura. Amirijeshi alitoa amri hiyo. Chambilecho angurumapo simba mcheza ni nani?

Baada ya siku mbili matokeo yalitangazwa. Asilimia kubwa ya wawaniaji kupitia chama cha Bw. Fadhili aliyekuwa rafiki wa karibu wa rais Tundu walirambishwa sakafu. Dalili ya mvua ni mawingu, wengi wa wananchi wakawa na tumaini la uongozi mpya ambao ungekosa chembechembe za migomo, dhuluma na chichimiri. Migomo iliambatana na vifo vya wananchi kiholela wasipate wa kuwapa huduma hiyo muhimu. Ijapokuwa mgomo kwa kudai haki uliorodheshwa kama haki kwenye katiba hiyo ya taifa la Wasakatonge, wahusika hawakuwa na lao kwani walipigwa kalamu na hata kunyimwa mishahara.

Mwenyekiti wa tume huru ya uchaguzi alianza kwa kuwashukuru wananchi kwa kujitokeza kupiga kura na kudumisha utulivu tume ilipokuwa ikijumuisha kura hizo. Alihitimisha kwa kumtangaza mshindi wa uchaguzi. “Mshindi wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu ni Bw. Fadhili Kombe aliyenyakua asilimia hamsini na tatu ya kura zote naye Bw Shoto akanyakua asilimia arubaini na tano huku asilimia iliyosalia ikitwaliwa na wagombea wengine.” Hamaki zilidhihirika miongoni mwa wapinzani. Makachinja walipata kazi. Wapo waliobumburushwa usiku wa mashetani wakiwa ulilini na kufanyiwa madhila nao akina mama wakibakwa na kuachwa hoi. Maeneo mengi ya

biashara yaliporwa huku makao ya wengi yakichomwa moto. Damu ilitapakaa. Tai walifaidi kitoweo cha miili ya watu.

Bw. Shoto na aila yake walikimbilia nchini Wangwana. Hapakuwa na wa kuwauni wananchi isipokuwa wanaharakati waliojaribu kupaza sauti ya kuikashifu serikali kupitia magazeti kutokana na utepetevu wao katika kukomesha vurumai iliyokuwa ikishuhudiwa nchini.

Muda ulivyozidi kusonga ndivyo miji mikuu ilivyobadilika na kuwa kumbi za vita nayo mawingu ya moshi uliotokana na uchomaji wa magurudumu yakiwa kitambulisho katika sehemu nyingi. Lisilobudi hutendwa, muungano wa mataifa uliamua liwalo na liwe ili kuliokoa jahazi la nchi ya Wasakatonge lililokuwa limetota maji likinusia kuzama.

Ripoti ya uchunguzi ilitumwa kwa uongozi wa kimataifa nao ukataka pawe na mazungumzo ya kitaifa miongoni mwa wagombea wote. Mazungumzo hayo yangemhusisha rais Tundu pia ambaye umri ulikuwa umempiga chenga na aliyekuwa anatundika daluga za uongozi wa taifa na kumpisha mwenzake ambaye angemrithi. Baadhi ya mapendekezo yalijumuisha kuhesabiwa upya kwa kura, kurudiwa kwa uchaguzi au kubuniwa kwa serikali mpya yenye rais, naibu wake na nafasi ya waziri mkuu ambayo ingetwaaliwa na mpinzani wa karibu wa rais. Suala la kuhesabiwa upya kwa kura lilipingwa vikali huku wengi wakisisitiza kuwa matokeo hayo yangesalia tu yalivyokuwa kutokana na idadi ya karatasi za kupigia kura zilizokuwa zimezidishwa wakati wa uchapishaji. Wapo waliokataa marudio ya uchaguzi na kubuniwa kwa serikali ya mseto yasifanyike wakizitaja gharama kuongezeka ukiwa mzigo kwa Wasakatonge waliokuwa na deni kubwa la Benki Kuu Ulimwenguni. Ama kwa kweli fahali wawili wapiganapo ziumiazo ni nyasi. Wananchi walizidi kufa kwa bunduki, panga, kuteketezwa huku njaa ikiwavaa na kuishi nao.

Kiburi ni kaburi, rais Tundu aliona taifa lake likiangamia, woga ukamwingia kutokana na hatua ambayo ingechukuliwa na Umoja wa Mataifa. Je, angefungwa jela au kukabiliwa na vikosi vya Umoja wa Mataifa kama alivyofanyiwa mwenzake wa taifa la Walokole? Alizungumza kupitia vyombo vya habari na kuwaomba Wasakatonge kutulia ili wasubiri mazungumzo kufanywa. Wananchi nao walitii wakasitisha vita. Bila shaka rais Tundu alitaka kujitakasa. Chambilecho maasi hufilisi heri ya mtu. Uamuzi huo ulikaribisha mazungumzo mapya ambayo kwa mara hii yalizaa matunda. Rais Tundu ambaye kipindi chake cha kuongoza kilikuwa kinafika ukingoni alisalia

uongozini kwa kipindi zaidi ya miaka miwili. Wananchi hawakupendezwa na hatua hiyo.

Wapinzani wale wa kiti cha urais: Bw. Fadhili na Bw. Shoto walihitaji kusubiri wenyewe wakieneza "*injili*" ya subira kuwa ufunguo wa faraja kwa wafuasi wao ambao walikosa utulivu wakimtaka rais Tundu ang'atuke uongozini. Mazungumzo yalipotamatika, uchaguzi mpya uliandaliwa naye Shoto aliyeibuka mshindi, akiwajumuisha wapinzani wake wote kwenye uongozi wake huku baadhi yao wakiteuliwa mawaziri na waliosalia mabalozi. Ama kwa kweli simulizi la babu Busara akiwa chini ya mfenesi katika kijiji cha Adabu kiliwateka akili na kuwaliza wajukuu jioni hiyo wakila ugali wa bada kwenye mwangaza wa mbalamwezi.

***Jitathmini:***

*a) Jadili maudhui manne yanayojitokeza*
*b) Eleza sifa za wahusika wafuatao: Rais Tundu, Bw. Shoto.*
*c) Andika insha inayodhihirisha methali; Amani haipatikani ila kwa ncha ya upanga.*

# ELIMU YA SUMU na Kamoti A. Nalianya

Ustaarabu ni nini? Ni kiumbe hai au kisicho na uhai? Kinapatikana katika uhalisia wa kileo au kikale? Kipo au kinapatikana kwenye ombwe tupu la sayari isiyo na jina? Wakwisha alikuwa amejipweteka kochini huku akitazama runinga kwenye kijirununu chake cha bei ya mkia wa mbuzi. Kwani angewezaje kununua rununu yenye jina rununu? Angepata wapi fulusi ya kununulia? Alifikiria namna angepata ajira kutokana na kisomo chake bandia alichopata skulini. Si dubwasha linaloonekana mbele ya watu kwenye kiwiliwili kwa mtu. Anajuta jinsi utu wa kumfanya awe mtu ulivyoondoshwa na kudondoshwa na wale aliowaamini.

Wakwisha alikuwa amefuzu chuoni na kuona ndio wakati mkoko ulikuwa umealika maua maishani mwake. Alikuwa tayari kuyalia kivulini yale yote aliyoyachuma juani kwa muda wa mwongo mmoja hivi. “Ningesalia chumba cha sita.” Moyoni mwa Wakwisha yalimpita mawazo aula kuwa miongoni mwa mapwagu wasiojua ba wala be katika ulingo wa elimu lakini wanaselelea katika ukwasi wa kupigiwa mifano. Pengine ningekuwa na akili nyingi ya kutafuta mali mapema kuliko nitilie maanani elimu kuwa ingenifumbua macho. Elimu ingenifumbuaje macho? Ni vile sikupewa elimu bali nilielekezwa kupita mtihani na kubisha malango ya taasisi ya elimu ya juu nchini.

Kumbe elimu si mtihani. Elimu si kubebwa na wanajamii na kuonyeshwa kwenye runinga au picha kubwa kubwa za waliofanya vyema. Kumbe elimu ni kuelimika kwa maarifa na utaalamu. Hii ndiyo sababu kubwa iliyomfanya Wakwisha kukosa kazi katika taasisi na ofisi aliyobisha. Hakuwa na chembechembe zozote za elimu. Alikuwa mbumbumbu.

Wakwisha alimhusudu babu yake Wakima na nyanya yake Nyakima waliosheheni hekima kuliko wenye hekima wote ulimwenguni. “Mitihani sikuifanya, nilifanyiwa, tulifanyiwa, walifanyiwa, sote hatukuifanya. Si mwaka wangu tu bali pia miaka kadhaa iliyotutangulia sisi na waliotufuata sote tulipata elimu chapwa. Elimu ya kuupita mtihani bila kuufanya mtihani wenyewe; tulifanyiwa na watahini.” Wakwisha anakumbuka walimu wake aliowaheshimu wakipita hapa na pale, wakifanya juu chini ili apate alama nzuri katika chumba cha nane. Hisabati kwake alijua tu tarakimu sufuri hadi tisa, Sayansi haikuwa lolote wala chochote, hakuelewa kitu. Alipita vyema sana. Pengine alipata maki themanini au tisini kwa kila somo. Alama zilizomwezesha Wakwisha kupata

nafasi katika mojawapo ya shule nzuri nchini. Wengi walidhani angeshindwa katika shule hiyo lakini wapi? Mkondo ulikuwa ule ule, tabia ikawa ile ile ya kupita mitihani kwa kufanyiwa. Kweli tabia ni ngozi huwezi kuivua. Nani aliyehusika kumfanyia mitihani?

Leo Wakwisha ameketi kwenye kochi ambalo limehifadhiwa katika mojawapo ya majumba makubwa kijijini pao. Jumba hili si eti wazazi wake walilijenga. La hasha. Hawakulinunua, hawakupewa, walilichukua. Walikuwa wazazi wenye nafasi maishani. Nafasi ya kupata watakacho, hata ya kumpeleka mwanao katika shule waliyoitaka, walikuwa nayo. Uzima ndio waliokosa kuununua kwa fulusi. Jumba hilo lilikuwa la mlowezi. Walipoondoka kijijini, mmoja wa wafanyakazi wao ambaye alikuwa mtumwa aliyejua siri za kurithi vinavyorithiwa alilirithi jumba hili. Mzee Subiri aliyekuwa wembe darasani mwetu ndiye aliyekuwa mmiliki wa jumba hili.

Mzee Subiri alikuwa mkulima hodari sana enzi hizo. Alilima kile kilichostahili kulimwa. Si matunda, si michai, si kahawa. Kile tulichojua. Alikuwa akila faida ya jasho lake. Ingekuwa leo angebandikwa majina ya: anayejuana na wakubwa au anayefanya kazi kwa kaunti. Faida yake ingeliwa na wengine iwapo angezaliwa katika karne hii.

Wakwisha alishangaa vile wanyonge walivyonyanyaswa na wenye uwezo katika jamii. Eti jumba hili ni lao sasa. Alimhurumia Mzee Subira.

Kabla ya kupata kazi hii ya udaktari, Wakisha alizunguka sana. Udaktari wenyewe haujui. Hautambui. Haufahamu. Si uongo nikisema wahadhiri wake hawakupenda ngwenje! Labda walipenda mabinti wa kiwaridi. Vitu hivi viwili vilimfanya Wakwisha kuwa na wakati rahisi chuoni.

“Mimi ninashangaa iwapo madaktari tajika ni kama mimi zumbukuku sijitambui, sijielewi, sijifahamu. Ni wale wataalamu waliotaalamika au wanaobambanya kama wale waganga wa mitishamba. Nashangaa mgonjwa aliye hali mahututi si hayati si mamati hajaumbwa hajaumbika mwenye ndwele za mguu yaani dondandugu anafanyiwa upasuaji wa ubongo. Kuna uhusiano gani baina ya kidonda na ubongo? Wapita mitihani kwa njia yoyote. Bora wamepita tu si kutaalamika katika nyanja zao za kitaaluma. Bila shaka kuna shida mahali. Wakwisha alipigwa kalamu baada ya wiki moja.

Kupita mtihani hushabikiwa na wote pasi na kutathmini mchakato mzima wa kupata alama hizi bora, eti heri mwisho wa jambo kuliko mchakato wa mwisho wa jambo lenyewe.

Wakwisha anamhusudu Subira, msichana aliyekosa karo ya kujiunga na shule ya upili nzuri na kujiunga na shule mojawapo kijijini. Subira aliamua kufuata nyayo za baba yake aliyekuwa mtoto wa pekee wa kiume wa babu mtu Mzee Subiri. Mzee aliyenyakuliwa shamba lake kubwa na jumba la wakoloni. Subira alijiunga na chuo cha kiufundi na kuhitimu kwa stashahada kwenye ususi. Yeye ni msusi hodari na tajika. Kazi hii anaifanya mwenyewe na kujipatia pato la haki bila kumwibia mtu. Kwani anayesukwa huona hakika Subira amefanya kazi. Kujitegemea kwa lile alilojifunza shuleni kwa bidii alizoweka masomoni. Yeye hakupata alama zile za kuwekwa kwenye gazeti au abebwe hobelehobela aonekane kwenye runinga. Hivi sasa ana amani na imani ya kuishi. Hajatamauka kama wengine wetu tuliozoa sifa sufufu na wananchi wote waliotuona kwenye runinga. Hatuna kazi. Hata kama kazi zingekiwepo, hatuna ujuzi. Hatujijui hatujielewi. Hatuwezi kuifanya kazi hiyo inavyowiana na kisomo chetu ghushi. "Huu msongo wa mawazo na haya maradhi yasiyo na tiba yatakuja kuniondoa duniani," Wakwisha alijisikitikia.

Ilikuwa ni bayana na waziwazi kama meno ya ngiri kuwa matokeo ya miaka minne chuoni sasa kwa uhalisia imegeuka karne ya miaka na mikaka.

Majibu ya mfuata nyuki kuramba asali. Asali chungu katika maisha matamu mafupi ya usasa. Nani kasema raha jipe mwenywe. Karaha uwape wavyele wako na kizazi chako. Wakwisha kwa sasa si waridi tena wa kuwavutia wahadhiri na watu wengi tajika maishani. Si matajiri, si vijana wenye misuli na misirimbi na mapandikizi ya majinyama tebwere tebwere. Wote walimpenda Wakwisha.

Anakumbuka mikahawa mikubwa alikokwenda wajuao walisema *five-star hotel*. Aliishi huko, alisahau kuishi ni kuisha na maisha huisha. Kumbe vya kutotolewa jasho havitunzwi. Hifadhi yake ya baruapepe bado imejaa picha za aina zote. Anajuta. Maisha ni gurudumu linalokimbia na kuisha. Kwa sasa hajielewi. Hana siha, hana kazi, hana elimu, hana mama, hana kila kitu. Hana hanani. Ni msafiri aliye katika bandari ya dunia anangoja safari. Safari ya kwenda na kutorudi milele.

Anamlaumu kila mtu. Anawalaumu walimu wake, wazazi wake. Anailaumu dunia kwa kutomhurumia. Dhuluma zilimfanya ajifie mbichi wakati ambao ukoko umealika maua ya maisha yake.

Mama yake alifariki kwa kuvuja damu ndani ya mwili, ndani ya nafsi yake na hisia zake. "Labda mamangu angeishi kama Mola angemjalia mwana wa kiume".

Baba alijuta kwa kutumia mali aliyoachiwa na babu yangu kutulipia karo katika shule hizo zilizoingiza mwiba kwenye maisha yangu. Mama. “Siishi maisha. Naishi duniani kupitisha muda. Usasa ni tambara mbovu, kiumbe usiuengemee.” Wakisha alimeza sumu ya elimu.

***Jitathmini:***

*Labda mamangu angeishi kama Mola angemjalia mwana wa kiume.*

*a) Weka maneno haya katika muktadha wake.*

*b) Eleza sifa tatu za mzungumzaji.*

*c) Jadili jinsi maisha ya msemaji yamezamishwa na “meli ya usasa”*

# PANG’OKAPO JINO na Onkoba Humphrey

Pana nafasi bila shaka. Mama Farida alikuwa amehitimu miezi tisa. Ving’ora vya ambulensi vilihanikiza katika janibu ya mtaa wa Madongo. Baba Farida alikuwa amejifunga kibwebwe kwenda kusaka gari hilo ambalo lingemwauni Mama Farida pindi tu uchungu wa uzazi ungeanza kumwandama. Dereva pamoja na tabibu walitoka nje wakiwa wamebeba machela tayari kumfaa Mama Farida. Baba Farida naye alitoka huku akitafuna mariungi. Alipenda sana kutafuna njiti za mmea huo. Mama Farida alikuwa amesita kupiga kite na kugaragara huku na kule. Uchungu wa uzazi haukumpa starehe kamwe, alikuwa kwenye bahari kuu, hakuwa wa maji wala wa dawa. Hali yake ilikuwa taabani. Tabibu alijizatiti kumpima joto kisha kwa usaidizi wa dereva wake wakamwinua juu kwa juu na kumlaza kwenye machela. Mama Farida alifikishwa kwenye hospitali ya wilaya na kuwapata wakunga wakiwa ange kumlaki. Alipokelewa kwa mikono miwili huku baba Farida akiwa ameachama asijue asaidie wapi wala atende lipi, alibung’aa tu”

Baba na Mama Farida, mapenzi yao yaling’oa nanga katika kikataa cha bibi ya Mama Farida. Walihamia mtaa wa Madongo. Mtaa ambao wakazi wake ni wenye kipato cha chini. Asilimia kubwa ya waja ni akina pangu pakavu wakiulizwa hawaungami.

Maisha yalikuwa raha mustarehe kati ya mahabuba hawa wawili. Walisaidiana gange zote. Walifahamu fika kuwa; mkono mmoja hauchinji ng'ombe.

Siku moja magharibi baada ya jua kutuliza miale yake nyuma ya safu ya milima ya Mikokotolo, mahabuba hawa waliketi chini ya mzambarau uliokuwa mkabala na kibanda chao cha msonge. Walinong’onezeana na kulishana nyama ya ulimi, ombi lao kwa Maulana lilikuwa moja tu, awabariki na kizazi kizuri cha kike. Hapo wakala yamini kuwa watakiita Farida na kuanzia kiapo hicho wakaanza kuitana Baba Farida na Mama Farida. Mapenzi yao yalinoga hata adinasi wengine wakawalilia ngoa. Kila walipopita barabarani au sokoni huku wameshikana nyonga, usingekosa kusikia mighuno na minung’uniko kutoka kwa waja. “Mmmh, msijali ni wengi walianza hivyo na leo hawapo pamoja, waliachana.” Hivyo ndivyo walivyokebehiwa na wenzao. La kushangaza ni kwamba hawakuyatilia mabezo hayo maanani, waligeuka sikio la kufa lisilosikia dawa.

Baba Farida alikuwa na matumaini makuu, alijiona amesalia na dakika chache mno kuwa Baba Farida wa halali na kweli. Alimwombea Mama Farida aweze kupata salama; Farida. Wakunga walionyesha bidii ya mchwa, walijifunga mkaja ili kumwokoa Mama Farida kwa sababu alikuwa amechoka sana kutokana na safari ya masafa marefu iliyokuwa imetatizwa na muundo msingi duni wa barabara. Moyo wake ulipapa kwa kasi. Mama Farida alijikaza mpaka kikembe cha kike kikakopolewa, wadi nzima ilijaa ng'a! Ng'a! Ng'a! Tabasamu na furaha ilidhihirika dhahiri shahiri wajihini pa Mama Farida. Baba Farida naye hakuwachwa nyuma, alimkumbatia Mama Farida na kumpongeza. "Nakuenzi ewe Farida ja mboni ya jicho la". Mama Farida hakumaliza kauli yake alianza kubanwa na kikohozi huku akijaribu kukohoa kohoa, machozi yalianza kumtoka kwa michirizi, pumzi ni kama zilianza kumkimbia, kifua kikajaa ni kana kwamba alikuwa anasakamwa na mfupa kooni.

Baba Farida alimchukua Farida kutoka mikononi mwake na kuwaita wakunga. Kabla ya kuku kumeza punje, wakunga walifika hapo na kuanza kujaribu kuyaokoa maisha ya Mama Farida. Aliwekwa kwenye oksijeni. Majonzi yalitwaa anga iliyokuwa imegubikwa na furaha. Mama Farida alianza kurusha rusha miguu kisha akakata kamba. Baba Farida hakuamini aliyoyaona. Alilia kwa mashaka. kubana kekevu lakini uchungu ulimsaliti. Aliifungulia mifereji ya machozi na kuyawacha yatiririke tiriri. Machozi yalimcharaza bila huruma. Nani angemtilia pondo katika malezi ya Farida? Alifadhaika hata zaidi. "Mama Farida, *wake up please"*

Mwili wa mama Farida uliondolewa na kupelekwa kwenye makafani. Farida alisalia hospitalini mikononi mwa manesi. Baba Farida alirejea kiamboni na kuungana na majirani katika maandalizi ya maziko. Mchuma janga hula na wa kwao. Janga hili lilikuwa limegubika wanamadongo wote hata wale waliokuwa wakimsimanga Mama Farida waliungana na Baba Farida kuchangisha pesa ili angalau wampe mkewe mazishi ya kufana. Umati wa watu ulikusanyika kila jioni katika kiambo cha Baba Farida. Waliendeleza kuchangisha ngwenje za kulipia ada ya ufuo. Mbolezi ziliimbwa kila jioni kiza kilipobisha hodi. Huzuni na furaha zilihanikiza hewani. Watani walijaribu kumchangamsha bwana huyu, alijilazimisha tu, akajitia tabasamu bandia japo ndani yake alikuwa akiugulika kwa kutengana na mkewe.

Baada ya siku saba, marehemu aliletwa nyumbani ili kuuaga mji wake kulingana na tamatuduni za wanamadongo. Baada ya maziko, kina mama wachache walisalia kuendeleza kazi za nadhafa. Walinadhifisha kila kitu.

Jumatatu alfajiri na mapema baba Farida alirauka na kujikokota hadi hamamuni. Mwili wake ulikuwa umemkataa kutokana na mavune yaliyokuwa yakimng’ata kama nge. Baada ya kuvalia magwanda yake alijirashia marashi ya karafuu angalau anukie vyema. Kisha akashika tariki kuelekea hospitalini. Alienda kumchukua bintiye Farida kwani ndivyo alivyohitajika kufanya baada ya mazishi. Hospitalini, alilakiwa na wauguzi wawili waliokuwa wakijiandaa kufunga zamu. Walimkabidhi mwanawe. Safari ya malezi ilipiga kwata maishani mwa Baba Farida na Farida. Kulea kulikuwa kibarua kigumu. Alijikaza usiku kucha na mchana kutwa kumpa Farida kila kitu alichostahili. Farida alianza kusota kisha kutambaa kwa magoti yake teketeke halafu hatimaye akasimama dede.

Farida alikuwa sasa ametimu miaka minane tangu akopolewe na kuingia humu duniani. Siku moja akiwa nyumbani jioni alisikia milio ya bundi ikitwaa anga. Alitoka nje kwenda kumwangalia ndege huyo. Aliporusha macho yake angani yalitua juu ya mzambarau uliokuwa umekomaa ubavuni mwa nyumba yao ya msonge. Aliinama chini na kuokota jiwe, jiwe alilotumia kumlenga yule adui wa waja. Ilisemekana ndege huyo akilialia karibu na kwenu jambo baya laweza kutendeka hasa mauti. Farida alifahamu fika hatari ya ndege yule kuwepo hapo. Giza totoro lilishamiri nje, milio ya kereng’ende na vyura ilizagaa kila mahali, Farida aliingiwa na hawafu. Aligwaya mno na kuanza kutetemeka. Alikimbia na kuingia ndani ya nyumba yao.

Farida hakuamini macho yake, babake alikuwa akiungua bila kujua. Ukemi na kilio. Farida alipiga kamsa. Moto ulinyakua roho yake. Farida aliachwa yatima. Mti mkuu ukigwa wana wa nyuni huyumba. Farida alisalia kuyumba na kutapatapa ja ndege tunduni. Alimtegemea nyanyake na majirani kwa lishe. Nyanya yake alimgeuka kwani alijigeuza lumbwi, alianza kumsimanga Farida kwa kudai yeye si mjukuu wake kwa sababu babake alipungia dunia mkono wa buriani kabla ya kulipa mahari ya mamake. Alimwonya asithubutu kumwita nyanya.

Kifo cha Baba Farida kilikuwa cha ghafla, ripoti ya daktari ilieleza bayana kwamba alifariki kutokana na majeraha aliyoyapata kwenye uti wa mgongo akiwa kazini katika machimbo ya umma, alipokuwa akiendeleza kazi zake za kuchimba migodi. Daktari alihimiza kampuni husika ilipe fidia kwa aila yake. Hapo ndipo mchezo wa paka na panya ulidhihirika. Wakuu wa kampuni walimzungusha bibi yake Farida. Hawakuwa na nia ya kumlipa fidia. Kila siku kulipokucha alikuwa kiguu na njia hadi kwenye ofisi za kampuni hiyo. Bibi

alipowasili huko alilakiwa na makufuli makubwa kwenye tumbuu za milango ya chuma. Miaka nenda miaka rudi, matumaini ya bibi huyo kupata haki yake yalididimia. Hilo lilisababisha kumfurusha Farida. Pengo lililoachwa na kifo cha babake lilizidi kuonekana wazi kwa sababu Farida hakuwa na mtetezi. Hakujua angeelekea wapi maana bibi yake alikuwa amekata uhusiano naye. Elimu yake ilifikia tamati. Hakuwa na wa kumfadhili wala kumwokoa.

Alijiunga na vijana wa mtaani. Vijana hao walikuwa na kadhia sawa na ya Farida. Matini ya aushi ya Farida yalikuwa yanafanana kama riale kwa ya pili na vijana wenzake. Zahama za kila nui zilijaa katika mitaa, si ubakaji, si wizi, si mauaji, vyote viliwasakama kina Farida na wenzake.

Jioni moja Farida alipata ujumbe kuwa alitakikana kufika kwa Masta. Masta ndiye aliyekuwa kigogo wa mtaa, yeye ndiye aliyekuwa akilinda himaya hiyo. Kila mja mgeni angefika kwake kwa usaili ndiposa aruhusiwe kuishi hapo. Masta alikuwa akiogopewa sana kama ugonjwa wa tauni madhali alikuwa mkali sana. Farida alijipa moyo na kujikokota mpaka kwake. “Fuata kanuni za hapa binti mdogo, piga magoti mara moja.” Sauti ya Masta ilipasua anga mithili ya radi. “Samahani Masta, nisamehe. Niwie radhi kwa usahaulifu wangu.” Farida alijitetea. “Haya basi, simama kititi na upige saluti kisha useme *yes* Masta!” Farida alifanya kama alivyoagizwa na Masta. Udogo wake kimwili ulimfanya akae kama kibonzo. Kitendo hicho kilimfanya Masta aangue kicheko. Inasemekana kuwa ilikuwa mara ya kwanza kicheko kusikika kutoka kinywani mwake. Alimdadisi hata bila salamu “Nina mzigo ambao ningetaka unisaidie kuusafirisha. Ukimudu kuufikisha kule basi utakuwa umefuzu ubatizo wetu.” “Ubatizo wa maji au wa moto huu? Sidhani nitauweza mzigo huo. Mimi ningali mdo,” “Udogo huo haswa ndio utakaotufaa katika biashara hii. Nisikize kwa makini, kama wadai makazi na malazi itakubidi utende hili.” “Sina budi, lisilobudi hutendwa. Kama ndio ufunguo wangu wa kuishi hapa basi nipo tayari kujaribu kuusafirisha mzigo wenyewe.” “Sadakta Farida. Anza kazi. Peleka mzigo huu hadi kwenye angatua ya Dongo. Utawapata wenyeji wakikusubiri hapo. Hakikisha humfichulii yeyote yaliyo mkobani.”

Farida alichukua mkoba na kung’oa nanga. Alipita kwenye vichochoro vilivyojaa mitaro yenye majitaka, harufu mbaya zilizohanikiza kila pembe nusura zilipue pua ya Farida kutoka wajihini mwake. Giza lilikuwa limetanda lakini mwangaza kutoka kwenye mbalamwezi na thurea ya nyota ulimfaa sana Farida. Farida alijikakamua na kufika kwenye angatua hiyo. Alizunguka kila mahali akiwasaka wenyeji wake waupokee mzigo wao. Hakukuwa na ishara za

binadamu kuwepo hapo. Alipaza sauti na kuuliza kama kulikuwa na mja yeyote hapo. Hakupata jibu lolote. Hapo kando kulikuwa na gari kuukuu la aina ya "*Nissan*." Farida alienda na kuchungulia ndani. Lo! Kile alichoona hakuamini, maghulamu wawili na banati mmoja walikuwa wametiwa pingu na midomo yao kuzibwa kwa gundi. Farida alijawa na woga, kijasho chembamba kilimtiririka kama maji.

Askari wanne walifika mara moja na kumkamata Farida. Walipiga sachi mkoba wake na kupata vifurushi mia moja vya dawa za kulevya vikiwa vimebanana humo. Farida alipigwa mugma. Alijaribu kujitetea lakini kilio chake kiliangukia sikio la kufa ambalo bila shaka halisikii dawa. Farida alitiwa pingu na kujumuishwa na wenzake. Dunia ilimgeuka, michirizi ya machozi ilimtiririka njia nne nne. Aliandamwa na paka mweusi. Sasa amekamatwa na anashuku atakula kalenda. Farida na wenzake walisukumwa korokoroni. Walifungiwa katika seli ya watoto.

Farida alikilaumu kifo kwa masaibu yake yote. Alijua fika kwamba kama sicho kifo cha wavyele wake, maisha yake yangetengemaa na angekuwa mtu wa maana duniani. Sasa hapa mambo yamemwendea shoro. Kama sicho kifo, angemaliza masomo yake na kutimiza ndoto yake ya kuwa tabibu. Alijutia sana kugundua kuwa wazazi wake waliangamizwa na ndwele tofauti. Kama sicho kifo kumpokonya nafasi ya kulelewa na wazazi, asingejitosa kwenye utovu wa kimaadili wa usambazaji wa unga. Kama sicho kifo, Farida asingebakia mwanamkiwa yatima asiyejua namna ya kujitetea katika dunia. Dunia hii ya Rabana. Haya yote yalikuwa yakimzonga Farida akiwa gerezani, hapo ndipo alipokuja kung'amua kuwa pang'okapo jino pana nafasi kweli!

| ***Jitathmini*** |
|---|
| *a) Mayatima na wana wa wasio na nafasi katika jamii hukumbwa na matatizo mengi katika jamii. Jadili kauli hii.*<br>*b) Taja na ueleze sifa tano za Baba Farida*<br>***c)*** *Taja na ufafanue maudhui yoyote matatu yaliyojitokeza kwenye kisa cha Pangokapo jino.* |

# YAKIJA NAYATWAE na Kaka Maina

Giza la maki lilitawala kwa amri zote. Kila upembe wa ulimwengu ulikiri kushindwa kustahamili kiza cha usiku huo. Mvua ya kidindia ilianza kuadhibu kila paa. Miale mikali ya umeme na mingurumo ya radi vyote vilishirikiana kukamilisha mandhari ya usiku huo. Wakristo waliiona kama siku ya kiama huku washirikina wakihofia nguvu zao yamkini ziliwatia hatarini. Kabla ya usiku, wakazi walikuwa wameshuhudia pepo kali kutoka kusini mashariki. Mavumbi mengi yalitifuliwa na kutunga moshi mchafu uliopaa angani kwa maringo ukidhihaki afya tulivu ya anga. Wakulima walikuwa wamefanya yao na kuweka ala chini. Kilichobaki ni ombi la Mzee wa kijiji, Mzee Mubalighi aliyekuwa ametwikwa jukumu la kuongoza ibada ya maombi kila baada ya upanzi. Wengi hawakukumbuka vipi alivyoupata wadhifa huo. Kila kiumbe kiliajabia mashaka yaliyohanikiza kote. Usiku huo ndio uliomkaribisha kijana huyu wa kiume. Wazazi wake walilalamikia miungu wao kwa kuwaletea kitoto hiki katika muktadha ule.

Wazazi waliona mbinde kukitafutia kitoto hicho jina. Mipango yao yote ilifutiliwa mbali na vituko vilivyozingira kuzaliwa kwa kijana Yakija. Baba Yakija, Bwana Nayatwae alikuwa mzawa kindakindaki wa hapa kijijini. Tangu utotoni alikuwa hajapata nafasi ya kutoka nje ya ua wa kijiji hiki cha Ulimbuka. Wazazi wake Bwana Nayatwae walikuwa majadi kubeli. Licha ya kuwa walalaheri, waliikosa elimu kabisa. Walisema kuwa mali yalitosha. Aghalabu walisema kuwa akili changa ya watoto haikuhitaji zaidi ya kulishwa na kupewa muda ijikulie yenyewe.

Kutokana na ufukara huo wa elimu, kina Nayatwae wakaishia kuikubali na kuitwaa hali yao kwa mikono miwili. Laiti wangemaizi kuwa mali bila daftari hupotea bila habari. Baada ya muda wa wavyele wao kuenda waendako. Nayatwae na ndugu zake wakarithishwa mali. Ndugu hawa waligombana tokea macheo hata machweo. Kipindi kirefu cha vituko hivi kilipita. Siku moja, alfajiri pevu, kaka yake Nayatwae aliamua kuwafuata wazazi wake. Nafsi yake ikamhakikishia kuwa huko ndiko alikostahili. Akaitwaa kamba waliyozoea kukifungia kidama kimoja kifyefye kilicholishwa kwa dhiki nyingi bomani pao. Ndiye huyo, akajitia kitanzi. Binadamu ngamba, hawakosi la kuamba. Wanakijiji hawakusita kukielezea kifo kile kama *zawadi kwa* Nayatwae.

Damu ni damu si kitarasa. Licha ya utesi na ugomvi kwa mara ya kwanza walionekena pamoja. Wakaungana usiweze kujua waliwahi kuinuliana mapanga

na kumzika mwenzao. Baada ya maziko hayo, haijulikani vyema kipi kilichowaingia nduguze Nayatwae, hawakusalia pale bomani. Walihitaji kuhanja na jua alimradi wapate kujua ya ulimwengu. Walitawanyika mithili ya ndege waliopigwa manati. Kila mtu na upembe wake wa dunia. Kwenda kwao kulimbakisha Baba Yakija bomani mle. Alihangaika. Alilalamikia kila hali. Mara ungemsikia akiwalaumu wavyele wake kwa kutowapa kile alichokiita "ufunguo wa Maisha" kama alivyowahi kudokezewa na rafikiye, Jeki. Huyu Jeki alimfaa sana Nayatwae. Aliitikadi fika udugu ni kufaana wala si kufanana. Alikuwa yeye ndiye hazina ya maarifa katika aila ya Nayatwae. Ilisemekana kijijini kuwa Jeki alikuwa na mchango mkuu katika namna alivyoyaendesha maisha yake Nayatwae. Haya pamoja na mengine mengi ndiyo aliyoishi kwayo Nayatwae. Usingekuwa ni moyo wake huo wa uvumilivu basi, huenda angekuwa amekwisha kuzifuata nyayo za kaka yake mkubwa.

Ndoa kati ya Bwana Nayatwae ilikuwa haielezeki. Kikubwa zaidi ni utengano wa ardhi na mbingu, kimaisha na kielimu ulioishi baina ya wapenzi hawa. Msaada wa Jeki ulisalia kuwa mshipa wao wa uhai. Yakija hakupata amani. Kuzaliwa kwake katika majira ya kifuku kuliitishia afya yake.

Kupitia mradi wao wa *"Jamii ni sisi na sisi ni jamii"* waliamua kuungana na kuchanga bia ili kuviokoa vijiji jirani vilivyokuwa vikizidi kuzama zii katika ufukara. Makadirio yao yaliwapa uwezo wa kuwajengea wakazi wa Ulimbuka zahanati kadhaa zilizowabadilishia hali. Kuna kina Nayatwae walioona taabu sana kulikubali wazo la "dawa ngeni" na kuna wale waliokubali kuwa huu ulikuwa mwamko mpya kijijini. Mwafaka uliobadilisha na kuyaokoa maisha ya Yakija. Dawa zile za mitishamba zilikuwa si kitu. Mama yake alihiari mwanawe kujiunga na shule za Songa huku baba yake akiona ugumu wa kumtuma Yakija shuleni kabisa. Pakazuka hozahoza na gatigati chungu tele. Ushauri wa Jeki haukuwa muhimu katika muktadha huu. Juhudi za bibi mtu ndizo, kwa mara ya kwanza, zilipata nafasi ndani ya fuadi ngumu isiyopenda elimu katu "Hakuna mwanamume mbele ya mwanamke," Nayatwae alikiri kimoyomoyo.

Waliishi maisha ya "bora kuna mvua, tukilima twavuna!" Makaribisho hayo yaliwaelekeza kwenye mikono mizuri na mikunjufu ya mwalimu mkuu shuleni Songa. "Karibuni sana, naona mmechoka tiki. Poleni sana, niwasaidie kwa lipi?" Mwalimu mkuu aliwauliza kwa upole na uraufu mwingi. "Asante. Tumepoa.Tumetoka Ulimbuka tumemtaka mwana wetu kuyaanza maisha yake ya kielimu, ipo nafasi?" Mama Yakija aliomba kujua. Wakati wote huo, baba na

mwanawe walikuwa wameufyata mdomo ungedhani ni mabubu. "Ipo nafasi ya mvulana mmoja tu kwa sasa. Mna bahati ya mtende, aisee! Wasichana kijijini hapa wameyakubali masomo mno. Tunawapata ghulamu kwa nadra sana. Bila shaka hata nisingekuwa na nafasi iliyo wazi, nisingeikosa ya kijana wa kiume kama huyu. Tunawahitaji sana." Mwalimu mkuu alielezea.

Kila alfajiri ya Musa kabla ya kiza kupisha mwanga Yakija alitakiwa kuwa amerauka, akajitayarisha, akapata kisebeho akaenda shoti hadi shuleni. Ilimbidi mvuli huyu kujituma zaidi hasa ikizingatiwa kwamba alikuwa amechelewa kwa miaka miwili. Mara hii alitaka kujiasa kwa ile "haidhuru" yake lakini akajikumbusha haraka kauli yake ya mwalimu wa Kiswahili, "Haidhuru haidhuru hudhuru hatimaye." Kama kuna falsafa iliyomchukua na kumkaa sawasawa kwa haraka ilikuwa hii ya haidhuru kudhuru. Yakija alifanikiwa kuwapa wavyele wake sababu ya kutabasamu. Alifanikiwa kupata alama bora zaidi shuleni katika muhula wake wa mwisho wa mwaka. Ukosefu wa vitabu vya kiada na ziada haukuwa taabu tena. Aliitikadi kuwa yote yawezekana mradi nia ipo. Nao wote waliomzunguka hawakusita kumpa wosia wa kila aina. Wosia wa bawabu wa Songa ndio uliomfurahisha zaidi na kumtumainisha. "Sijakuona hata umechelewa isipokuwa leo. Nakuomba uukumbuke wosia wangu huu, *YAKIJA YOYOTE YALE MAISHANI, NAKUOMBA UYAPOKEE."*

Licha ya matatizo yaliyomsibu asubuhi hiyo, alipata tena kurejelea hali yake ya ukaramfu. Asubuhi ya siku hiyo ndiyo iliyompa dhiki na kilio cha kite kwa kufiwa na baba. Aliona hapakuwa na haja ya kuendelea kulia zaidi. Aliona kuwa sasa ukurasa mpya wa maisha ya nusu uyatima ulikuwa halali na halisi. Mama yake tayari alikuwa na ulemavu aliouona siku zote kama mkasa wake yeye. Siku hiyo ndefu sana hatimaye ilifikia tamati na wanafunzi wakawaaga walimu na wote pale shuleni kisha wakafumukana kila mtu na kwao. Bi. Nayatwae hakuamini taarifa za mauti ya bwana wake hadi siku halisi ya maziko. Kaburi jingine katika boma hili likajilaza na kujitandaza sawasawa kwa kejeli zote. Misalaba ya waliokuwa chini ya mishumbi ya udongo ikasalia kuutazama ulimwengu wa walioachwa kwa dhihaka kuu. Kuwahakikishia kuwa izraili yupo, na yuaja kabla ya Masia anayetazamiwa sana na Wakristo. Yakija alistahili kuyastahamili na kuyahimili haya yote hasa alipoikumbuka nasaha ya Bawabu wake shuleni.

Nalije baa liondoe baa. Msemo huu ulikosa maana katika hali ya sasa nyumbani kwa Bwana Nayatwae. Badala yake, ukweli kwamba hakuna msiba

usiokuwa na mwenziwe ulifaa zaidi kuelezea mambo yalivyokuwa. Yote yaliyojiri yalimpokonya Yakija nafasi ya kufanya mtihani wake wa mwisho. Lisilo budi hubidi. Umri wake mdogo wa mwongo mmoja unusu kwa kweli haukustahili makubwa na mazito kama haya. Yalikuwa nanga hasa. Miongoni mwa mabadiliko haya ni vita vilivyozuka baina ya vijana wa Ulimbuka na Songa. Vikosi hivi viwili, chini ya uongozi wa Harabu na mpinzani wake kutoka Songa vilipigana hadi mwisho wa pumzi zao. Wapo waliorudisha kope zao kwa Mwenyezi. Vita vikahatarisha usalama wa kina Yakija wa kwenda shuleni. Kama walifanikiwa kufika shuleni, basi ilikuwa kwa majaliwa tu. Elimu ilikuwa muhimu, lazima ingetafutwa alakulihali. Amani ilipatikana kwa juhudi za Mzee Mubalighi, "*Kasisi*" wa Kijiji cha Ulimbuka aliyepinga vikali kaulimbiu ya vita hivyo kuwa "*AMANI HAIJI ILA KWA NCHA YA UPANGA"*. Jitihada zake za kuujenga upya muamana baina ya vijiji hivi viwili ndizo zilizomwokoa Yakija dhidi ya kurudia darasa la nane tena kwa mara ya tatu. Vinginevyo asingepata nafasi ya kuuvuka Mto Bondeni akielekea shuleni.

Mzee Mubalighi sasa alikuwa mkongwe kabisa, heshima alizopewa kama namna ya kumshukuru kwa kuuleta usalama zilikuwa kubwa sana. Alitawazwa kuwa hazina ya busara na hekima baina ya vijiji hivi viwili. Siku ya Muogo ilichukua mkondo mpya. Iligeuzwa kuwa siku ya kuadhimisha ujamaa ulioanzishwa na wasomi waliokuwa wametoka Songa. Siku hii ikageuzwa jina na kupewa jipya la *Jamii ni Sisi*. Lengo la siku hiyo likageuka na kuwa siku ya kukutana kwa vijana na Mzee Mubalighi pamoja na viongozi wengine kwa nasaha na kuweka mikakati ya kuzidisha makuzi ya Haradali na mapatano mazuri baina ya mtu na mtu.

Yakija kwa sasa alikuwa amehitimu masomo yake hadi chuoni. Ingawa hakupata kazi ya kuajiriwa, alijiunga na kundi la vijana na kuanza miradi mbalimbali pale kijijini. Alihakikisha awali ya yote amewahamasisha wote katika kulijenga daraja aushi mtoni Bondeni kuwavusha wote kutoka ng'ambo moja hata ile nyingine. Alikuwa na kila sababu ya kufanya hivi, aisee! Daraja hili halikuwavusha watu tu bali pia lilileta mshikamano zaidi. Mama yake aliyekuwa kwa sasa akichungulia kaburi alifurahia sana kuyaona mabadiliko haya yote. Alitamani sana Nayatwae angalikuwa bado yu hai naye pia apate kuonja baraka hizi wazi. Shule nyingi na zahanati zilijengwa Ulimbuka na kote pamoja na kuimarishwa kwa miundomsingi. Harabu alibaki kuwa nazi iliyozidi kuoza na kuambukiza uvundo na fondogoo kwa vijana.

**Jitathmini**

a) *Eleza tamathali tano za lugha zilizotumika kwenye kisa hiki.*
b) *Kwa kurejelea Makala, fafanua ufaafu wa mada "Yakija Nayatwae."*
c) *Elimu ina manufaa mengi si tu kwa maisha ya aliyesoma bali pia kwa jamii nzima. Ukirejelea hadithi hii fafanua ukweli huu.*

## MALI YA UMANDE na Patrick Mukanga.

Mzee Obambo alikuwa ameketi chumbani kando ya kigoda akibarizi. Hiki kilikuwa chumba alichopenda kupumzikia. Madirisha yake ya vyuma yaliboreshwa na vioo vilivyobadili mandhari ya mahali pale. Watu waliomwona Obambo walitamani maisha yake sana. Mzee Obambo alikuwa na wanawe wanne na wajukuu tisa. Alifanya bidii, wajukuu na wanawe hawakumpa moyo wa kuendelea kuafikia malengo yake maishani. Alikuwa mfanyibiashara wa kuuza samaki wa aina zote. Wengi walimsihi asomee taaluma ya ushaurinasaha ambao ulionekana kumtoka kila uchao alipokaa na wenzake.

Siku moja mzee Obambo aliwaita wanawe sebuleni alipoketi. Aliwasha kibatari na seredani akawaita wanawe sebuleni alikoketi "Enyi wanangu, Inaashiria kuwa kuna watu aina nyingi. Usipoepukana nao utaangamia. Wengine watakuzima kama upepo uzimao mshumaa majira ya usiku, sikilizeni wanangu, dunia ni tambara bovu. Inahitaji ukakamavu na bidii za mchwa. Ujitume, utumike. Kuanzia leo, nimewapeleka shuleni kusoma ila si kufanya porojo." Akatua.

Nasirumbi mkewe alipogutuka na kuyatilia mkazo maneno hayo, kando na wosia wa busara na hekima kwa familia yake, Obambo alitambuliwa na wanakijiji wote kwa kuleta upatanisho wa amani. Miaka yoyoma, miaka pindukia, mtu ni utu! Saa sita kamili. Usiku wa maneno, ndipo Mzee Obambo alipogundua kuwa Mondo, lile joka lake halikuwa limepewa chajio. Kwani alihofia wajukuu wake kusikia siri yake. Siri ambayo aliishikilia kwa miaka na mikaka. Ilimletea faida.  Joka hilo liliwawezesha kuishi kwa usalama pale maskani pao kwani lililazwa karibu na mlango kila walipotaka kulala.

Baada ya kushinda bila kulishwa siku nzima, joka lile liligaragara pale lilipolazwa kando ya chungu kimoja cha maji. Suala la kushangaza ni kuwa yalikuwapo malazi yaliyosharifiwa vyema kwa kulifurahisha lile joka. Kila mmoja alipolala, alilala bila wasiwasi kwani alijua kuwa "*askari*" yu mlangoni. Usiku huo walipolala, waliamka alfajiri kumlisha "*askari*" wao. "Yuko wapi askari wangu?" Obambo alijiuliza. "Huenda amenyerereka hadi jikoni kujitafutia mlo." Alimtafuta "askari" wake kila pembe ya nyumba. Si upenuni, si ushorobani. Aliamua kumwita mwanawe Kibuye aliyekuwa usingizini ili aje amsaidie kumtafuta. "Nasirumbi! Nasirumbi! Uko wapi? Askari" wangu ameuawa". Japo hakujua aliyemuua. Ukemi wa Mzee Obambo uliuchochea

umati wa watu kuingia na kutoka kwa zamu. Ilimlazimu mzee Obambo kutafuta hifadhi kwa jirani, angaa ajipumzishe mzigo aliotwishwa. Mzigo wa mawazo kuhusu kifo cha Mondo.

Kibuye, kifunguamimba wa mzee Obambo alirejea kutoka shuleni na wenzake jioni hiyo. Walishtuka ghaya walipokutana na ramram ya wanakijiji wakingia na kutoka nyumbani kwa mzee Obambo. Yeye na wajukuu wa Obambo hawakufahamu kilichojiri kwani waliondoka bukrata kichea kwenda shuleni. "Mlipoondoka asubuhi, mlituacha tukimtafuta ‘askari’ wetu. Joka ambalo limetulinda kutokana na maadui zetu.” Aliendelea, “Jana hatukuwajibika kumpa chakula cha kutosha.”

Mzee alinyanyua daftari la shajara lililokuwa mvunguni. Akatoa nambari za simu za maafisa wa huduma ya wanyamapori, baada ya saa moja hivi walifika. Walimbeba Mondo. kwenye gari lao kachara la kubebea nyamachinje na nyamafu. Walimlazimu Obambo kuandikisha taarifa kwenye ofisi zao aseme kwa nini alifuga wanyama hatari nyumbani bila idhini.

Mzee Obambo alikuwa akifanya biashara ya kupunga pepo. Alikuwa mganga. Wakazi wa Kajificheni waliosikia sifa zake, walikimbilia kwake ili wapate suluhu ya shida zao. Majadi kubeli walifika kujionea waliyoambiwa na wale waliowahi kufika pale kwa mzee Obambo. Sifa za mzee huyo zilienea kama maradhi msimuni. Wengi walifika kwa minajili ya kushauriwa. Boma la mzee Obambo lilijaa watu kuanzia alfajiri hadi jioni.

Mzee Obambo alinunua mashamba aliyopanda karoti, nyanya na mitikiti ambayo ilimfaa sana. Ukulima huo ulimwezesha kupanua soko lake katika maeneo kadhaa kando na biashara yake ya kuuza samaki na omena, aliona kwamba ni vyema aekeze katika mali mengine ikiwamo kusafirisha mizigo kwa malori yake. Obambo hakupenda sifa zake zididimie. Kila siku ya Jumamosi Mzee Obambo alirauka mtoni kuteka maji baridi ya barafu. Maji hayo yalitumiwa kuoshea vichwa vyao. Aliwahakisishia kwamba maji hayo yalikuwa na Baraka tele ambazo hazingeisha katu. Baraka za kupata watoto kwa wale wasiobarikiwa na watoto, baraka za kupata kazi na kupendwa kazini na kadhalika. Palikuwapo jivu lililojaa kwenye gunia moja la kahawia ambalo alilihifadhi ghalani mwake. Jivu hilo liliundwa kwa miti ya misonobari, mibambakofi na mimea mingine kama vile mishubiri na kifaurongo.

Aliikausha na kuichoma. Hatimaye aliwarambisha wateja wake. Siku zote hakutaka watu wajue waziwazi kilichokuwa kwenye maghala yake matatu. Mondo aliyemfuga alimlisha Omena na Samaki waliovunjika hususan wakati

waliposafirishwa kutoka soko moja hadi jingine. Wateja wengine waliosikia habari hizo waliatuka moyo sana kiasi kwamba hawakutamani kununua samaki wala omena kwa mzee Obambo. Walizungumza mengi kumhusu. Mambo ambayo yalishusha hadhi yake. Fununu na umbeya ulizidi ukweli uliomhusu mzee wa watu. “Nimedinda kununua samaki na Omena kwa mzee Obambo...nakisia kwamba omena hao hulaliwa na Mondo. Wengine wetu tunafahamu anakowatoa wale samaki. Mzee hununua kutoka kwenye bwawa la Ojwang’ ambalo limejaa kinyesi.” Waling’aka. Hakika mahasidi waliendeleza uzandiki wao dhidi yake. Wazabizabina hawakuachwa nyuma. Walikuwa mkumbo mmoja. Walifanya kila waliloweza kuhakikisha kwamba wamemuangusha.

Mzee Obambo alitiwa mbaroni japo alijaribu kujitetea ila kilio chake kikagonga mti wa msonobari. Uchunguzi ulifanywa na majasusi wa hifadhi ya Pori na baadaye ikabainika kuwa Mzee Obambo alikuwa na mashtaka ya kujibu. Mahakama ilimpiga faini ya milioni miamoja. Baadhi ya biashara yake ilipigwa mnanda. Maisha yaliyokuwa ya maziwa na siagi yakawa ya maisha ya maji. Alijaribu kujitetea ila wapi. Mali yake ikawa umande.

Alijaribu kuuza vilivyouzika ila hela hizo hazikuyosha. Ama kweli njia ya mkato ina makali hatari. Waliolala tajiri walikesha wakielekea kwenye lindi la ulitima. Miaka ikipita akiwa husununi. Aila yake ilikosa na kukoseana. Wanawe na wajukuu wake walikosa karo. Biashara yake ilikauka. Wingu jeusi tititi la ufukara lilifunika aila yake kwa muda aliokuwa jelani.

Baada ya kifungo chake cha miaka mitano kutia nanga, aliamua kufungua ukurasa mwingine. “Dunia ina nyuso mbili. Uso mmoja ukiharibiwa, ugeuzie uso mwingine,” Mzee Obambo aliyanena hayo. Ama kweli mali ya umande haifichwi juani.

**Jitathmini**

*a) Mzee Obambo alifanya biashara gani?*
*b) Familia ya Mzee Obambo ilikuwa ikiishi wapi?*
*c) Umejifunza yapi kutokana na kisa hiki cha Mali ya umande?*

## TUMAINI na Amos Khayota

Kimya kilitawala. Kimya kilichoweza kumtisha hata shetani. Ulikuwa usiku wenye giza la kaniki ulioshamiri baridi kali. Ndani ya kijumba cha msonge, lilikuwemo kundi la wasichana takribani ishirini hivi. Labda ukali wa baridi ulioshika usukani usiku huo ulichangiwa na maji ya mto uliokuwa mita chache mbele ya kijumba hicho na kuchochewa na msitu wa Majuto uliokizingira. Nani asingehofia? Hasa ikizingatiwa kuwa kilijisimamisha kitwea?

Mlango wa kijumba kile ulifungwa kwa komeo kubwa ya chuma. Karibu na mlango walilala maajuza watatu kana kwamba walichelea kuwapoteza 'wateja' wao. Miongoni mwa wasichana wale alikuwepo Tumaini. Licha ya mikoromo iliyovavagaa kote katika kijumba kile, Tumaini alikuwa macho. Alikuwa ameletwa pale jioni ile na baba yake ili ajiunge na 'wenzake', namna baba yake mzazi alivyozoea kumwita.

Tumaini hakuelezwa alichopelekwa kufanya pale. Pukachaka! Angeelezwa na nani? Tangu lini kinda kama yeye akaelezwa kilichomtarajia? Tena wa kike? Japokuwa hakuna yeyote aliyempasulia mbarika kuhusu yaliyomsubiri, Tumaini alikisia kuwa hakuwa na lake. Maji yalikuwa yamemzidia unga. Mawingu yalikuwa yametanda, yakawa dhahiri pale alipomwona mama yake amejiinamia kwa huzuni wakati alipoandamana na baba yake wakitoka nyumbani. Kilichosalia sasa kilikuwa mvua. Mvua ambayo asilani alikula yamini kutoipa nafasi ya kumnyea maadamu ingeyadhuru maisha yake.

Kulingana na mila ya jamii yao ya Kale, Tumaini alikuwa amehitimu umri wa kukeketwa. Kijumba alichokuwemo kilitengewa maalum kwa shughuli hiyo iliyothaminiwa na wanajamii wa Kale. Alikumbuka alivyokaribishwa na maajuza wale wenye nyuso zilizoshamiri chale huku wakiwa na mikoba iliyoundwa kwa ngozi ikining'inia shingoni ikishiba nyembe.

Pale penye mkeka walipolala Tumaini na wenzake, yeye katu hakukubali kope zisalimu amri ya usingizi. Alitia na kutoa jinsi angepata mpenyo wa kujinasua kutoka kwenye mtego uliomkodolea macho. Zilisalia saa chache kabla ya shughuli yenyewe kung'oa nanga. Ulikuwa usiku wa mashetani.

Penye nia pana njia. Tumaini aliupiga moyo konde, akaamua kutoroka liwe liwalo. Aliuvua woga wa kunguru akauvaa ujasiri wa simba jike aliyejeruhiwa. Kwa kuwa dirisha halikuwa kwenye kijumba chenyewe, ilimbidi autumie mlango kutoka. Alisimama. Alipohakikisha kuwa hakuna aliyekuwa macho,

alipiga dua akanyatia hadi mlangoni. Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe; kwa bahati mbaya, Tumaini alimganyaga ajuza mmoja kichwani. Kamsa iliyopigwa ingemwamsha hata mfu. Kila mmoja akaamka kwa mshtuko. Tumaini hakupoteza nukta. Alifungua mlango na kutokomea asikokujua.

Tumaini alijipata msituni. Usiku wa manane. Giza totoro. Baridi shadidi; Tumaini hakuwa na viatu wala sweta. Alikuwa petupetu. Blauzi iliyochanika aliyovalia isingemsitiri kutokana na baridi ile. Licha ya changamoto zote zilizomsubiri kwa hamu kuu, hakufa moyo. Alimeza mrututu akaiahidi nafsi yake kuwa kamwe asingerejea alikotoka.

Majuto. Huo ndio msitu ambao ulimtisha kila mmoja pale kijijini Kale. Iliaminika kuwa wanyama aina ainati walifanya makao humo. Si chatu si simba si chui wote walikuwepo. Tumaini alipenyeza kila alipopata nafasi ya kukanyaga bila ya uhakika wa nyayo zake. Upo wakati ambapo miba ilimdunga na kubaki miguuni ila hakujali.

Ujasiri wa Tumaini uliyeyuka kwa ghafla pale aliposikia mingurumo ukimjongea kutoka alikoelekea. Alisimama kwa hofu. Mara viguu vyake viliposhindwa kukishikilia kiwilili chake, alichutama. Nywele zilimsimama kwa wasiwasi. Mwili wote ukaloa kwa jasho ya baridi ya usiku huo. Upweke aliokuwa nao ulimwongezea unyongeunyonge mbele ya nduli yule ambaye sasa angemfanya kitoweo. Akiwa amelala kifudifudi, fikra zilimpita kwa kasi kuhusu hadithi alizozisikia kuhusu msitu huo. Akajuta kutorokea huko. Roho ikiwa mkononi.

Kwa nyota ya jaha, mnyama yule alilizunguka shina la mti uliokuwa karibu akaenda kando. Ilikuwa mara ya kwanza kwa Tumaini kumwona simbamarara. Hakika; mcha Mungu si mtovu. Simba yule alikuwa na jeraha labda aling'atwa na mwenzake. Alikuwa akiyakimbilia maisha yake. Tumaini hakuamini kuwa simba yule hakumla mzima mzima. Aliyaona mauko. Kwake likawa tukio la maisha.

Baada ya simba yule kupotelea msituni, Tumaini alijizoazoa, akasimama na kuendelea na mwendowe. Ukubwa wa miti yenye matawi na majani makubwa yaliyofunika ardhi kama blanketi jeusi ulikoleza giza zaidi. Kila alipopiga hatua, alikumbuka ahadi aliyojiwekea ya kuendelea na masomo yake ili afuzu.

Muda haukupita mrefu, giza likaanza kuaga na kutoweka polepole. Miti sasa ikaanza kuonekana na kukawa salama kwa kiasi fulani. Tumaini akaona fahari japo alikuwa mchovu na mwingi wa maumivu. Akatembea kwa kuchechemea hadi alipoziona nyumba baada ya msitu ule. Tumaini alijawa na nguvu mpya.

Akaelekea kulikokuwa na nyumba, kwa nini mbwa afe maji akiwa ameuona ufuo?

Pindi tu alipofika mwisho wa msitu ule, Tumaini aliuona mwanga maishani mwake. Kulikuwa kumekucha. Angekuwa huru tena. Aliambua nyayo pole pole na kuelekea kulikokuwa na nyumba. Huko, alikaribishwa kwa mikono miwili. Mgeni alipewa nafasi ya kupumzika kutokana na uchovu aliokuwa nao. Huku akipumzika, aliifikiria familia yake; marafiki zake na jamii yake kwa pamoja.

Siku iliyofuata, Tumaini aliletewa mgeni aliyesemekana kuwa aliishi mjini na kuwa angependa kumwona. Mwanamke yule ambaye ndiye aliyekuwa mgeni alionekana mcheshi, aliyeithibiti hali yake ya afya na mwenye nafasi katika jamii. Hayo yaliwekwa bayana kutokana na aina ya gari alilolitumia kufika pale. Lilikuwa shangingi jeupe lenye utulivu wa kipekee. Mgeni yule wa Tumaini aliyejitambulisha kama Mwanga alijua kuwasiliana bila kubagua yeyote kutokana na tofauti ya tabaka. Tumaini alishangaa ni vipi walielewana haraka hivyo hata wakawa na usuhuba?

Baada ya kufahamishana na kujitambulisha, Mwanga aliwashukuru wenyeji kwa ukarimu waliomwonyesha Tumaini. Pia, aliwahakikishia kuwa Tumaini angekuwa katika mikono salama. Wenyeji na wageni waliagana huku Mwanga na Tumaini wakielekea mjini, huko ndiko kulikokuwa makao makuu ya shirika la haki za watoto wa jinsia ya kike hasa.

Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni; kila kitu kilimwajabisha Tumaini, tangu apande shangingini hadi alipowasili katika lango kuu la shirika lile. Langoni, maandishi makubwa yaliwakaribisha: 'KARIBU MWANGANI'. Ua mrefu ulizungushiwa majumba ya ghorofa yaliyopambwa yakapambika. Mawaridi yalipandwa kando ya majumba yakamvutia kila aliyeelekea upande ule. Baada ya kutua alikaribishwa na wenyeji wa aina yake. Alimsimulia Mwanga mlima wake wa maisha kutoka ulando hadi ukoko. Mwanga alimhakikishia kuwa angemuauni ili aafiki ruwaza yake. Tumaini alijiunga na majengo ya elimu. Alitiririsha aya za elimu yake hadi chuoni.

Siku ya Ijumaa ilimjia Tumaini. Baada ya kuhitimu elimu yake ya shule ya msingi, aliweza kupata ufadhili kutoka kwa shirika moja lililotoka Ughaibuni. Alijikaza kisabuni. Msemo wa atafutaye hachoki ulimnasa. Hakutaka kumpaka tope mwokozi wake Mwanga. Wafadhali walipendezwa kwa juhudi zake. Aliweza kuhitimu masomo ya upili na kisha akajiunga na chuo kikuu ughaibuni alikosomea taaluma yake ya uwakili, taaluma aliyoienzi tangu utotoni.

Siku moja kijijini Kale, hali haikuwa hali. wakazi walikuwa wamezamia katika istighali zao za kila siku. Ilikuwa siku ya sherehe ya Wanakale. Kama ibada, wakazi walijitokeza ili kusherehekea utamaduni wao na hata kushuhudia tafrija hiyo. Wasichana wengi walikusanywa chumbani ili kufanikisha siku hiyo. Ulikuwa muda wa mafunguliang'ombe. Gari jeusi lilitua katika ukanda huo wa mzee Mila. Mjumbe wa Kale. Waliokuwa na macho walishangaa kwani ndiyo iliyokuwa mara ya kwanza kushuhudia mmemeto wa gari sampuli hiyo. Sherehe zilisimama. Macho yalipata mlo. Tumaini alishuka akiwa Tumaini wa leo. Nywele za singa zilimchukua. Baada ya kipindi cha 'ni yeye ama siye' kutamatika, alipasua mbarika kwa masimulizi yaliyowaacha wengi kwa michirizi ya machozi. Elimu iliwanasa. Mjumbe akaelimika na kuwa mjumbe wa elimu. Mwanga aliamua kuwapa elimu ya bure. Kijiji kilivalishwa sare za elimu ya kike.

| ***Jitathmini*** |
|---|
| a) *Nani aliyempeleka Tumaini kukeketwa?* |
| b) *Sababu kuu ya Tumaini kutoroka kutoka katika kijumba ilikuwa nini?* |
| c) *Eleza namna haki ya mtoto wa kike imekiukwa.* |

## BONDE LA MASIKITIKO na Mwalimu Sammy

Sauti ya Sonona ilimzindua Taabu. Bila kujali kilichokuwa mekoni alichomoka kama risasi kuelekea chini ya mwembe alipokuwa akipungia unyunyu. Aliwasili akiwa amevaa malapa moja. Mkononi alikuwa amebeba kijiko. Alimpata Sonona akigaragara sakafuni kama kuku aliyedenguliwa. Tangu Siri aliposhukiwa kuwa na ukongo wa kiharusi, uhawinde uliwatembelea na kufanya makazi ya kudumu. Walikuwa wamejaribu kila aina ya mitishamba. Jitihada zao ziliambulia patupu. Hali ilipozidi kudorora zaidi aliwaalika makasisi wa kanisa lake la "*Mbinguni International"*

Hawakuchelewa. "Tunamwamini Mungu. Uponyaji nakutabiria. Roho aliniambia kuwa asipelekwe hospitalini. Tukamwombee Maulana. Tuombe, Mungu mjalie afya mja wako anayeumia. Wewe ni Mungu awezaye yote. Uhimidiwe na kusujudiwa daima dawamu. *Pepepep! arararara! Entererre! Bonzaya! ripapap! Shekeleretetebobobo!* Katika jina la Yesu Kristo! Amina, kila mmoja aliitikia ombi licha ya kutoelewa baadhi ya misamiati ya kasisi.

Taabu alikuwa mkereketwa wa dini. Jitihada za Sonona na Choka kumrai Taabu kumpeleka Siri zahanatini zilikuwa sawa na kujenga ghorofa ya karatasi baharini. Hazikuzaa matunda. Zilizaa uhasama baina yao. Tasa aliwaona kama wakaidi wasiomcha Alah. Aliisubiri kwa hamu na ghamu watakapovunjika guu kwa kukosa kusikia la mkuu. Afya ya Siri iliwavuta pamoja kama sumaku. Kwa sasa wote waliungana kumwombea Siri aishi hata kwa dakika. Walimshukuru Muumba wao kwa kila sekunde ambayo Siri aliongeza.

Punde, Choka akawasili akiwa na matawi kwapani. Kawaida yake kila aingiapo nyumbani yeye huelekea jikoni kunywa uji chapwa. Neno sukari lilikuwa geni kwao tangu janga la kiharusi libishe kwao. Aliyatupa macho yake kwenye kizaazaa kilichokuwa chini ya mwembe uliokauka kaukau miaka iliyopita. Hakusadiki alichokiona. "Tumpeleke hospitalini," "Hospitalini?" Taabu alimdakiza. "Roho wa bwana alisema kuwa tusiende hospitalini." Taabu alisema. "Ni lazima tumpeleke! Iwapo hakuna nauli nitambeba. Zamani angekataa. Leo Hana budi kutii." "Choka ni lini utakapokoma kufanya mzaha kwenye masuala adhimu?" Taabu alimsaili. "Ni lini ukabeba hata karatasi? Kila siku huwa umenyongonyea kama mnyonge aliyenyongwa." "Vitanzandimi vyako vitaambulia patupu kumpa baba afua. Baba atatibiwa liwalo na liwe." Choka alisistiza. "Mkaidi hafaidi," Mama tusipoziba ufa tutaujenga ukuta.

“Mwacha mila ni mtumwa nionacho kwenye kigoda hukioni hata ukikwea mkalatusi.”

Siri aliyakodoa maozi akasema, “Mke wangu ninakupenda ja mboni ya jicho langu. Sonona wewe ni roho yangu. Nayo pumzi ya uhai wangu, Choka. Ninawathamini. Sitaki mteseke duniani nilivyoteseka. Niliwawekea akiba ili nitakapoitwa na Muumba mtumie kujiinua kiuchumi. Kweli akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni. Choka ulete mkebe umo mvunguni mwa kitanda change” Choka alirejea na mkebe uliojawa kutu. “Libomoe.” Choka aling’ang’ana kukutu kuubomoa mkebe ule lakini wapi! Taabu aliuchukua na kuuvunja kwa kifaa kilekile alichokitumia Choka.

Mkebe ulipofunguka, *manoti* yalizagaa. Kila mmoja aliyahesabu mabunda aliyokusanya na wakajumlisha. Hakuna aliyefaulu kujua idadi kamili isipokuwa Siri aliyekuwa akiyakagua manoti hayo kila mara. “Pesa hizi zinaweza kuwageuza kuwa wendawazimu wasio na thamani.” “Pesa zipo tuende hospitalini.” Choka alimdakiza baba yake. “La.” Siri alimjibu Choka. “Sikutaka pesa kupotezwa hospitalini mkabaki wakata wa sina sinani. Milima na mabonde ya maisha yasiwaingize kwenye maovu. Ko ko ko ko ko ko ho ho ho,,, Kikohozi hicho ndicho kilichokua usemi wa mwisho wa sri duniani.

Hafla ya mazishi ilipambwa ikakubali mapambo. Mahema ghali yalilipamba boma la Siri. Maelfu ya waombolezaji walikuwepo. Waliokuja kuomboleza waliomboleza, waliokujia chamcha waliridhika. Mzee Siri alijulikana. Hulka yake ya subira iliwavutia wengi. Mamilioni ya fedha yalitumika kwenye mazishi yake licha ya kuwa maskini hohehahe. Chanzo cha pesa hizo kilikuwa kitendawili kwa waombolezaji. Aila hii iliyazika masaibu yao katika kaburi la sahau na kuzamia asali waliyoitamani miaka nenda miaka rudi. Sonona aliyavaa mavazi yaliyoziacha sehemu za mwili wake wazi. Leo paja, kesho mabega, keshokutwa kifua, mtondo mgongo na mtondogoo magoti. Wengi walijiuliza sehemu ambayo ingekuwa wazi baada ya mtondogoo. Nguo hizi zikawa sinema ya bure kwa wanakijiji waliozidi kujifunza mitindo.

“Hodi?” Mwanamume mrefu kama twiga aliubisha mlango. “Karibu,” Taabu alijibu kwa sauti yake ya kumtoa nyoka pangoni. “Mimi ni bwana Kombo rafikiye Siri. Mapenzi yetu yalianza zama zile. Yalikolea kila mmoja alipopata jiko. Huzuni tele isingeniruhusu kuwaona siku ya mazishi. Marehemu aliniahidi kuyakidhi mahitaji ya aila yangu ningetangulia. Amenitangulia! Naomba kuwafaa kwa hali na mali. Naomba kumwajiri binti yako, kwenye kampuni yangu mjini. Baadaye nitamshughulikia kaka yake na hata wewe.”

Nyuso za watu zilijaa tabasamu za kuyeyusha barafu. Sonona alijikwatua kwatu kwatu akawa mrembo kama mbega. “Samahani dada, yabadili mavazi hayo. Hayaonyeshi heshima. Heshima si utumwa.” “Vazi langu chaguo langu,” Taabu alimfokea Choka. Mgeni alitingisha kichwa chake, ishara ya kuridhishwa na kauli ya Taabu. Punde si punde mgeni na Sonona wakang’oa nanga.

Alilipwa mshahara mkubwa ilhali hakuwahi kutokwa na jasho hata chembe. “Nakupenda Sonona,” ulikuwa usemi wa kawaida mle jumbani. Jibu likawa, “Nakupenda pia Mzito.” Kauli hizi zingetamkwa mara elfu kwa siku. “Ninaenda kukagua miradi mipya na huenda nikachelewa. Furahia chochote hata kitanda changu. Nitarejea kesho.” Mzito aliondoka kwa shangingi lake. Sonona alifuata maagizo asije akajimwagia unga uliomlisha na aila yake. Baada ya kula shibe alizama kwenye usingizi wa pono chumbani mwa Mzito. Ko! Ko! Mbisho kwenye mlango ulisikika usiku wa mashetani. Sonona hakutarajia mgeni akahofia giza totoro.

Alipigwa na butwaa alipomfungulia Mzito aliyempa mkono wa tahania kwa ulinzi. Furaha ilimyeyushia magumegume ya usingizi. “Naomba nikuandalie kilalio?” “Asante mpenzi wangu nina cha kutia tumboni. Pengine nikugawie.” Sonona alilibofyabofya tumbo lake kutafuta nafasi zaidi. Hakukataa chakula kile licha ya kuwa alishiba ndi kama chatu aliyemeza kondoo mnono tamthili ya nguruwe. Alitamani kuonja “vya juu” - alivyoviita vyovyote alivyokuwa navyo Mzito. Mzito aliandaa vinywaji maridhawa. Walikula kiasi na kunywa kwingi kisha wakaongozana kupata lepe lililosalia. “Ninaenda chumbani mwangu,” “Hakuna haja ya kuandaa malazi yako twende kwangu.” Alimjibu Sonona. Sonona alitabasamu kisha wakaenda moja kwa moja.

Walijirusha kitandani ungedhani ni magunia mawili ya viazi. “Samahani sina budi kukupiga kalamu. Ungekuwa mke wangu ungesalia humu. Kata kauli uwe wangu mke ama urudi kwenu.” Namna alivyozidi kukataa ombi la Mzito ndivyo ulevi ulivyomwandama. “Sawa Mzito ninakupenda sana.” Sonona alimjibu. Alikuwa amepiga maji. Kulipokucha Sonona alionyesha uchovu. Alianza kutapika. Hakuujua ugonjwa uliomwathiri usiku. Mzito alipompata akizidi kuyatema aliyoyala alishtuka. “*Nimemess*,” alijisemea. Alipiga hatua tatu mbele, nyuma, mbili kulia, kushoto, aligeuka kusini, kisha magharibi, mashariki hatimaye akarejea kaskazini. Siku ziliunda majuma kwa upesi. Nayo majuma yakaiunda miezi. Ikawa meno ya ngiri kuwa usiku ule aliporudi kwake bwana Mzito ndipo alipoupata ujauzito wake wa kwanza Sonona.

“Hiki kitu kitaniaibisha". Akamwita Sonona. “Nenda nyumbani ukampelekee mama hizi. Asijue kuwa nilisababisha mimba hiyo. Mwambie ni kijana wa mtaa. Baada ya siku mbili nitakuja kukuchukua. Utaenda kusimamia miradi niliyoenda kukagua. Barua hii umpe. Ni shukrani zangu kwake na kwako. Nitakupa dereva atakayekupeleka. Sonona unahitaji huduma bora.” “Asante, kwaheri.” “Ya kuonana. Be carefull,” Mzito alimjibu. Walifika kwa mzee Siri. “Maisha ya asali na maziwa. Umerudi ukiwa na kitambi kuzidi cha rais wetu mtukufu Fisadi.” “Una uhakika ni kitambi?” Choka alimwuliza Taabu. Taabu alizipokea zawadi kwa mikono miwili na moyo mkunjufu. Alikabidhiwa waraka wake naye akaanza kuusoma kwa makini.

Bwana Mzito,
S.L.P 234578,
Dhulma.

5 - 8- 2020

Kwa mama Sonona,

Pokea salamu. Nina matumaini u salama huko Kijiweni. Huku Nina imani kuwa Sonona amefika na kuwasili nyumbani salama salmini. Kusudi la baruai ni kukuomba umkanye Sonona. Mimi Mzito bin Dhulumu asithubutu kulipaka jina langu tope. Baada ya kuwa na jicho la nje akawa jamvi la wageni ananisingizia. Kila ninapotoka yeye pia hutoka. Akawa panya kutawala aondokapo paka. Nimejaribu kumvumilia lakini habadiliki. Nimefikia uamuzi wa kumfikisha kwao kwa kuwa anaweza akawa na ujauzito wa pili hata kabla ya kujifungia. Naomba ujaribu. Huenda akakutii zaidi. Kunao watu ambao huwatii wazazi wao zaidi ya mtu yeyote. Kwaheri mama Sonona. Kila la heri katika pilkapika zenu za maisha.

Ni mimi wako,
Bwana Mzito.

Barua ilianguka ghafla. Akamtazama binti yake. Machozi yakamwosha ungedhani alinyeshewa. Sonona aliichukua na kuisoma. Machozi yalimbubujika. Choka alibaki kinywa wazi. “Uongo! Ni yeye!” Sonona alilia. “Sitakubali,” Taabu alisema kisha akaingia chumbani. Aliondoka mle minghairi ya kusema na yeyote. Baada ya saa nne wanakijiji walikusanyika kwa Siri. Tasa alilielezea baraza hilo kinaga ubaga madhila aliyotendewa. Sonona aliyathibitisha. Chifu aliahidi kuchukua hatua. Baada ya upelelezi, ilikuwa wazi

kuwa Mzito alikuwa mshukiwa mkuu. Aliombwa kujiwasilisha mahakamani. Watu walifurika mahakamani kusikia namna dhulma zake zingefikia kikomo, kama alivyoahidi jaji Tamaa. Kizimbani, Sonona alisimama tisti. Naye wakili wa bwana Mzito alikuwa ange kumtetea mteja wake. Mshtaki alithibitisha madai yake. Aliyasema kuanzia shina hadi kileleni. Zamu ya bwana Mzito ilipowadia, wakili wake alimfanyia haki. "Kwa kukosa Ushahidi tosha uchunguzi zaidi ufanywe. Matabibu wahusishwe. Kesi hii itasikilizwa tena tarehe tano mwezi ujao."

Kwa Tamaa, wanapiga gumzo na Mzito. "*Deal sealed*." Bwana Mzito aliondoka. Tamaa alimsindikiza. Aliondoka kwa mwondoko wa njiwa akiwa na furaha riboribo. Iliyosubiriwa ilipofika hapakuwa na mengi. Jaji Tamaa alishika usukani na kuamua kesi. "Kwa kukosa ushahidi wa kutosha mahakama imeamua kuwa kamati ya wanakijiji iundwe. Isikilize na kuamua malumbano haya. Mahakama hii inaomba kujuzwa matokeo ya hayo baada ya mwezi mmoja." Aila ya Siri iliondoka ikigubikwa gubigubi na mawingu ya majonzi.

Usiku huo bwana Mzito alimtuma dereva wake kuichukua familia ya Siri hadi kwake. Walipofika, walikaribishwa kwa mapochopocho ya kila nui. "Familia ya Siri singetaka niwakosee. Ninawaahidi, nitagharamia mahitaji yote ya mtoto wangu. Si mavazi si maakuli si karo. Nitawapa mkono wangu wa tahania. Baada ya mtoto wangu kukua nitalipa karo ya Sonona ya shule ya upili ili atimize ndoto yake ya kuwa hakimu. Kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi." "Nina furaha tele kuwa umeamua kutufaa wakati huu wa balaa." Taabu alikuli. Dereva wa bwana Mzito aliwaendesha hadi nyumbani kwao. Choka hakuonyesha dalili za kuridhika.

Kila mwezi alimtumia Sonona vitu kadha wa kadha ili kugharamia mahitaji yao. "Ninaomba kumwona Sonona." Dereva alimwambia Taabu. "Sonona dereva anakuita." "*Hello*? Naomba tuandamane hadi garini." Dereva na Sonona waliandamana polepole hadi garini. "Sonona nimekuletea zawadi kutoka kwa bwana Mzito. Ameomba utie saini yako kwenye karatasi hii ili kuthibitisha kuwa nimekuwa nikikushughulikia. Sahihi moja itie hapa, na nyingine hapa. Barabara kabisa kwaheri." Dereva alimwaga Sonona na kuondoka. Taabu alikata kauli kurudi mahakamani baada ya ukame wa misaada. Tamaa alimwonyesha barua mbili. Ya kwanza aliiandika Sonona na kutia sahihi kuwa Mzito hakuhusika katika mimba yake. Taabu alishangaa. Alimrai jaji kumwonea binti yake mbawazi. Jibu la Tamaa likawa msumari moto juu ya kidonda. "Visa vya mabanati kupata ujauzito kisha kusingizia matajiri

vimekithiri mno. Baada ya kushiriki mapenzi na waja wasioweza hata kuwanunulia sodo, wao hukimbilia wenye nafasi katika jamii."

Alfajiri mbichi Sonona alikuwa akiendelea na usafi wa nepi. "Sonona!" Taabu alimwita huku akiangalia mavazi yaliyoanikwa. "Iliyoanikwa hapa ni kanga yangu?" "Sina chochote. Mavazi maridadi niliyokuwa nayo niliyauza kugharamia mahitaji ya mwanangu. Mjukuu wako," "Mjukuu wangu! Then?" "Nilikosa hata kipande cha nguo cha kumpangusa. Niliichukua kanga hii iliyochanika. Nikaigawa sehemu nne niitumie kama nepi. Niliitumia kanga yako kama ubinda mama," "Iwe siku ya mwisho kutumia chochote changu kwa huyo mwanaharamu unayemwita mjukuu wangu. Nitawalea watoto hadi lini. Mwisho wangu kulea nilidhani ulikuwa miaka kumi na mitano iliyopita nilipokuzaa. Mama asiye na kwake. Tafuta kwako mama mwenzangu. Bwana Siri alimwoa mmoja. Toka!"

Hayo yalimkata Sonona maini. Akajipata kwenye bonde la masikitiko. Alitamani alie akajutia matendo yake. Alisimama kidete ungedhani kapigiliwa msumari. Alitazama nyuma akamwona mtoto wake akihemahema kwa uchungu, njaa na uchovu. Alikata kauli. Alifuata kijia kilichoelekea mto uliofurika furifuri. "Laiti ningekutana na mvulana yeyote asiye na mke anioe. Nimwue huyu mtoto?" Alijisemea njiani. "Sitaki mteseka duniani kama nilivyoteseka. Milima na mabonde ya maisha yasiwaingize kwenye maovu." Aliyakumbuka maneno ya marehemu baba yake akiwa njiani. Punde akafikia mto. Akatazama mbele, nyuma na kando asimwone mtu. Akamtazama mtoto wake. Akasimama wima kwenye ubigoubigo wa mto. Alichowazia alikijua mwenyewe.

| **Jitathmini** |
|---|
| a) *"Nikaigawa sehemu nne niitumie kama nepi. Niliitumia kanga yako kama ubinda mama," tia dondoo hii katika muktadha wake.* |
| b) *Jamii imetawaliwa na maovu ya aina nyingi. Kwa kurejelea Bonde la Masikitiko, taja baadhi ya maovu ambayo wanajamii wanapitia.* |
| c) *Taja na ufafanue maudhui yoyote matattu yanayojitokeza katika hadithi, Bonde la Masikitiko.* |

# MTINDI WAMPONDA na Moses Odongo

Katika karne za mababu na mabibi zetu yaani fuzi na dahari zilizotupa kisogo aliondokea ghulamu mmoja aliyeitwa Kalewa. Kalewa alikopolewa katika kitongoji cha Nelaa, kaya iliyojulikana kotekote kama faranga kwa maswala ya ugimbi na upigaji tarumbeta.

Toto la waja lilizaliwa na wavyele waliokuwa wameibugia munyu si haba. Waliishi maisha ya ufukara licha ya kuwa aila yao ilikuwa maskini waso na lolote wala chochote. Wavyele wa shababi walijaribu kwa udi na uvumba kumpeleka kwenye shule ya msingi ya Nelaa katika darasa la kukomoa. Hakuona umuhimu wa masomo, aliamua kuingilia starehe, maskini wa Mola aliamua kuwa bendera kufuata upepo.

Naam, hakuchelea kurauka kuwatembelea wagema wa kijiji cha Nelaa kwa majina Babapima na Mamanitilie. Wagema hawa walikuwa wakirauka bukrata kuandaa tembo na kuwaalika wengi kwenye dhifa kama ilivyokuwa ada na kaida yao. Siku ayami kijana Kalewa alipopiga hodi kwenye boma la wagema hao mwendo wa saa kumi na mbili alfajiri, alikaribishwa kwa bilauri ya pombe haramu iliyokuwa imejulikana na wengi kijijini humo kama "*Chang'aa.*" Aisee kwa lugha ya mtaa walevi huita "*Oluya Olwe Inyungu*"

Alfajiri hiyo kinda hili halikuwa limetia kitu tumboni. Lilikumbatia gilasi kwa tabasamu isiyo na kifani pasi kubaini ya wahenga kuwa kutangulia kwenye baa si kulewa. Kalewa alipiga funda la maji machungu, waswahili husema alipiga tarumbeta akainamisha kichwa huku akisema kwa lugha ya mtaa '*kano ni malulu.*' Aliitisha ya shilingi ishirini, akasisitiza alikuwa na ishirini tu. Mamanitilie alijaza. Ilikuwa ni dhifa kwa maskini wa Mungu Kalewa kuzidi ile ya nzi kwenye karamu ya minofu na mizoga! Alisalimu amri na kuapa kuwa nzi kufia kwenye kidonda si hasara. Jamaa huyu alibugia mkojo wa firauni akawa haoni lolote wala chochote.

Asubuhi hiyo Kalewa hakubaini kuwa alikuwa na mtu nyumbani. Alimtonesha kidonda bibi yake Bi. Masumbuko na wanawe wawili. Alipozidi kuwa mraibu, alikuja kuishiwa na ngwenje. Alianza kumwibia mkewe bidhaa na hata vyombo vya jikoni pasi kusahau vijiko. Alivipeleka kwa Mamapima. Alipoonywa na wavyele wake, lulu za kumkanya hazikuzaa matunda. Alijifanya kiziwi asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini.

Kijana huyo wasemavyo wazee hatimaye '*alibomoa*' nyumba yake. Bibi yake aliamua kumpa talaka pamwe na watoto wake. Wote walitokomea mjini. Wazazi walijaribu kumshika sikio lakini wapi. Aliweza kukata kauli ya kutobanduka kwa mgema. Kalewa alijulikana kitongojini kama fulusi. Alianza kuwaibia wazazi wake.

Alivyozidi kufanya hivyo, ndivyo ulevi ulivyozidi kumkolea maishani mwake. Akasahau kuwa sana ikizidi sana huwa ni makosa sana. Pombe ilimfanya kuwa maskini wa sina sinani, fukara fuke asiye na chochote wala lolote. Hata nguo zake za mwilini zilikuwa zikiicheka hali yake.

Umaskini ulibisha hodi kiamboni. Aliishi maisha ya nyuni. Alilalia maponeo akaona ni bora aonje pombe kujiliwaza na kujisahaulisha na hali halisi iliyomkumba. Mavazi yake yalikuwa yamekwajuka kwajukwaju, alivalia vitema na mademu yaliyokuwa yameraruka raruraru. Haya hayakumhusu ndewe wala sikio. Utu ulimtoka kabisa. Akabaki kutembea nusu uchi.

Kalewa alikaribisha shida nazo zikabisha hodi. Zilitawala na kukita mizizi kwelikweli. Kijana huyo alionekena kakonda na kukondeana kimbaumbau mwiko wa pilau kando. Akabaki ng'onda. Wazazi wake walianza kuwasingizia wanakijiji kwa kumfanyia mwanao usihiri lakini kilio si dawa aidha yakija yapokee. Waliamua kuwakimbilia waitwao '*walokole*' kwa maombi. Dua yao haikufika kwa Mungu. Ikawa sawasawa na ya kuku iliyokosa shabaha kwa mwewe. Kijana wao alizidi kuharibika akawa hawezi kufanya lolote nyumbani huku kadai chakula kila kuchao. Nyumba yake ya msonge ilikuwa ikivuja maji. Ndani mlikuwa sawa na nje.

Afya na siha vilimhepa akawa wa kuuza kila kitu hata kisakata cha shamba alichopewa na mvyele wake. Kule kwenye kilabu alikutana na virukanjia akawa wa nipe nikupe. Toto la watu liliabiri mtumbwi wa kiza. Wazazi wake kwa huruma walimpeleka hospitalini na ikabainika wazi kuwa pombe ilikuwa imemsababishia saratani ya ini akawa hawezi kutibiwa Wavyele wake walilia lakini kilio hakikuwa dawa.

Wote walijawa na hasira za mkizi pamoja na uchungu wa mwanao. Walikumbuka walivyojaribu kumuonya mwanao na kumtia nasaha huku wakipiga darubini jinsi uchochole ulivyokuwa umewakodolea maninga. Tayari wavyele wake waliamua kubaini usanii wa wahenga kuwa maji yakimwagika maji hayazoleki, tayari yalikuwa yamemwagika. Samaki hakukunjika kamwe akiwa mbichi.

Wanakaya wa Nelaa na wajumbe wa nyumba kumi waliweza kukongamana pamoja na maafisa wengine wa serikali ya jimbo la Busia kujadili kimaso juu ya suala hili. Nao ni naibu wa chifu wa kata ndogo ya Sikoma Bw. Patrick Opata, Chifu wa Marachi ya kati, pasi kumsahau mwakilishi wadi Bw. Obuya na Mheshimiwa Oyula Mbunge wa Butula "Ndugu zangu amkeni mpigane vita dhidi ya suala hili ili mkaokoe kizazi cha siku za halafu." Wote kwa kauli moja waliamua kulijadili na kuweka bayana athari zake.

Mikakati kabambe iliwekwa kukabili watakaokwepa mkono wa sheria. Vituo vyote vya mtindi vilipigwa mnanda kijijini vikiwemo: Klabu ya Boyz na Kamnyweso. Vijana walionywa dhidi ya kubugia pombe haramu. Athari zake ziliwekwa bayana mathalani: kupatwa na gonjwa la saratani ya ini, ugonjwa wa moyo, kuua kizazi cha wanaume na kuvunjika kwa ndoa. Pombe hufyonza vyakula na kuleta ugonjwa wa kongosho. Ugonjwa wa ini. Hudhuru ubongo wa kijana aliyebaleghe. Madhara mengine yasiyo ya kiafya ni kuwa: ukosefu wa ajira, umaskini, kutotangamana na wengine hasa wa aila yako bila kusahau kifo. Mafunzo yaliwekwa paruwanja.

"Wananchi wenzangu tukome kutumia pombe haramu kama tulivyokoma titi la wavyele wetu. Chambilecho wahenga mchezea tope haliachi kumrukia. Kwa sasa vijana wengi wamepokea mafunzo juu ya suala hili. Wanakijiji wa Nelaa amkeni, pombe na ulevi havitatufaidi kamwe. Tukimbilieni maabadini na walioko karibu na Mungu tuombeni na kukesha dhidi ya nduli na zimwi hili. Enyi mnaopika tembo mjirudi, kumbukeni kuwa damu ya wale wanaolia wakilala njaa huku mkiwahadaa wateja wenu, inatonesha sana.

Mjibadilishe na kufanya uamuzi bora wa biashara mbadala. Ewe mlevi piga hesabu ya hela ambazo umezitumia tangu mwaka uanze hadi sasa na ufanye uamuzi busara wa kupiga teke suala la ulevi kwa kufanya hivi utaimarisha jamii yako na kizazi chako. Hebu tuangalie upande wa masomo, shuleni wanagenzi wanapotumia pombe na mihadarati kwa ujumla wanapofanya mitihani wanaandikisha matokeo duni licha ya wazazi kulipa karo muhula baada ya mwingine. Wanafunzi watakaohusika katika matumizi ya dawa za kulevya waonyeshwe paa. Aidha, wapewa adhabu inayostahili mbali na kuonywa vikali. Kamwe tusiwe Kalewa. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu" Maneno hayo ya chifu yalimponda sana Kalewa. Kalewa alibadilika na kuasi mtindi.

**Jitathmini**

*a) Toa sababu zilizomfanya Kalewa kuwa bendera ifuatayo upepo?*
*b) Eleza mbinu zozote za lugha zilizotumika kwenye kisa hiki.*
*c) Andika insha ukielezea athari za pombe.*

# KILIMA CHENYE BUBUJIKO LA MOYO na Washington Bin Juma

Ni yakini yakinifu kuwa atangaye na jua hujua. Uhakiki na uhalisia wa nasaha hii aghalabu umeendelea kumroweza kijana barobaro almaarufu Sitamauke. Chimbuko lake la kung'ong'onwa na kutafunwa na soneneko, jitimai na shakawa isiyosemezeka wala kukadirika lingali kitendawili. Hisia hizi zinapojikunjua na kujidhihirisha kimachomacho akilini mwake, mvulana huyu amekwisha kuukwea na kuuparaga mlima au niseme mwinuko wa Sikuta kama unavyojulikana kwenye kijiji hiki cha Kamasia. Mlima uliojaa majabali makubwamakubwa; Mengine ya kutia kiwewe na mengine yenye mvuto na haiba ya ajabu.

Akiwa amejibweteka kwenye mojawapo ya majabali hayo, kwenye kilele cha mlima, macho yake yanapigana pambaja na mandhari ya aina yake. Kule chini ya mlima ni eneo pana la makazi ya watu. Ndicho kijiji cha Kamasia. Milolongo ya akina mama na vikembe wa kike, inaonekana ikielekea upande wa mto. Mto auonao japo kwa mbali. Vimulimuli vinavyosababishwa kwa miale ya jua, bila shaka vinaufanya uonekane bayana. Licha ya kipindi kirefu cha kiangazi, maliasili haya yameibukia kuwa suluhu ya kudumu kwa wanakijiji hawa. Kila mmoja amelibeba gudulia la maji kichwani ili ajipatie shughuli za nyumbani. Wanalazimika kujihimu mapema ili waambulie maji maenge. Mara nyingi baada ya saa nne, kupatikana kwa maji safi huwa vigumu.

Baada ya takriban dakika thelathini hivi, anajikokota ingawa si mgonjwa. Pengine hii imetokana na kazi za sulubu alizokuwa amezitekeleza kutwa iliyotangulia. Baada ya kitalifa kifupi hivi, alizimia kuketi baina ya majabali mawili ingawa kwa tahadhari kubwa. Si ajabu kuwa mazingira ya sampuli hii huwa makazi aali kwa wanyama hatari kama vile majoka. Akiwa ametulia tuli kama maji ya mtungi, anajikuta akipumbazwa na upepo mwanana. Mbali na hii, anajihisi salama katika hewa hiyo. Ghafla kama ajali, anaitundulia anga iliyomtazama kwa kipindi kirefu kama kwamba ilikuwa imemwalika pale. Kwa kawaida ni nadra kuwepo kwa wingu katika eneo hilo la Lodwar hasa miezi hii. Iwapo maghubari yangeonekana basi yangetoweka mara moja. Siku hiyo ilikuwa tofauti sana madhali mawingu mepesimepesi yalitanda kila pembe za eneo hili. Mengine yalionekana yakienda kwa kasi kana kwamba yalikuwa yakibishania zawadi.

Maswali bila majibu yalimpiga kumbo Sitamauke asipate wa kumsaidia kuyakabili. Sekunde zilivyozidi kuunda dakika, ndivyo mavunde yalivyoendelea kuenea kotekote. Hali hii ilimzidishia hamu ya kukifumbua kiini cha wingu hili. Mandhari yenyewe yalianza kubadilika. Anga ikageuzwa na kuwa kurasa za picha na taswira. Sitamauke aliingiwa tena na taharuki. Mwanzo wa ngoma ni lele. Ghulamu huyu asingebaini dhahiri kuwa ndio mkoko ulikuwa umeanza kualika maua. Mara tena, ingawa kwa wazi mno, mawingu yalianza kuumba na kudhihirisha kadhia ya viumbe mfano wa wanadamu. Sitamauke alibaini kuwa hawa hawakuwa watu wa kawaida.

Upande wa kaskazini, kitalifa kifupi hivi kutoka palipo viumbe hawa, anakaribishwa na michoro ya watoto waliovalia sare za shule zenye rangi za aina yake. Vigoli walivalia marinda ya samawati na blauzi za manjano nao maghulamu walijisetiri kwa kaptura nyekundu na mashati meupe pe. Kila mmoja alitundika mkoba wa vitabu kwenye mtulinga. Mwendo si ule wa kobe bali wa haraka ungedhani walikuwa wakiuponda wa fisi. Hili nalo lilimduwaza kijana huyu.

Kitushi hiki cha wanafunzi, kinamrejesha Sitamauke nyuma. Alikumbuka akiwa shule ya msingi ya Kieleweke. Vitoto hivi vikaibua na kuamsha mjadala kuhusu elimu yenye msingi wa nidhamu. Akatanabahi jinsi mwalimu wake wa somo la Kiswahili, Mwinyi Jikaze sio mara moja, akiwashauri wadogo wake kuhusu elimu bora, si bora elimu na makuzi ya kutegemewa. Alhamisi moja aliwahamasisha kuhusu jamii. Akasisitiza kuwa jamii thabiti huhitaji misingi madhubuti ya makuzi ya watoto. Akaongeza kuwa ni muhimu wanajamii kuwasomesha watoto.

Kumbukizi hii iliyojaa ukweli mchungu, ilimwingia sikioni na kujenga makao ya kudumu. Mara akamkumbuka tena Bw. Jikaze. Huyo alikuwa mwalimu mmoja kati ya maelfu. Alikuwa mfunzi, na mtambuzi mwenye lulu na tabasuri. Alikuwa mweledi na msomi aliyebobea katika ufunzaji wa Kiswahili. Kifo! Kuntu hakina huruma! "Kifo kilitupora mwalimu rafiki tuliyekuwa aliyetegemea kwa mengi. Bw. Jikaze hakufa bali aliiaga tu dunia".

Nasaha za mwalimu wake zilimrejelea tena Sitamauke akiwa angali katika hali hiyo hiyo ya taharuki, “Wadogo wangu, kumbatieni na kuiandama nidhamu ya maisha kwani mtoto ajifunzaye adabu ipasavyo aghalabu hawezi kutetereka popote; iwe ugenini au nyumbani. Enyi akina Sitamauke, mna jukumu la kuyaimarisha maisha na mustakabali wenu. Ipo haja ya kujitenga na kasumba na tamaduni potovu za kigeni. Ziigeni jamii nyoofu kinidhamu kwani

mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina yake." Huo mchoro wa nguva ulioonekana ukimwandama mwanamume aliyeonekana mlemavu wa miguu yote miwili tayari kumfanyia lolote, liwe liwalo, uliimkumbusha ghulamu huyu kadhia ambapo aliandamwa na kuviziwa na mchawi yapata miaka ishirini na sita iliyopita.

Ulikuwa usiku mchanga saa mbili hivi baada ya jua kuiaga mikoche na baada ya kupata chajio, mlo ambao ulipatikana kwa taabu. Mwezi mpevu ulionekana na kutoka upande wa mashariki na kutapanya miangaza yake kotekote. Nyingi za familia hapa hazikuwa na uwezo wa kupata chakula mara tatu kwa siku. Huu ndio mlo uliosubiriwa kwa hanjamu la marejeo ya chombo. Sihitaji kukueleza kuwa janibu hizi zimelemewa na ukata, uhitaji na urumo wa sina sinani. Maisha ya wengi hapa ni ya mradi mkono uende kinywani. Wakajaribiwa kuenda nguu, hata hivyo, wakaipiga mioyo yao konde madhila hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe. Aidha, wakasadiki kuwa Mterehemezi ana uwezo wa kufufua nyama kitangani.

Kitongoji cha akina Sitamauke ni baadhi ya vijiji ambavyo vilizongwa na usihiri uliovuka mipaka. Maisha ya wengi yalikatizwa bila huruma. Sitamauke pamoja na ndugu zake wawili mvulana, Kunguru na msichana Sistahimili, waliondoka nyumbani himahima wakielekea kwa ajuza yao Bi. Vumilia baada ya chajio. Walikipitia kichochoro hicho tangu utotoni. Walizoea kumtembelea usiku mchanga kwani aliwatambia ngano mbalimbali zenye nasaha za maishani.

Kulisikika sauti na milio tofauti za viumbe hai wakiwemo kereng'ende na sodomti. Si ajabu kuwa palikuwepo pia na zile za vinyemere na vyura walioyafurahia hayo mandhari mufti. Mchanganyiko wa hizi sauti zote ulihanikiza kote mfano wa vikorombwe na kuwakumbusha kuwa bado kuna kesho! Mbele kidogo kabla wafike kwenye kijishamba cha mihindi, migomba na mihogo, tayari vivuli vya mimea hii vilikuwa vimeifanya njia kuwa na giza la kaniki.

Malaika yaliwasimama. Parafujo za mwili zikawalegea. Kijasho kikawanyiririka mikondo mikondo kutoka visogoni, ikaunda njia kwenye uti wa mgongo, wakahisi ikidondoka kwenye eneo fulani, kule chini wasikoweza kukuelezea ila Mungu na ibilisi pekee. Mitima ikawapapa, wakagubikwa na kiwewe cha ajabu. Ghafla kama risasi, pande la jitu lilibumburuka na kutoka kwenye kichaka hatua chache kutoka kwenye kijia hicho. Hayawani huyo

alipokuwa nusura awafikie, ndipo walipomaizi kuwa alikuwa mwanga kwani alikuwa kavalia *Suti ya Mungu.*

Sitamauke akadhukuru ngano aliyotambiwa na babu yake mzee Wakazeni. Alielezwa kuwa mwanga yeyote yule huongozwa na nguvu fiche asizoweza kuzidhibiti. Uraibu huu wa kukimbia usiku humpa nafasi murua ya kuridhisha uchu wake. Bila kufanya hivi, hukosa utulivu wa mawazo. Iliaminika kuwa baadhi yao hurithi tabia hii kutoka kwa wazazi ilhali wengine ni msukumo wa binafsi tu! Kwa dakika kama tatu hivi, pakazuka patashika kati ya Sitamauke na mwanga mhuni huyo alipogundua kuwa hakuwa na mbinu nyingine mbadala ya kumkabili kijana huyu, aliamua kuikimbiza roho yake na kutokomea vichakani. Sitamauke, kijana asiyekubali kamwe kutamauka maishani alijipa mkono wa tahania.

Japo alirejea kwao akiwa hoi bin tiki na mchovu wa mwili na roho, ilikuwa afueni kwa baba yake, Bw. Kizito kwani alikuwa amekwisha zipata tetesi za kufadhaisha na kuogofya kutoka kwa wale waoga akina Sistahimili. Mzee alizongwa na mawazo mchafukoge akaachwa hoi, taabani na chordo. Alidhani kuwa yamkini mwanawe aliangamizwa au kufanyiwa kitendo chochote cha kinyama! Ingawa dua ya kuku haimpati mwewe matarajio ya wakazi wa eneo hili la Kamasia yalikuwa yakisubiri siku ifike ambapo hapangesikika kisa chochote cha usihiri, fakachi, ukabila, ufisadi, kutowajibika, ubinafsi, dhuluma au unyanyapaa, siasa duni utovu wa amani na usalama, uongozi duni wizi wa mali ya umma, vita vya kijamii hasa baada ya uchaguzi na na ukosefu wa usawa katika ugavi wa mali ya umma.

Japo kulikuwa na ripoti za ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma, kwa kiwango fulani kulikuwa na dalili na chembechembe za maendeleo. Hii ililetwa na kukopolewa kwa ugatuzi kwa misingi ya katiba mpya. Hivi sasa kuna baadhi ya baraste zilizowekwa lami, usambazaji wa stima, ukarabati wa madaraja, hospitali, shule, uboreshaji wa huduma za usalama, utalii na kilimo. Ishara tosha kuwa ilishuhudiwa na Sitamauke alipogeuka na kuyaelekeza macho yake upande wa mashariki ya Lodwar. Aliliona jengo la ghorofa ambalo kwa yakini lilikuwa refu kuliko yote. Alilakiwa na maandishi yaliyonakiliwa kwa rangi yenye mchanganyiko wa wekundu, kijani, weusi na weupe. Kwa jumla, mjengo huu ungeuona ungedhani ni ule wa *Harambee House* kwani lililandana na kushabihana barabara. Hii ilikuwa dalili tosha ya utaifa. Jina lililoonekana

waziwazi lilikuwa ni SALAMA. “Lazima limesetiri siri fiche” Sitamauke akajisemea.

Historia ya mji huu kwa mintaarafu ya walioujua kutoka mwanzo ni kuwa kabla ya jengo hili la SALAMA, haya yalikuwa maeneo ya stendi ya magari na wanabiashara wa aina yote. Hili eneo lilikuwa kivutio kikubwa kwa wengi. Biashara belele zilianzishwa hapa zilizoharamishwa na zilizohalalishwa. Vioja na visanga vingi vikapata shamba, vikapandwa, vikachipuka, vikanyunyuziwa maji, vikatiliwa rutuba hadi vikarutubika vikapaliliwa kisha vikazaa matunda ya uovu ambao hadi leo hii bado unasadikika. Akina baba na akina mama, watoto wa jinsia zote walijitosa kijongoo kwenye ulingo wa pombe haramu na matumizi ya kasumba bila kujali wala kubali. Athari zake zikawa wizi wa kimabavu, ubakaji ugaidi umaskini na ulaghai bila silaha yoyote. Ndio sababu eneo hili likaitwa Sokomoko.

Mbali na matatizo hayo, watu walijiendea haja zote peupepeupe bila kujisetiri. Si pembeni mwa barabara, si nyanjani, si kwenye mitaro iliyojaa na kutuama majitaka. Vyoo vilikosa maana na kuadimika kama mizizi ya mawe. Sitamauke aliposikia haya, alikumbuka usemi wa mwalimu wake Bw. Jikaze kuwa, “Uso haukuumbwa na soni.” Kinyaa cha kukirihisha mintarafu ya harufu ya uozo huu, kikazagaa na kuhanikiza kila mahali. Wengi wakaathirika na kuiaga dunia kutokana na mkurupuko wa ndwele hatari za waba na kichocho. Serikali ilijaribu kwa jino na ukucha kukinusuru chombo kilichotishia kuyaangamiza maisha yao lakini wapi? Tangu lini sikio la kufa likasikia dawa?

Ni papa hapa Sokomoko ndipo nilipomjua mjomba wake Sitamauke. Alikumbana na mapwagu waliomlaghai kwa njia rahisi sana yaani wizi wa akili bila silaha yoyote. Siku ya Ijumaa tarehe tatu Aprili mwaka wa 1999, mjomba wa mtu aliandaa safari ya kuelekea mji wa Nyeri. Kusudi lilikuwa kuenda kuvichukua vyeti vyake baada ya kuhitimu taaluma ya ualimu kwenye taasisi ya Kamwenja. Alikaribishwa kwenye stani hii kwa heshima na intidhamu na utingo huyu. Hii ilikuwa tofauti na kinyume na hapo awali ambapo abiria waling’ang’aniwa na mataniboi kama vile shibli waviziavyo windo la nyama. Wakati mwingine abiria alijikuta amenyakuliwa hangahanga bila kujali heshima ya kijinsia. Siku hiyo alipigwa na pumbao kutokana na makaribisho haya ya kipekee. “Huenda huu ni mwanzo mpya na kigezo cha kuigwa na utingo wengine,” Akajinong’onezea.

Aliongozwa hadi kwenye ofisi na kuandikiwa stakabadhi kisha akalipia jumla ya shilingi elfu nne na mia saba pesa taslimu. Baadaye alimwendea

mshoni wa viatu kwani viatu vyake vilistahili kushonwa na kupigwa rangi. Baada ya fundi kuvikagua, alimshauri kuwa ni bora anunue makanyagio mapya. Fundi alipokea shilingi mia nne kutoka kwa Ningejua. Ili kununua soli iliyolingana na viatu hivyo, ilimbidi aende na viatu vyenyewe. Lakwata! Kutokomea kwa fundi huyo ndiko kulikokuwa mwanzo na mwisho wa kuonana na Ningejua. Alikuwa ameporwa kwa wizi wa akili. Kuna watu na viatu, wenye kutu si utu.

Kipindi cha dakika ishirini kilimtosha kumkumbusha kuwa pwagu yule asingerejea tena. Alipojaribu kujipima viatu kuukuu na kweche aligundua kuwa vyote vilikuwa ni vya mguu mmoja mbali na kuwa visingevalika na mtu mwenye akili razini kama yeye. Akachanganyikiwa asijue la kufanya. Mbwa hafi aonapo ufuo. Alipoitazama akrabu ya saa, zikawa zimesalia dakika tano ufike wakati wa gari kuondoka. Akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni. Aliyachukua masurufu aliyokuwa amebaki nayo ya shilingi mia mbili na kununua kandambili kisha, akaserereka na kusepetuka mfano wa kuku alinyeshewa na mvua ya kifuku.

Alipofika stanini, alienda hadi maegeshoni. Nambari ya usajili kwa mintarafu ya risiti yake ilikuwa KBC 249 K. Mle ndani mlikuwa na “abiria” saba hivi yeye akaikamilisha idadi ya nane. “Dereva” aliingia na kuketi kwenye kiti chake. Tambo la mtu lililokula likashiba. Mazungumzo ya chini kwa chini yaliendelea baina yao isipokuwa Ningejua. Pale Karibu na dereva, uso ameuangusha, kichwa kimemlemea kwa uzito wa mzongo wa mawazo. Baada ya dakika ishirini hivi, hapakuwa na yeyote aliyeingia wala aliyetoka. Kiwewe cha mishipani kikaanza kumtinga. Baadaye, “dereva” aliondoka kisha “abiria” wakaanza kuondoka mmoja mmoja. Alijikuta amesalia mle ndani peke yake. Japo alihisi hatari ya namna fulani, hakuchukua hatua ya haraka, yawezekana aligandamana na methali ile ya kabla ya kuruka agana na nyonga.

Alipoenda ofisini ili kutaka kujua mbivu na mbichi, alimkuta mhudumu mwingine kabisa. Baada ya kuikagua stakabadhi yake ikabainika kuwa haikuwa rasmi kwani risiti halali sharti iwe na mhuri wa kampuni ya magari pamoja na sahihi. Hii haikuwa na haya mahitaji yote mawili. Maneno ya huyo mhudumu yalimwingia Ningejua akilini kwa mpigo na mrindimo wa radi. Moyo wake ukachuruzika na kunyiririka damu, damu ya machozi-machozi ya samaki yasiyodhihirika kwa macho ya nje. Akakitafuta kitambaa cha kuyafuta akakosa. Dunia! Dunia! Dunia tambara bovu; ukivuta utachana.

Alipokuwa akipita karibu na gari hilo alikutana na mama mmoja aliyekuwa akiuza ndizi pembeni. Aliusoma moyo wake kwa jicho pevu na kugundua kuwa akili zilikuwa zimemduru. Ningejua akauitikia wito wake wa ishara ya mkono na kumwendea. Hapo ndipo alipopasuliwa mbarika kuwa gari hilo limekuwa pale zaidi ya miezi kumi baada ya kuharibika! Aghalabu laghai hawa wamekuwa wakilitumia kuwapunja abiria wasio na ufahamu wa kanuni za usafiri kama huyu maskini. Licha ya kipato chake chechefu, mama huyu alimsabilia Ningejua kwa mengi. Haya ni pamoja na kumnasihi dhidi ya kukata tamaa maishani na kisha akamlipia nauli ya kumrejesha nyumbani. Alifika kwao akiwa na tahayuri na uchungu usiomithilika. Ilimgharimu zaidi ya miezi minne kuyauguza majeraha ya moyo na akili. Kumbe dunia nzito kwa mtu asiyefahamu!

Ni mwendo wa saa thenashara za machweo, jua angavu linapoendelea kupenyeza miale yake yenye wekundu wa damu, Sitamauke anaonekana kwa mbali akiteremka na kuteremua kutoka kwenye kilima hiki. Kinachoshangaza, hatembei kwa maguu yake bali yuaonekana akisowera, kutambaa na kujisombea kwa magoti. Kisa na maana yakini yuajua mwenyewe. Kwenye mkono wake wa kuume, alikibeba kijitabu kidogo chenye mchanganyiko wa rangi tofauti za upinde. Maandishi yaliyokuwa kwenye jalada yalisomeka waziwazi: *Klima chenye bubujiko la moyo.* Jua linapoendelea kuiramba mikoche na giza la kaniki kushika hatamu, ndivyo Sitamauke anavyoendelea kuyoyomea, kufichamana na kuvogomea kwenye ule utusitusi.

**jitathmini**

a) *Eleza mbinu ya lugha iliyotumika hapa "macho yake yanapigana pambaja na mandhari ya aina yake"*
b) *Taja maudhui yaliyojitokeza kwenye Makala haya.*
c) *Taja sifa bainifu za mhusika mkuu.*
d) *Eleza namna maudhui ya uongo ulivyomuathiri mhusika mkuu.*

# DAWA YA MAKOVU na Moses Nawale

Mzee Fwamba na mkewe Bi. Sarafina ndio waliokuwa wavyele wa Makovu mwana waliotunukiwa baada ya mahangaiko na pandashuka chungu tele. Makovu ndiye aliyefungua na kufunga ukurasa wa uzazi katika aila hii. Hata ujauzito huo ulipohitimu miezi sita madaktari walimshauri alazwe hospitalini ili aangaliwe kwa jicho la kitabibu wakati wote. Ulikuwa wakati mgumu sana kwa mzee Fwamba kwa sababu ya gharama ya hospitali pia upweke wa kumkosa mke wake. Kazi yake ya uhandisi iliyomlazimu kuzuru nje na ndani ya nchi haikuwezekana. Kwa nyota ya jaha Sarafina alijikopoa. Baada ya ganga ganga za matabibu, Sarafina alihakikishiwa kuwa asingeweza kuhimili kwani chupa yake iliondolewa kwa sababu za kiafya.

Makovu alizaliwa akiwa mwingi wa neema. Wazazi wake walimuenzi na kumuengaenga kama yai huku wakifahamu kuwa mtoto ni kito. Hawakusita kumkosoa na kumwonyesha tariki sahihi ya kufuata huku wakiwa vielelezo katika makuzi yake. Naam mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Licha ya wavyele wake kuwa wakwasi, Makovu hakusita kutangamana na watoto wenzake kutoka matabaka mbalimbali. Walicheza pamoja na hata kuwaalika maanzilini pao, ukarimu wake usingemruhusu kuwaacha bila cha kutia mdomoni. Angehiari kuwapa chakula chote. Jambo hili lilimsababishia ugomvi na wazazi wake kwani angeonekana akipiga miayo kila wakati kwa makali ya njaa.

Watoto wenzake walimpenda na kumuenzi kama mboni ya jicho. Makovu alijulikana sana, hata mtoto aliyezaliwa asubuhi kufikia jioni angemfahamu. Alikuwa na heshima, nidhamu na intidhamu kwa wakubwa na wadogo. Bidii zake za gogota agogotaye mti masomoni zisingemithilishwa. Alifahamu fika kuwa bidi hulipa na mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Katika darasa lake la saba aliibuka kifuambele kwa alama sheshe. Isitoshe, alikuwa mchezaji wa kutegemewa katika gozi. Shule ya Pantosha ilimtegemea sana katika ufungaji wa mabao yaliyoiletea shule yake ushindi. Kipaji hiki kilifanya shule nyingi zimmezee mate hususan shule za upili zilitaka sana ajiunge nazo baada ya kuufanya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane. Nazo shule nyingine zikimmezea mate kwa werevu wake masomoni na ucheshi uliomfanya kuteuliwa kufawidhi hafla mbalimbali shuleni.

Wazazi wake walijivunia sana. Mama yake aliyekuwa mwakilishi wadi, eneo la Mengichi, aliweza kuchaguliwa mara nyingi kwa sababu ya sifa za

mwanawe. Jina lililovuma lilikuwa mama Makovu, si katika maabadi yao ya Miujiza si shule zilizokuwa eneo hilo. Fwamba alijinyakulia kandarasi anuwai kwa sababu ya umaarufu wa mtoto wake ingawa pia kazi yake ilikuwa yenye ujuzi wa hali ya juu.

Makovu alipofika katika darasa la nane ilikuwa ibada shuleni Pantosha wanafunzi wote kuishi shuleni. Wazazi walikuwa na wakati mgumu kukubali. Walimzoea mtoto wao aliyekuwa burudani manzilini baada ya kutoka shuleni. Mwanao hakuwa na tatizo lolote kwani yeye aliyazoea maisha yoyote. Hawakuwa na budi kufuata sheria za shule kwani elimu ndio daraja imvushayo mja kutoka gizani hadi mwangaza. Aidha, tohara ya kisasa ni vitabu sio kisu cha ngariba. Baba yake mavuno alichukua muda ayami kumshauri mtoto wake kwani alikuwa anaelekea ulimwengu tofauti usiojali hali na nafsi.

“Makovu mwanangu, kesho tunakupeleka shuleni ambako utaishi hadi mwisho wa muhula. Isitoshe, umefika darasa la nane, unastahili kutia juhudi zaidi. Marehemu bibi yako siku zote alinikumbusha kuwa ukivipoteza vitu vyote utavipata, ukipoteza muda wako hutaupata kamwe isitoshe kesho yako imo ndani ya leo yako. Wewe ni mtu mwenye sifa kochokocho, Aisee! Mtu mwenye sifa bila matendo ni kama kalamu isiyo na wino. Unapoenda shuleni utatagusana na wanafunzi wa kila aina ambao wamechanganyika kama mchele na ndume. Usiwahi kusombwa na wimbi la shinikizo la rika. Usiambukizwe maradhi ya kutofuata sheria.” Mama yake alimbwagia nasaha kwani jungu kuu halikosi ukoko. Kwa sauti ya ninga alisema “Vijana wa hirimu yako wasikuteke na kukushawishi kuwafuata mithili ya bendera. Unaowaamini ndio wanaoweza kupotosha.”

Walishikana mikono na kupiga dua kwa Maulana, hiyo ilikuwa ada kwao. Usiku huo makovu hakupata hata lepe la usingizi kwani maneno hayo yalimkata mifupa na kumchoma uboho. Aligaragara kitandani huku akitafakari kuhusu maisha yake bwenini. Alikula yamini kuuma jongoo kwa meno na kujinoa vilivyo kukabiliana na mawimbi katika bahari ya elimu. Siku iliyofuata walijiandaa baada ya kushiriki staftahi na kung’oa nanga kuelekea shuleni. Walipitia madukani kununua vitu vitalivyomfaa mwanao shuleni.

Shuleni, waliwakuta wanafunzi wengi wakisajiliwa. Waliozoea mandhari wakiendelea na hamsini zao, Makovu alikutana na wanafunzi kadhaa waliokuwa wanajuana kutoka shule mbalimbali kwa sababu ya talanta yake iliyompa fursa ya kuzuru kwingi. Baada ya shughuli za usajili na Makovu kuonyeshwa bweni pamoja na kitanda chake. Alichukuliwa na marafiki zake

huku akiwaaga wazazi wake na kuwahakikishia kushikilia papatu wosia wao. Fwamba na mkewe walirudi nyumbani wakihisi upweke wa kumkosa mwanao. Wote walikata kauli kuwa aimarishe mustakabali wake na pia aanze kukabiliana na changamoto za ulimwengu mapema, chambilecho wahenga "Hii si dunia ya kulala. Dunia ni kazi. Ni dunia ya mapambano," alimwambia mkewe kuwa wazazi wasiowapa wanao elimu huwa wamewaua kifo cha uhai.

Makovu aliendelea kudhihirisha umaarufu wake pasi kulegeza kamba. Aliuma uzi masomoni. Alizidi kutamba katika michezo na ucheshi wake ukipanda upeo mpya kila uchao. Muhula wa pili uliwadia, muhula ambao huwa na shughuli chungu nzima kwa wanafunzi wanaokaribia kuifanya mitihani ya mwisho. Siku hii shughuli ziliendelea kama kawaida pasi ishara yoyote ya maafa huku Makovu akijizatiti kama ilivyokuwa ada yake.

Baada ya shughuli za kutwa na mavune yote, wanafunzi walienda bwenini kujinadhifisha kabla ya chajio. Ilivyyo ada katika shule nyingi za aina hii na wanafunzi wa kiwango hiki, wakati huo hutumika kucheza. Makovu alikuwa bwenini na masahibu wake wakipiga soga na kupanga mikakati kuhusu ufanisi wao masomoni. Haukupita muda mrefu kabla maghulamu hao waanze michezo ya paka na panya. Pengine hawakufahamu kuwa mchovya asali hachovi mara moja. Mchezo ulipamba sana kiasi cha kuanza kuchupia vitandani kama nyani. Juhudi za Makovu kuwasihi wenzake kukoma ziliangukia masikio yaliyotiwa komango. Makovu alisimama kitandani pake na kuanza kuvipanga vitu vyake akikosa wa kusemezana naye. Wenzake walimuasi na kumuambaa kama ukoma. Kwa muda usiomruhusu paka kunawia mate mwanafunzi mmoja, Potoka, aliruka na kumgonga nusura amng'oe meno. Kwa bahati ya mtende Makovu alimhepa na kumwacha aanguke kama gunia lililoshiba viazi. Alijaribu kuwatahadharisha lakini wakamkejeli kwa matwezo. Aliendelea na shughuli zake huku akiwaacha wenzake kucheza michezo yao waambao huamba mwana mkaidi hafaidi hadi siku ya Idi.

Akuchukiaye hakosi ila la kukutia. Bui wake Mavuno walikuwa wenye misuli tinginya ilihali yeye alikuwa kifyefye cha mtu. Potoka ndiye aliyekuwa amejaliwa na maungo. Ulafi wake wa fisi ulimlazimu kula sana. Kijana huyu alihiari mchezo kuliko masomo. Makovu alipokuwa amesimama juu ya kitanda chake huku akifunga vizuri chandarua, alisukumwa na Potoka aliyekuwa ameruka kutoka kitanda kimoja hadi cha Makovu. Aliruka kwa kasi ya umeme na maungo yake mazito kukutana na Makovu aliyekuwa ng'onda.

Kijana mdogo aliangukia mgongo huku akiangukiwa na Potoka. Kishindo kikubwa kilisikika huku akitoa sauti ya kite kwa maumivu makali. Alizirai. Wanafunzi walikusanyika wengine wakikimbia kumwita mwalimu wa zamu. Walimkimbiza hospitalini kwa gari la mwalimu. Wauguzi walimfanyia gangaganga zao ili kuokoa uhai wake ulioning'inia kwenye uzi mwembamba. Wazazi wake walipofahamishwa waliwasili kwa kasi, waama uchungu wa mwana aujuao ni mzazi. Mwalimu mkuu aliwaeleza kilichotokea shuleni. Daktari aliwaita wazazi wake pamoja na mwalimu mkuu. Kila mmoja alikuwa na hamu ya kujua hatima ya Makovu. Aliwafahamisha kuwa "Kulingana na picha za uyoka ameumia kwenye uti wa mgongo. Kwa hivyo itakuwa vyema kupelekwa katika hospitali ya rufaa kwa matibabu Zaidi." Baba yake alikubaliana na daktari mradi mtoto wake awe salama salmini. Aliletwa huku akisukumwa kwa machela hadi kwenye ambulensi na kung'oa nanga.

Walipowasili katika hospitali ya rufaa ya Twapona walipokelewa na wauguzi waliompitisha hadi kwenye sadaruki, ambapo walimweka kwenye mitambo maalumu kumuezesha kupumua. Madaktari walioshiba tajiriba walimzunguka na kumhudumia. Baada ya juhudi za wataalamu, Makovu alijirudisha fahamu zake. Alitiririkwa na machozi alipowaona wazazi wake huku mama yake akishindwa kuzuia kilio. Wajuzi wa lugha waligonga ndipo waliposema, mzaha mzaha hutunga usaha. Siku zilizidi kusonga. Makovu akiwa hospitalini huku wazazi, walimu na marafiki zake wakifunga safari kila uchao kumtembelea hospitalini. Safari iliyoanza kama mchezo iliishia hospitalini na kumgharimu Makovu. Mkono uliokuwa umevunjika ulifungwa kwa plasta nao uti wa mgongo ukishindwa kustahimili mwili wake, jambo ambalo lilimlazimu kutumia kiti maguro.

Baada ya kipindi cha miezi mitatu hospitalini, Fwamba alimchukua mtoto wake kutoka hospitalini baada ya madaktari kumhakikishia Makovu yu shwari ila tu asingeweza kutembea. Lazima atumie kiti maguro. Akawatahadharisha kuwa wawe waangalifu na iwapo atalalamika kuchoka na kuhisi uchungu mahali popote wamkimbize hospitalini. Ilikuwa hali ngumu kwake Mavuno. Pale nyumbani alitembelewa na marafiki zake, wanafunzi wenzake na pia watu mbalimbali waliomfahamu. Wazazi wa Potoka walikuwa miongoni mwa wale waliomtembelea huku wakiwa na mazungumzo ya kina na Fwamba, waliahidi kumfidia Mavuno kwa vyovyote vile huku kila mmoja akikashifu kitendo cha Potovu.

Mtihani wa kitaifa ulibisha hodi huku Mavuno akiwa hospitalini. Alilazimika kufanyia mtihani wake wa kitaifa pale pale jambo ambalo liliwahuzunisha wengi. Makovu aliwasihi wazazi wake wasikubali fidia kutoka kwa wazazi wa Potoka. Lililowaatua moyo ni pale aliposisitiza kuwa wamwite Potoka wazungumze pamoja na wazazi wake na mwalimu mkuu.

Asubuhi hiyo jamii zote mbili na mwalimu mkuu pamoja na viongozi walikuwa pale. Makovu aliketi kitandani na kumtazama Potovu. Makovu alipaza sauti na kusema “Nafurahia kuwaona, namshukuru Mola kwa kunipa nafasi nyingine ya kuishi ingawa mlemavu. Sitasita kumcha Mungu katika hali yoyote ile jinsi watushaurivyo makasisi wetu. Nachukua nafasi hii kumsamehe ndugu yangu Potovu na pia kuwaarifu wazazi wake wasigharimike kunifidia yaliyotokea tuyazike katika kaburi la sahau na tuangazie yajayo”.

Aliwasihi wote washikane mikono na kumwamuru kasisi kuomba, huku naye akiwa amemkumbatia Potovu. Jambo hili liliwaacha wengi wakiwa na maswali mengi bila majibu ikizingatiwa wote wawili walitoka katika makabila mawili yaliyokuwa maji na mafuta. Siku ya pili baada ya Makovu kutoka hospitalini matokeo ya mtihani yalitangazwa. La kushangaza Makovu alikuwa amejizolea alama mia nne ishirini na tisa juu ya mia tano na kuwa wa kwanza katika gatuzi lao. Alisherehekewa na wengi huku akihojiwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari, alialikwa na rais ikuluni. Alifadhiliwa masomo na hata maisha yake. Hali hii ilifungua ukurasa mpya katika maisha yake na ya wazazi wake. Kwa kweli msamaha ni dawa mujarabu ya makovu yote maishani.

***Jitathmini***

a) *Taja sifa zozote tano za wahusika wafuatayo: Potovu na Makovu*
b) *“Hii si dunia ya kulala. Dunia ni kazi. Ni dunia ya,” Weka dondoo hii katika muktadha yake.*
c) *Taja mbinu zozote za lugha zilizotumika.*

# KILEMA CHA MUNGU KINA MWENDOWE na Elizabeth Barasa

Wenyewe waliionea shule paa. Huku hakukuwa kupenda kwao. Zama zao kusoma kulikuwa gharama sana si kama siku hizi ambapo masomo ya msingi ni dezo. Walitamani kurudi shuleni lakini wapi? Kila siku wangerauka mapema kuanza kutafuta ajira kwa njia yao ya kawaida, ombaomba. Daima walikasirika sana kuwaona vijana walioenda shule wakivaa suruali huku zikiteremshwa makalioni. Wasichana kuvaa mavazi yaliyowaacha nusu uchi kuliwahuzunisha ajabu. Walisema kuwa wana wao wasingekuwa wakiathiriwa na mmomonyoko wa maadili.

Ndoto hizi zilipigwa chenga. Hawakuwa na mtoto. Miaka kumi na mitano katika ndoa. Hilo ndilo lililokuwa doa kubwa sana zaidi kwenye ndoa hii. Juhudi zote za kupata mwana ziliambulia patupu. Viongozi wa dini walioshauriwa nao hawakukosa jibu lao la kawaida. “Ipo siku Mungu anaweza.” Bwana Subra na Bi. Kosa walikosa watoto katika kipindi cha miaka kumi na mitano katika ndoa yao. Kila mmoja wao hakukosa mshauri wake. Kosa alishauriwa awe na jicho la nje kwa kuwa huenda mumewe ndiye aliyekuwa gumba. Naye Subra akashauriwa kuwa akamwoe mke mwingine kwa kuwa huenda Kosa alikuwa tasa.

Yote hayakuwahusu ndewe wala sikio. Hawakutaka kufuata njia walizofuata familia ya Tamaa. Nao walikosa mtoto. Mama alishauriwa akashaurika kutafuta mtoto nje ya ndoa yao. Naye baba akamwoa mke mwingine. Bwana huyu alimfukuza mke baada ya mwengine. Mkewe naye alifanya vivyo hivyo. Alivyokosa ujauzito ndivyo alivyowabadilisha. Kisima kilijaa siafu baadaye. Mchezo wao ulifanya waambukizwe maradhi ambayo hawakuwa na mwao kuyahusu. Walianza kukonda kama ng’onda. Mili yao ilikosa kinga dhidi ya ukongo. Walikataa katakata kuenda hospitalini kwa kuwa waliamini ushirikina. Baada ya kipindi kifupi maisha ya bwana na Bi. Tamaa yalisimuliwa kijijini kama hadithi ya kufundisha uvumilivu na kutokata tamaa maishani.

Kufumba na kufumbua Bi. Kosa alipata ujauzito. Waliowadharau walizifyata ndimi zao. Vyakula walivyokula huenda visingetosheleza mahitaji ya malaika huyo. Walikula aina moja ya chakula. Kama hao wenyewe walizidi kukondeana wangeyakimu kweli mahitaji ya mwana wao? Mjamzito alipokosa

chakula ilimbidi kunywa maji mradi kikembe tumboni asikose cha kutia tumboni. Siku zilisonga. Kujifungua kwa mama kulitarajiwa baada ya wiki mbili. Naye Mungu alijibu ombi lao. Bwana wake alipata ajira katika kampuni ya kuoka mkate mjini. Kazi hii aliifanya mchana kutwa pasi na kupumzika. Aliporudi jioni au usiku mchanga alikuwa amenyong'onyea. Aliweka akiba ili ije iwafae siku za usoni hasa mkewe atakapojifungua. Naam, alijikumbusha kuwa akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni.

Usiku wa manane siku ya Ijumaa, mkewe alilalamikia maumivu tumboni. Hii ilikuwa taashira tosha kuwa wakati wa kujifungua umewadia. Mumewe alikimbia kwa majirani ili kuomba msaada. Majirani hawakumfungulia mlango. Akaamua kuanza safari ya kurudi kwake. Alihisi kuwa bui yake wa kufa kuzikana angekuwa suluhu. Naye hakukosa sababu ya kukosa kuenda. Sauti yake ilisikika kutoka katika kibanda chake, "Nitapitia alfajiri. Kwa sasa kuna giza sana." Alikutana na mtoto wa umri wa miaka kumi na miwili hivi kwa jina Masika. Alikuwa na sura ya kawaida. Hakuna hata mmoja aliyejua alikoishi wala kulala.

"Mbio gani hizi usiku huu?" "Mke wangu anajifungua sasa hivi nilikuwa nikitafuta msaada kwa marafiki nikakosa." "Naomba niende nikusaidie," yule chakaramu akalonga. "Mimi niliachia masomo katika darasa la nane. Shuleni nilikuwa gwiji hususan wa Sayansi kwa hivyo naomba niandamane nawe huenda nikatumia ujuzi mdogo nilioupata kutoka kwa mwalimu wangu wa Sayansi mwalimu Elifasihi Wambambo." Bwana Subra alipata ujasiri wa kuandamana na kijana huyo.

Walipofika nyumbani, mke alikuwa tayari amejifungua salama salmini. Masika aliinawa mikono yake na kuomba kisu alichokitumia kuikata kamba iliyomwunganisha mama na mtoto wake. Alipojaribu kuamka alimzuia na kumwambia kuwa atulie kwa kuwa baada ya dakika za kuhesabu kuna kitu ambacho kingezaliwa. Mama na mume wake walipigwa na butwaa. Hawakuwa na shida ya pacha. Janga kubwa zaidi lingekuwa kuwalea. Kitu kilichofanana na nyama kilitokeza. Aliwajuza hicho ndicho kilichomlisha mwana tumboni. "Ukila ama kunywa mtoto hayanywi maji hayo moja kwa moja. Viungo havijaimarika kiasi cha kusaga vyakula na kukibadilisha katika hali iliyo sawa kutumika mwilini."

Alimshika yule mtoto vyema mama. Mzazi alikuwa amechoka hoi bin tiki. Alimpangusa malaika na kumpiga kofi moja jepesi. Alilia kilio kilichomzindua mama yake. Alipoona kuwa wasiwasi ulitanda mle, aliwaweka wazi kwa haraka

kuwa kofi hilo linamzindua na kuamsha viungo vyake. Hapo ndipo alipoanza kupumua. Baada ya michakato mizima ya kuzalisha aliomba kuondoka baada ya kuwashauri kuenda hospitalini asubuhi ili ukaguzi zaidi ufanywe. Aliwaambia kuna chanjo maalum ambayo mtoto angepewa. Alikatazwa kuondoka. Aliombwa kuwa pale kama mwana wa boma hilo. Hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya pekee ya kuonyesha shukrani. Alikubali.

Baba alienda jikoni kuandaa uji wanywe baada ya kazi hiyo. Masika alimzuia. “Mpe mkeo masimulizi na umshukuru Mungu. Mpe matumaini nikiandaa uji tunywe.” Alipouleta uji wenyewe mezani hawakuamini walichoonja. Alipoulizwa alikoitoa sukari, aliwajibu kuwa katika kuomba kwake hapa na pale alikuwa akila tano na kusaza tano. Siku iliyofuata alimsindikiza Kosa hospitalini huku Subira akienda kazini. Alikuwa amechelewa kutokana na shughuli alizokuwa nazo usiku. Punde alipofika alisalimiwa na barua ya kupigwa kalamu kwake. Walipitia kipindi kigumu cha uchumi. Masika alikuwa wa kwanza kufanikiwa. Alipata ajira katika duka kuu la mzungu fulani jijini. Hakuwahi kuwa na mfanyakazi mwenye maadili kama Masika. Masika alimweleza asili yake. Alimaliza kwa kumjuza wazazi wake wapya na madhila yao. Bwana Subira aliulizwa anachotaka. Akasema. “Naomba mwanangu Masika alipiwe karo.” Bila kupoteza muda Masika alipelekwa shuleni na nafasi yake pale dukani kutwaaliwa na bwana Subira.

Masika aliyazika masaibu yake yote katika kaburi la sahau. Alikata kauli kuzamia matopa ya vitabu. Polepole alianza kuwapiku wanafunzi wenzake ambao walikuwa wakilaza damu pale darasani. Baada ya muhula mmoja hakuwa chura tena. Tabia zake bulibuli zilipigiwa mifano. Mwaka ulipoisha na matokeo ya mtihani wa kitaifa kutangazwa aliibuka kuwa wa tatu katika nchi nzima. Alipata mfadhili aliyemsomesha. Akawa na bidii za duduvule agotaye gogo. Alihitimu kwa alama A chanya. Hatimaye alijiunga na chuo kikuu aliposomea uhandisi. Hatimaye akahitimu na kuanza kutafuta ajira katika miji mbalimbali.

Mseto wa mawazo ulimtinga kila mtu kwenye familia hiyo. Majanga yalibisha hodi kwao. Namna Baraka alivyozidi kukua ndivyo mguu wake ulivyozidi kuteguka hadi akawa kiwete. Wavyele hawa walitumia kila mbinu kumponya Baraka lakini wapi?

Baada ya miaka kumi. Masika alikuwa mkurugenzi katika kampuni moja mashuhuri ya ujenzi wa barabara nchini Ujerumani. Masika alirejea nyumbani kwa lengo la kumaizi maendeleo ya nyumbani pale. Aidha, alikuwa

na mpango wa kupata jiko. Alitaka kuwahusisha "wazazi" wake. Alipofika nyumbani alipigwa na butwaa ghaya. Alimhurumia mdogo wake. "Wazazi wangu ni sharti Baraka aende shuleni hii ni karne ya ishirini na moja. Kila mtoto licha ya ulemavu ana haki ya kusoma. Awe kiziwi au kiwete." Kosa na Subra walikubali kuwapeleka wana wao shuleni kwa ufadhili wa Masika. Baraka alilemewa na masomo. Yaliingia kwenye sikio moja na kupitia kwenye jingine. Hata hivyo, alikuwa gwiji wa kandanda za viwete. Alifaulu kuiwakilisha shule katika mashindano mbalimbali. Katika fainali za kombe la jimbo Baraka alikuwa mvamizi. Alipata nafasi ya kuiwakilisha jimbo lake. Alikuwa mfungaji bora katika michuani yote iliyotangulia. Hili lilimfanya kuwa tegemeo kubwa sana katika jimbo na hata kwa wachezaji wenzake. Alikuwa tayari kumenyana na jimbo la Bingwa ambalo ndilo lililotwaa kombe hilo katika msimu uliopita.

Prrrrrr! Kipenga kilipulizwa na bila cha msalie mtume wala nabii mechi ikang'oa nanga. Nambari tisa mgongoni alimwandalia Brighton pasi nyerezi kimo cha kuku. Alitamba nao na akapiga mnazi kumtafuta Hazard lakini wapi! Duma alirushiwa mpira na pasi kuganzaganza akaupasi kwa Sungura. Baada ya ujanja wa hapa na pale, akampa pasi Panzi. Alijipenyeza katikati ya msitu wa wapinzani. Akatoa pasi maridadi kwa Baraka aliyefunga bao maridadi. Kila mchezaji alizitumia mbinu zake zote kutafuta ushindi. Wakati fulani baadhi ya walinzi walikuwa mbele ungedhani ni washambulizi. Mchezaji wao nyota aliwavisha walinzi kanzu na akabaki na kipa peke yake. Akaupiga mpira kwa nguvu zake zote. Sakata ikaponea chupuchupu baada ya mpira kukigonga chuma cha lango na kurudi ndani. Ulipokelewa na Ronko aliyepiga krosi ndefu kumtafuta Karia ambaye alikuwa amechoka sana. Alimwona alipokuwa Baraka na akauacha mpira kupita bila hata kuugusa. Alimchenga yeyote aliyedhamiria kumnyang'anya mpira ule. Hata nyasi zilipokea chenga za maudhi. Mlindalango kwa umahiri wake alichupa kama nyani kuudaka mpira ule. Akaelekea kulia kumbe Baraka aliuelekeza mpira kushoto. Yakawa mabao matatu kwa nunge.

Hakuna aliyesherehekea bao hilo. Hata wachezaji walibaki mdomo wazi wakishangazwa na mbinu ya Baraka. Wapinzani na mashabiki wao pia walitulia tu. Ilikuwa vigumu kujua lilivyofungwa. Wengine walidhani katumia miguu, wengine mikono, wengine mgongo na kadhalika. Katika sintofahamu hiyo refa alipuliza kipenga na mechi ikaishia hapo. Baraka alipokea tuzo za mchezaji bora na mfungaji bora. Baadhi ya mambo aliyofurahia baada ya ushindi huo ni kupata nafasi ya kuchezea timu ya Uatilifu. Alipata nafasi ya

kuichezea timu hiyo iliyochukua nafasi ya tatu katika msimu uliokamilika nchini Uingereza. Timu hiyo ya Walema ilikubali kumlipa milioni mbili kila wiki. Pia angeendelea na masomo yake huko Ulaya. Sherehe zilitanda kote kijijini mwao. Katika jimbo lao hakujawahi kuonekana mlemavu akifanikiwa hivyo. Habari zake ziligonga vichwa vya habari nchini kote. Katika hotuba yake alipokuwa akiaga kuenda Uingereza, alidokeza kuwa baada ya mwaka mmoja angerudi kuwajengea walemavu viwanja vya kuchezea michezo mbalimbali. Aidha, alisema kuwa angefanya juu chini kuwatafutia wenzake udhamini wa kusomea nje. Alijitolea kubadilisha mtazamo wa wengi kuwa walemavu wamelemewa.

Baraka anakumbuka miaka kumi iliyopita, Ndege mbili zilitua ghafla katika uwanja wa shule ya Utawala. Wananchi wote, wakubwa kwa wadogo walichana mbuga kuenda kujionea kilichojiri shuleni. Aghalabu wakazi wa sehemu hii wanapoona ndege hujua kuwa huwa ni mwanasiasa fulani anayewania uongozi au anayetaka kusalia uongozini. Waja walifurika uwanjani furifuri wasione hata mmoja aliyetoka mle. Licha ya kuwa ngojangoja huumiza matumbo wanakijiji hawa walijitia moyo kuwa subira huvuta heri. Hawakuchoka kusubiri. Kila mmoja alikuwa na ufahamu kama ilivyo desturi yao kuwangoja hadi mamia ya watu yajae. Dakika thelathini baada ya ndege zile kutua magari matatu meusi tititi kama kaniki yalifika pale. Yalijipenyeza katikati ya halaiki ya watu hadi palipokuwa na ndege zile. Watu wanne waliokula wakashiba walitoka. Walikuwa wamenenepa ungedhani ni nguruwe. Walikuwa wafupi kama nyundo ya seremala mbilikimo. Baada ya kukagua umma kwa dakika moja wengine wawili walijitokeza. Kwa haraka waliingia garini na kuondoka bila kunena chochote. Hakuna aliyesadiki tukio hilo. Wengine walisikika wakijiuliza kile wangekula siku hiyo. Hii ni kwa sababu walikuwa wameacha amara zao adhimu kwa kutegemea cha wanasiasa. Wakawa sawa na aliyeifungulia mlango bahati ya mwenziwe.

Msafara huo wa magari ulijipenyeza katikati ya vibanda vilivyokuwa makazi maalum ya watu wa sehemu hizo. Wananchi waliokuwa na kiu ya kutia chai mfukoni hawakuchoka kuufuata. Licha ya magari yale kuonekana kuwa na haraka, matope na hali mbaya ya barabara za sehemu zile isingemruhusu kuenda kwa kasi. Mwendo wao ukawa wa kobe. Hawakutamauka kuendelea na safari yao. Kumbuka, mbio za kasa si mbio lakini humfikisha mbali. Wananchi pia hawakuchoka safarini. Kwa kweli, walikuwa mawindoni wakiwinda chajio cha siku hiyo. Chajio chenyewe kilikuwa pua na mdomo. Wengine walidondokwa

na mate kinywani kwa tamaa ya chajio ambacho kulingana na wengi kilikuwa kikinukia. Wengi waliacha amara zao. Walikuwa na uhakika kama mauti kuwa heri cha bure upatacho kwa dakika moja kuliko jasho lako lijalo baada ya kujipinda mgongo. Mwendo huo ulichukua muda mrefu bila hata mmoja kujua hatima yake.

Kwa kweli, hakuna refu lisilokuwa na ncha. Wageni wale walishuka kutoka kwenye mashangingi yao. Walienda masia moja kwa moja katikati ya vibanda kadha wa kadha. Hatimaye wakatua na kutulia kwenye kibanda cha Kosa na Subira. Hawakuwa na budi kusimama kwa kuwa pale hapakuwa na kiti chochote. Vigoda vitatu vilivyokuwa mle walipewa ila wakakataa katakata kukalia. Kwa ukarimu waliachiwa ila msimamo wao ukawa uleule. Wageni wale waliomba wazazi na mwana wao wavitumie. Kwenye paa masizi ya zama za zama yalikuwa yametawala na kutamalaki. Vikombe vichache vilivyokuwa na utando wa buibui vilikuwa vimekusanyika kwenye kona kwa masikitiko. Katika kona nyingine kulikuwa na jiko lenye mafiga mawili. Mafiga yenyewe yalikuwa safi kwelikweli. Baadaye ilikuwa wazi kama jua la mtikati kuwa mafiga hayo mara nyingi yalitumika kama viti. Hakukuwa na mende hata mmoja mle. Ni kunguni chungu nzima walionekana vumbini. Walikuwa wamekonda na kukondeana kama ng'onda. Wageni wale wakizidi kushangazwa na hali ile mmoja wao alitoka nje na kuingia garini mwake. Aliporudi alikuwa na chupa mzomzo za maji na vinywaji. Alimkabidhi bwana Subira.

"Mimi ni waziri wa michezo katika nchi yetu," mmoja wao alijitambulisha. "Tumefika hapa ili kumpongeza kijana Baraka kwa kuinua sanaa ya kandanda nchini. Aidha, pokeeni pongezi za rais aliyetamani kufika ila akakabwa na majukumu ya kitaifa. Hata hivyo ameagiza kuwa Baraka amzuru ikuluni atakapokuwa na likizo. Gharama zote za usafiri zipo." Mamia ya wanahabari walifurika pale furifuri. Kamera za video na picha zilimulika kila mahali. Waziri wa serikali alifika kwa mara ya kwanza katika makavazi yale.

Amini usiamini, kwa mara ya kwanza waliyaona magari ya kifahari. Bwana Subira na mkewe walihojiwa na wanahabari wale. Masaibu waliyokuwa wakiyapitia awali yalisheheni mazungumzo yao. Isitoshe, walimmiminia sifa sufufu mwana wao, ama kweli kilema cha Rabana kina mwendowe.

Baada ya saa kadha wa kadha pale, wageni wale waliondoka baada ya kuahidi kurudi pale. Pamwe na hayo, waliahidi kumpa kazi Kosa. Wazazi wake pamoja na wakazi wote wa maeneo yale waliahidiwa makazi bora. Wanakijiji walirudi katika hamsini zao. Wengine walijutia kuacha amali zao. Wengine pia

waliondoka wakiwa na tumaini jipya. Walikuwa na ufahamu kuwa mja yeyote anaweza kufua dafu katika jambo lolote analolifanya. Kamwe maumbile na ulemavu si kizingiti chochote katika ufanisi wa mja. Wengine pia walipata mafunzo kuwa heri kutia bidii kazini mwako kuliko kutarajia usaidizi wa wengine. Ukawa ukweli wa usemi unaosema kuwa mtegemea cha nduguye hufa maskini. Familia ya Kosa na Subira nayo ilibaki ikiogelea katika dimbwi la furaha ya mvuvi aliyekinasa kishazi cha samaki.

Maisha yao yalikuwa yameanza kuchukua mkondo mpya. Kweli baada ya dhiki ni faraja. Miezi miwili baadaye, nyumba za gharama ndogo zilianza kujengwa katika maeneo yale. Juhudi za Baraka nazo hazikuzikwa katika kaburi la sahau. Aliukumbuka usemi maarufu wa aliyekuwa mwalimu wake wa Kiswahili, Funza Mweusi, "Huduma kwa jamii ni huduma kwa Maulana." Kila mwezi alirejea pale mtaani na kuzindua miradi chungu nzima. Si viwanja vya soka si shule za walemavu. Alinunua ploti na kuwajengea wavyele wake makazi ya maisha.

| **Jitathmini** |
|---|
| *a) Taja na ufafanue sifa tatu za mhusika Masika.*<br>*b) Kila mja ana uwezo maishani. Toa ithibati ya kauli hii kwa mujibu wa hadithi hii.*<br>*c) Mungu akifunga njia hapa hufungua kule. Thibitisha kauli hii.* |

# SHEREHE.

## 1. <u>Kimbunga - Wepoh Wesah</u>

- *Kisaa* - salio
- *Rangaito* - wasiwasi au vangaito.
- *Hakufaitika* - hakuchelewa au hakukawia
- *Taksiri* - hali ya kutokamilika. Pia huitwa upungufu
- *Aliangema*- alikata tamaa au kuvunjika moyo.
- *Saburi* - uvumilivu
- *Magube* - ujanja.
- *Gubeti* - omo ya jahazi.

## 2. <u>Nguvu za Sindano - Kaka Fred</u>

- *Vunga* - nywele nyingi zisizotunzwa vizuri
- *Moma* - aina ya nyoka aliye na mdoadoa
- *Mng'ong'o* - mti mkubwa wenye majani madogomadogo.
- *Shazasi* - dawa ya kumnusisha aliyezirai ili azinduke
- *Mzuza* - daktari wa nyoka
- *Kania* - dawa inayotibu mishipa
- *Uzio* - ua wa maua, miti au matofali

## 3. <u>Pesa Nyeusi - Hector Mbati</u>

- *Alisadiki* - aliaminikavutwa
- *Chochea vidondo* - fitini au sababisha watu wakosane.
- *Mshawasha* - kiu ya kufanya jambo fulani
- *Likaburutwa* – likavutwa

## 4. <u>Aliporudi - Samwel Nyongesa</u>

- *Arubii*- Haraka au upesi.
- *Fahaiwa* - Maana.
- *Paruwanja* - Waziwazi.
- *Nanigwanzula*- Mjusi kafiri.

## 5. <u>Tundu la Tamaa - Vitalis Nadecho</u>

- *Beramu* - kitambaa cha kuonyesha chama au taifa; bendera.
- *Chauchau* - hongo, kadhongo, mlungula, chai.

- *Shangingi* - gari zuri la kifahari.
- *Mwiko* - jambo lisiloruhusiwa kufanywa.
- *Ugali wa bada* - ugali wa unga wa mihogo au ndizi

## 6. Elimu ya Sumu - Alex K Nalianya

- *Ombwe* - Uwazi katika kitu kilichotolewa hewa.
- *Dubwasha* - kitu kisicho na thamani.
- *Wanaselea* - ishi mahali kwa muda mrefubila ya kuondoka.
- *Fulusi* - hela, pesa.
- *Pembejeo* - vitu kama vile; mbegu, mbolea nk kwa ajili ya kilimo.

## 7. Pang'okapo Jino - Humphrey Onkoba

- *Zahama* **-** ghasia kubwa, fujo au vurugu.
- *Kadhia* **-** jambo linalotendwa; tukio, mkasa.
- *Kiambo* **-** mahali wanapoishi watu
- *Aligwaya* **-** kutetemeka kwa hofu au baridi
- *Tanabahi***-** kukumbuka kwa kushtukia, kujua ghafla

## 8. Yakija Nayatwae - Kaka Maina

- *Mbinde* **-** taabu, dhiki
- *Kuhanja* **-** kutangatanga, kuenda huku na huku
- *Afua***-** afya nzuri, uzima
- *Mishumbi*- mlima mdogo wa kitu kama vile udongo.
- *Gubu*- hali ya kutokuwako utulivu; ghasia

## 9. Mali ya Umande - Patrick Mukanga

- *Kibatari - taa ndogo yenye utambi pia huitwa koroboi*
- *Fanya porojo - mazungumzo ya kupitisha wakati*
- *Kachara – taka*

## 10. Tumaini - Amos Khayota

- *Kitwea* - hali ya kukaa mahali pekee. Pia huitwa upweke.
- *Chelea* - acha kufanya jambo kwa kuhofia matokeo mabaya.
- *Pukachaka*! - neno linalotumika kubeza au kudharau kitu
- *Chale*- alama ya kuchanjwa kwenye mwili wa binadamu.

## 11. Bonde la Masikitiko - Mwalimu Sammy

- *Kuli*: Sema
- *Adhimu*: Muhimu
- *Mbawazi*: Moyo wa wema, huruma, shufaka, rehema
- *Ubigoubigo*: Mwisho wa kitu; ukingo

## 12. Mtindi Wamponda - Moses Odongo

- *Ugimbi* - pomba au ulevi
- *Faranga* - fedha zinazotumika Ufaransa na Ubelgiji
- *Ukiritimba* - tabia ya kujilimbikizia mali, sifa au madaraka bila ya kujali wengine pia huitwa, uhodhi.
- *Nduli* - adui asiye na huruma. Pia huitwa dhalimu au katili.

## 13. Kilima chenye bubujiko la Moyo - Washington Bin Juma

- *Gudulia* - mtungi mdogo wa udongo wa kauri.
- *Kadhia* - kijiji au kitongoji.
- *Akadhukuru* - akakumbuka.
- *Mchafukoge* - vurugu
- *Kukirihisha*- kufanya mambo ya kuchukiza watu. Pia huitwa hizi.

## 14. Dawa ya Makovu - Moses Nawale

- *Sadaruki*: chumba hospitalini kilichotengwa kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa mahututi. Pia *sakarati*.
- *Utatagusana*: utatangamana.
- *Kula yamini*: Kutamka jina la Mungu kwa ajili ya kuthibitisha jambo au kitu.
- *Kito*: jiwe la thamani.

## 15. Kilema cha Mungu kina Mwendowe - Elizabeth Barasa

- *Chura* - wa mwisho.
- *Kasa* - mnyama wa baharini afananaye na kobe.
- *Dezo* – bure.

# SHAJARA YA WAANDISHI

**1. Wepoh Wesah**
Wepoh ni mzawa wa *Mumias,* kaunti ya Kakamega. Ni ashiki wa lugha ya Kiswahili. Alisomea shahada ya *Ukapera* katika Chuo Kikuu cha *MOI,* kisha Shahada ya *Uzamili*, Chuo Kikuu cha *Nairobi.* Amefunza katika shule ainati mathalani: *Shule ya wavulana ya Kolanya* na *Friends School Kamusinga*. Kwa sasa ni mwalimu wa shule ya *St. Joseph's Nalondo,* Bungoma.

**2. Kaka Fred**
*Kaka Fred* ni mzawa wa Magharibi ya Kenya. Ameandika riwaya za *Siri ya Hujafa*, *Sumu*, *Gizani*, *Safari ya Dafina*, *Malezi ya Kiswahili* na diwani mathalani: *Mwamba wa Dhahabu na Hadithi Nyingine*, *Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine*. Amehariri vitabu vingi na kuchangia makuzi ya Kiswahili katika vyombo vya habari. Ni mkurugenzi mkuu wa KITOVU CHA HADITHI.

**3. Hector Mbati**
Mbati ni mzawa wa *Tongaren* kaunti ya *Bungoma*. Alisomea Shahada katika somo la Kiswahili na Dini katika Chuo Kikuu Cha Moi. Amechangia makuzi ya Kiswahili kupitia tamasha za muziki. *Hector* amechangia kunoa lugha ya Kiswahili katika shule ainati zikiwemo; *Luri High School Siaya, Lenana Girls, Light Academy na St Erastus schools Bungoma*. Kwa sasa ni mwalimu wa Shule ya Wavulana ya Kitaifa ya *St. Joseph's Kitale.*

**4. Samwel Nyongesa**
Nyongesa ni mzaliwa wa *Kamukuywa* gatuzi la Bungoma. Alisomea stashahada ya elimu chuo cha walimu cha Chesta kaunti ya Pokoti Magharibi. Amefunza shule ya *Limo's Kitale.* Kwa sasa ni mwalimu wa shule ya Sunflower Kapenguria kaunti ya Pokoti Magharibi.

**5. Vitalis Nadecho**
Nadecho almaarufu *Mtema Madini* ni mzawa wa Busia. Ana tajiriba katika somo la Kiswahili. Amefunza shule ainati zikiwemo; *Esirisia* Busia na *White Cots*, Kiambu na Shule ya Wavulana ya *Lukonyi* mjini Busia.Ni mwandishi wa riwaya ya Shaka na Shake. Amechangia katika uandishi wa diwani; Mwamba wa Dhahabu na Hadithi Nyingine, Wosia wa Mashairi na Diwani Ya Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine.

**6. Kamoti A. Nalianya**
Nalianya ni mwalimu mwenye tajriba katika ufundishaji na utahini wa Kiswahili. Ni mwandishi maarufu wa vitabu na mashairi. Amechangia ukuzaji wa Kiswahili kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Kwa sasa ni Mwalimu wa Kiswahili na Jografia katika shule ya *St. Joseph's Girls Kitale*, Trans-nzoia.

**7. Onkoba Humphrey**

Onkoba ni mzawa wa kaunti ya *Nakuru*. Ni mwandishi mwenye tajiriba ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Amefunza katika shule tofauti nchini. Kwa sasa ni mwalimu wa *shule ya upili ya Karati* kaunti ya Nyandarua. Onkoba ni mtahini wa kitaifa katika somo la fasihi.

**8. Kaka Maina**

Maina ni mzawa wa mkoa wa kati. Ni mwandishi aliye na tajiriba katika fasihi na lugha ya Kiswahili. Amefunza katika shule tofauti nchini. Ni mtahini wa kitaifa katika somo la fasihi. Amechangia hadithi kwenye diwani ya *Wingu limetanda na Hadithi Nyingine*.

**9. Patrick Mukanga.**

Patrick Mukanga ni mzawa wa *Bujwang'a* kaunti ya Busia. Alisomea taaluma ya uanahabari na kufanya kazi na shirika la *KBC ATG TV* na *PA TV* akiwa mhariri mkuu. Ni mwandishi aliye na tajiriba katika lugha ya Kiswahili.

**10. Amos Khayota**

Khayota ni mzawa wa Kaunti ya Bungoma. Ni mwandishi wa lugha na fasihi ya watoto. Amechangia katika makuzi ya lugha kupitia michango yake kwenye vipindi vya redio na runinga. Alihusika kwenye uandishi wa diwani ya *Mwamba wa Dhahabu na hadithi nyingine* na *Zawadi ya baba na Hadithi Nyingine*. Kwa sasa, yeye ni mwalimu wa shule ya *Christ the King*- Bungoma.

**11. Mwalimu Sammy**

Oluoch almaarufu *Mwalimu Sammy* ni mwalimu mshtiti wa lugha ya Kiswahili katika shule ya *Utawala* kaunti ya Narok. Amekuwa mstari wa kilele kuhanikiza lugha ya Kiswahili kupitia kwenye vyombo vya habari. Ameandika: *Siri za Insha Aula*, *Kisima cha Mkata*, *Mwamba wa dhahabu na Hadithi Nyingine* pamoja na *Zawadi ya baba na Hadithi Nyingine*

**12. Moses Odongo**

Odongo ni mzawa wa *Neela* kaunti ya Busia. Ni mwalimu mshtiti wa lugha ya Kiswahili katika shule ya *Sikoma* kaunti ya Busia.

**13. Washington Bin Juma**

*Washington Bin Juma* ni mwandishi aliyetopea katika uandishi wa Fasihi. Ameandika; *Chozi la Damu*, *mkuki wa Moyo* na kuhusika katika Antholojia ya *Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine.* Amefunza shule ainati zikiwemo; *Makini* school tawi la Kisuma na *The Fountain Grammar School Matunda*. Kwa sasa anafunza *Turkana Blooms* Mjini Lodwar akiwa naibu wa Bw. *Maurice Wakhungu*.

**14. Moses Nawale**

Moses Nawale ni mzalendo kindakindaki wa lugha ya Kiswahili. Ameijenga lugha hii katika shule mbalimbali humu nchini. Alichangia hadithi kwenye antholojia ya

*Mwamba wa Dhahabu na Hadithi Nyingine* na *Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine.* Kwa sasa ni mwalimu wa shule ya *Parklands Baptist* Nairobi. Mchango wake umekuwa hisani katika

**15. Elizabeth Barasa**

Barasa ni mzawa wa gatuzi la Kakamega japo amelelewa kaunti ya Busia. Amefundisha katika *shule ya msingi ya Otimong'* gatuzi ndogo la *Teso Kusini*. Alichangia katika uandishi wa diwani ya *Zawadi ya Baba na Hadithi Nyingine*. Ni mchanganuzi wa fasihi ya watoto. Barasa ni mtahini wa kitaifa katika somo la Kiswahili na Insha. Kwa sasa anafundisha katika *shule ya Angoromu*.